ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Sita – Tarehe 31 Machi, 2010

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti,(Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi) alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani muhutasari wa ripoti ya kazi za Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 3

Upandaji wa Miti Katika Manispaa ya Zanzibar

Mhe. Ali Abdalla Ali: (Kny: Mhe. Haji Mkema Haji): - Aliuliza :-

Miti mingi iliyopandwa katika Manispaa ya Zanzibar ambayo ilikuwa ni kivutio cha mji pamoja na kutia kivuli katika mji imekatwa katika maeneo mbali mbali. Mfano wa maeneo hayo ni Miembeni ambako Miembe yote imekatwa, na Kidongochekundu ambako michungwa imezeeka na mengine kukatwa.

(a) Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili mikakati ya Baraza la Manispaa juu ya mradi wa upandaji miti katika Manispaa ya Zanzibar?

(b) Baadhi ya miti iliyobakia katika Manispaa ya Zanzibar ni mibovu na inaanguka ovyo na kuhatarisha maisha ya binadamu mfano ni ile mivinje ya barabara ya kiembesamaki, Mwanakwerekwe. Je Baraza la

Manispaa litachukua hatua gani juu ya miti ili kuepusha ajali kwa wananchi wake?

Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake na 3 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Baraza la Manispaa huwa halikati miti ovyo isipokuwa kwa sababu maalum kama za kuhatarisha maisha ya watu na baada ya kupata kibali cha Taasisi husika. Hata hivyo, Baraza limejiandaa na limejiwekea mkakati wa kupanda miti 25,000 kila mwaka na linashiriki kila mwaka katika sherehe ya siku maalum ya mazingira Duniani kwa upandaji miti, Baraza kwa kushirikiana na Afisi ya Mkuu wa Wilaya kupitia kwa Madiwani linashiriki katika kampeni ya kuwahamashisha wananchi kupanda miti katika maeneo yao. Maeneo yaliopandwa miti katika kipindi cha karibuni ni kizingo, Kilimani, Botanic garden, Muungano na Mikunguni n.k.

b) Kwa upande wa miti mibovu hatua inayochukuliwa na Baraza la Manispaa ni kuiarifu Idara ya Misitu na Mazao ya Biashara na Matunda na hatua za kukata miti zinazochukuliwa mara tu baada ya kuthibitika miti inayohatarisha maisha ya binaadamu na kupatiwa kibali na Taasisi husika.

Nam. 55

Changamoto Katika Kilimo cha Mwani

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Kilimo cha Mwani ni maarufu hapa Zanzibar lakini kinakabiliwa na changamoto nyingi; mojawapo ni kuanguka kwa bei.

Je, Mhe. Waziri, Wizara inachukua hatua gani za kusaidia kuondoa tatizo hilo kwa lengo la kuwapa moyo wakulima hao?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 55. Lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba kwanza kuweka sawa hoja iliyotolewa kupitia swali hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kilimo cha mwani ni maarufu hapa Zanzibar lakini kinakabiliwa na changamoto nyingi. Hata hivyo, miongoni mwa changamoto hizo ni bei kuwa ndogo na sio kuanguka kwa bei.

Mhe. Mwenyekiti, kilimo cha mwani kinaendelea kuwa ni tegemeo muhimu kwa wananchi kujiongezea kipato chao katika vijiji vingi vya pwani ya Mashariki ya Zanzibar. Kuna aina mbili za mwani unaolimwa na kusafirishwa nje ya Zanzibar, aina hizo ni mwani mnene (cottonii) na mwani mwembamba (*spinosum*).

Mhe. Mwenyekiti, asilimia 92.16 ya mwani unaozalishwa ni mwani mwambamba, hali hii imesababishwa na uhimili wa mabadiliko ya hali ya hewa inayotokana na mabadiliko ya miongo hapa Zanzibar. Histoira inaonyesha kwamba mnamo mwaka 2000 bei ya mwani mwembamba ilianguka kutoka shilingi 120 hadi kufikia shilingi 50 kwa kilo, hii ilitokana na uzalishaji wa mwani huo kwa wakati ule uliongezeka sana katika nchi zinazozalisha kulingana na upatikanaji wa soko.

Mhe. Mwenyekiti, mnamo mwaka 2002 bei ya mwani mwembamba ilianza kuongezeka tena kutoka shilingi 100 hadi kufikia shilingi 160 mpaka sasa na baadhi ya makampuni hununua kwa bei ya shilingi 180.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia 7.84 iliyobaki ni ya mwani mnene ambao unaota kwenye maeneo maalum wakati wa kipindi cha baridi kuanzia mwezi (April – Septemba). Ingawa bei ya mwani mnene inabaki kuwa kubwa zaidi ambapo mnamo mwaka 1995 bei ya mwani ilianza kuongezeka kutoka shilingi 200 hadi shilingi 300 kwa kilo.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo uzalishaji wa mwani huo umekuwa ukipungua siku hadi siku kwa sababu wakulima ambao wengi wao ni wanawake wamekuwa wakivunjika moyo kutokana na uotaji wake kuathiriwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira miongoni mwa hatua ilizochukua katika kukabiliana na tatizo la bei ya mwani ni pamoja na:-

(a) Kwa kuwa bei ya mwani mwembamba ni ndogo na ni vigumu kuongezeka kwa sababu uzalishaji wa mwani huo ni mkubwa kulingana na mahitaji ya soko, Wizara kupitia mradi wa *MACEMP*

inaendelea kutoa miradi mbadala kwa wanajamii kama vile ufugaji wa samaki, kuku, mbuzi na kadhalika ili kuweza kuwasaidia katika kuongeza kipato chao na kuondokana na umasikini.

(b) Kuendelea na kutafuta Wawekezaji ambao wataweza kuwekeza katika kusarifu mwani hapa Zanzibar ili kuweza kuongeza thamani ya mwani wa Zanzibar.

(c) Tafiti mbali mbali zinaendelea kufanyika kupitia mradi wa *MACEMP* ili kuweza kutafuta mbegu ya mwani mnene (cottonii) ambayo itaweza kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa kuwa kilimo cha mwani mwembamba baada ya miezi sita kitakuwa hakionekani kutokana na matatizo ya uotaji wake.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni sababu zipi ambazo zinasababisha mwani huo kutokuota? Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijibu lile swali mama nilisema kwamba huu mwani moja katika tatizo lake kubwa ni kuwa uzalishaji umekuwa mwingi na unapokuwa uzalishaji ni mwingi na bei ni ndogo duniani, basi ina maana hilo ni moja katika tatizo. Lakini sikumbuki kusema kwamba baada ya miezi sita mwani huo utakuwa haupatikani tena hapa Zanzibar.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wakulima wa zao hili la mwani mara nyingi wamekuwa wakilalamikia bei ambayo inaonekana ni ndogo kuliko shughuli yenyewe na kwa kuwa hawa wafanyabiashara ambao wananunua zao hili, mara nyingi huwa wanalalamikia bei ya soko duniani.

Je, Mhe. Waziri wizara yake imefanya utafiti gani juu ya bei ya zao hili katika soko la dunia, ili kuwaeleza hasa kwa uwazi wananchi?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mjumbe aliuliza kuwa ni kwa sababu gani bei inaanguka na je wizara ina mpango gani wa kuweza kufanya utafiti au kufuatilia bei ya soko likoje duniani?

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na serikali kwa miaka miwili iliyopita kama sikosei, niliunda tume baina ya wizara yetu, wizara ya fedha na wizara ya biashara tukatuma ujumbe kwenda China ambao ndio wanunuaji wakubwa sana wa mwani. Kule walifanya kikao na ikaonekana kwamba kwa kweli hakuna tafauti kubwa sana ya bei za kule na hizo ambazo watu wetu wananunua hapa nchini.

Lakini pamoja na hayo wizara kama tulivyosema katika majibu yetu mama kwamba bado wizara inaendelea kufanya utafiti zaidi katika sehemu zote za dunia ili kuweza kutizama uwezekano wa kuwaongezea wakulima wetu wa mwani bei. Ahsante.

Nam. 70

Mhe. Zakiya Omar Juma: (Kny: Mhe. Rashid Seif Suleiman) – Aliuliza:-

(a) Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili uwiano wa vikalio na idadi ya wanafunzi katika Skuli za Serikali katika Wilaya za Unguja na Pemba?

(b) Je, wizara inachukua hatua gani za kurekebisha uwiano huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 70 lenvye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba skuli zetu nyingi zinaupungufu wa vikalio kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi na licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo machache hayo niliyotoa, sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti skuli zetu za msingi na sekondari zina jumla ya wanafunzi 287,469 ambapo idadi ya madawati yaliyopo katika skuli hizo ni kama ifuatavyo:

i) Madawati ya mwanafunzi mmoja mmoja yako 8,248.

ii) Madawati ya wanafunzi wawili wawili yako 3,271 na

iii) Madawati ya wanafunzi watatu watatu yako 37,743.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ni madawati 49, 262. Mhe. Mwenyekiti, madawati haya yanatumiwa na wanafunzi 128,019 kwa mkondo

mmoja mmoja na wanafunzi 256,038 kwa mikondo miwili. Kwa hivyo, utaratibu wa mikondo miwili ya masomo, jumla ya wanafunzi 31, 431 wanahudhuria masomo bila ya kuwa na vikalio katika madarasa yao.

Mhe. Mwenyekiti, uhaba wa vikali upo katika takriban katika skuli za wilaya zote kwa Unguja na Pemba. Lakini wilaya zenye upungufu mkubwa ni Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi ambazo ndizo zenye wanafunzi wengi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara siku zote inahakikisha kuwa kuna uwiano baina ya skuli na skuli na wilaya na wilaya katika ugawaji wa madawati. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inatumia fedha za bajeti na fedha za wahisani mbali mbali katika kuchonga madawati na kuyasambaza maskulini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kwa mwaka 2009/2010 wizara imechonga jumla ya madawati 1,350 kwa kutumia fedha za bajeti ya serikali na madawati 1,640 ni kutokana na fedha zilizotolewa na Shirika la Kimataifa la Msaada la Swiden. Meza na viti 2600 kupitia Shirika la Msaada la Maendeleo ya Kimataifa la Kimarekani USA.

Mhe. Mwenyekiti, madawati hayo yamegaiwa katika skuli za wilaya zote kwa kuangalia mahitaji ya skuli mbali mbali, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali swali langu kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna skuli ambazo hazina, sisemi madawati lakini nasema vitu vya kukalia, kwa sababu madawati ni kitu kimoja, kiti si dawati. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna skuli ambazo ukosefu huu upo zamani sana kuliko skuli nyengine zinazopewa hayo madawati.

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kuwacha skuli zilizokosa vikalio zamani na zikapewa skuli zilizokosa vikali karibuni?
(b) Je, zile skuli ambazo hakuna hata kiti na meza ya mwalimu hazionekani kama kuna haja ya kuonekana mwanzo?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali mama kwamba vigezo vinavyotumika zaidi ni mahitaji ya maeneo ambayo yanaupungufu. Hivi karibuni tumekuwa tukigawa madawati hayo kwa kuzingatia vigezo hivyo na hivi sasa tuna zoezi la kugawa

madawati katika skuli mbali mbali zikiwemo hizo za Pemba, ambapo hivi sasa nadhani kuna madawati au vikalio pamoja na meza karibu 900 zinapelekwa Pemba na skuli za Unguja takriban kuna vikalio karibu 800 ambavyo sasa hivi tunagawa.

Kwa hivyo, kama kuna skuli ambazo hazina kabisa na zimekosekana, basi nadhani Mhe. Mwakilishi atujulishe ili tuweze kufanya utaratibu wa kuweza kuzigaia hivyo vikalio. Mhe. Mwenyekiti, kwa hizo skuli ambazo hazina viti hata meza pia namuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane basi ili tuone nazo zinapata hizo meza na viti angalau kwa mwalimu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri hapa katika jibu alilomalizia amesema kwamba kuna madawati yapatayo 900 ambayo yanataka kugaiwa katika skuli mbali mbali za Pemba.

(a) Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua hasa utaratibu walioupanga ni skuli ipi na ipi wataipelekea madawati hayo?

(b) Kwa mujibu wa majibu aliyomalizia sasa hivi. Kwa hivyo, atakubaliana na mimi kwamba hawana utafiti wanaoufanya wa kujua ni skuli ipi na ipi ambazo hazina madawati, kutokana na kwamba wanaomba sasa msaada kutoka kwa Mhe. Mohamed Ali Salim

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilijibu kwamba kuna vikalio karibu 900 vinapelekwa Pemba. Lakini kwa bahati mbaya orodha ya hizo skuli sasa hivi sina, nadhani akihitaji nitampatia haraka inavyowezekana.

Lakini kuhusu utafiti. Nadhani katika jibu langu mama nilieleza kwa kina skuli pamoja na madawati yaliopo, inaonesha dhahiri kwamba tumefanya utafiti na kuona kuwa katika skuli gani na gani madawati hayo hayapo. Ndio maana tumetoa takwimu hizo tumejua hasa madawati yako mangapi na mangapi yanahitajika kwa hivi sasa. Kwa hivyo, utafiti tumeufanya.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi wanayoichukua katika kuhakikisha watoto wetu wote wanapata vikalio maskulini.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na matatizo ambayo yanaonekana ya vikalio vya watoto. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba suala la wanafunzi kukaa chini kwa kweli halipendezi, lakini linakuwa halipendezi zaidi pale ambapo wanafunzi wa skuli za sekondari wakikaa chini.

Je, wizara yake ina mkakati gani wa makusudi ili kuhakikisha wanafunzi wote wa skuli za sekondari wanapata vikalio?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba suala la wanafunzi kukaa chini halipendezi. Mhe. Mwenyekiti, mikakati tuliyonayo hivi sasa ni kuhakikisha kwamba kila tunapojenga skuli, basi tunaweka na madawati na hili tayari tumeshaanza kulifanya katika skuli mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hayo pia tuna utaratibu hivi sasa wa kumega au kutenga fedha za serikali kwa ajili ya kutengeneza madawati na hiyo kazi tayari tumeshaanza. Kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba tumetumia fedha ya serikali mwaka jana kutengeneza madawati kwa yale madarasa ambayo hayakubahatika wakati yalipojengwa kuwekwa madawati.

Nam. 90

Starehe Club

Mhe. Ame Ussi Juma: (Kny: Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu) - Aliuliza:-

Starehe Club ilianzishwa kuwa ni sehemu ya burudani na mapumziko na ilikuwa inatosha wakati ilipoanzishwa kulingana na wakati na idadi ya watumiaji wa wakati ule. Lakini sehemu hiyo sasa inaonekana ni ndogo na haitoshi kwa mazingira ya sasa. Vile vile inatumika kinyume na matarajio kama eneo la maficho ya vibaka na wala unga.

(a) Mhe Waziri, kwa sababu ya udogo wa jengo la Starehe Club, na kwa kuwa shughuli za utalii zinakua kwa kasi; na kwa kuwa bado Starehe Club ipo chini ya dhamana na umiliki wa Serikali; kwanini Serikali isipange kupanua sehemu hiyo na kuongeza shughuli za biashara kwa ajili ya kukuza uatalii kuliko kupaacha pakatumika kama maskani ya wala unga na vibaka?

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwaondoa vibaka wazoefu na wavuta unga wanaoendesha shughuli zao katika eneo la Starehe Club?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 90 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Starehe Club ilianzishwa ni sehemu ya burudani na mapumziko na hadi sasa inaendelea kutumika kwa madhumuni hayo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kwamba, wakati tukisubiri uamuzi wa mwisho wa Serikali juu ya hatma ya Club hii, ukumbi wa Starehe Club kwa sasa umekodishwa kwa mfanyabiashara kwa ajili ya kufanya biashara ya chakula, vinywaji na bidhaa za kazi za mikono na si vyenginevyo. Mfanyabiashara huyo amekodishwa kwa mkataba mfupi wa mwezi mmoja mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Eneo la Starehe Club kwa hakika halikidhi hasa mahitaji ya ilivyotarajiwa, lakini linatumika kwa kazi hiyo iliyokusudiwa kama nilivyosema. Isipokuwa eneo hilo linatumika nusu tu na nusu halitumiki, kwa sababu ya kuwepo burudani nyingi katika eneo hilo na kushindwa kushindana na wengine ambao wako katika eneo hilo.

(b) Eneo la Starehe Club si maficho ya walaunga na vibaka, lakini eneo la nje ya Starehe Club kuna eneo la wazi ndilo ambalo linatumika na watu wa aina hiyo, lakini sio ndani ya Starehe Club.

Mhe. Juma Duni Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, kiasi mara mbili nimemsikia akisema anasubiri uamuzi wa mwisho kuhusu Starehe Club. Ninavyokumbuka uamuzi wa huwa ni waraka unaopelekwa Baraza la Mapinduzi ili kufanya maamuzi.

Kwa maana hiyo je, waraka umepelekwa na Baraza halijaamua au *minute* imepelekwa kwa Rais hajatoa maamuzi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka kwamba eneo lote la kelele *square*, mambo msige na ukanda mzima mpaka Starehe Club alipewa mwekezaji, mwekezaji huyu alichukua muda mrefu kulitumia na baadae eneo hili likachukuliwa kutoka mikononi kwa mwekezaji yule. Lakini kwa muda wote Starehe Club ikiwa chini ya Shirika la

Utalii tulizuiliwa kufanya uwekezaji wa kudumu na ndio maana tukakodisha kwa mwezi mmoja mmoja.

Kwa hivyo, hatima ya suala hili liko kwenye mikono ya wizara inayoshughulikia ardhi na ujenzi na hasa Mji Mkongwe. Kwa hivyo, sisi tunasubiri wao watuambie lile eneo limepangwa kwa madhumuni gani.

Nam. 92

Jengo la Ofisi ya ZSTC Dar – es - Salaam

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: (Kny: Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi) - Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa Ofisi ya Shirika la ZSTC iliyoko Dar – es Salaam haiko katika hali nzuri, huoni kuwa iko haja ya kufanya utaratibu wa kulipata jengo ambalo linatumiwa na Ofisi hiyo kisheria ili likarabatiwe upya na kutoa nafasi nzuri zaidi itakayotoa mandhari nzuri kikazi na kuliongezea pato Shirika?

(b) Kwa kuwa suala hilo limekuwa likifanyiwa kazi kwa karibu miaka mitatu sasa bila ya mafanikio, Je, Mhe. Waziri ni kipi kikwazo kinachosababisha hali hiyo?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 92 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji imeona umuhimu wa Tawi la Shirika la ZSTC la Dar as Salaam kupatiwa Hati Miliki ili liweze kulifanyia ukarabati jengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua za kufuatilia suala hilo Wizara ya Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji bado inaendelea na mazungumzo na wahusika, yaani Wizara ya Ardhi na Nyumba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuatilia suala hilo la hiyo nyumba ambayo ZSTC wanaitumia.

Mhe. Mwenyekiti, Mazungumzo yanaendelea vizuri na kwamba pande zote zimekubaliana kimsingi kukamilisha hatua zilizobakia. Ni tegemeo letu kuwa mara baada ya kukamilika kwa hatua zilizobakia jengo hilo lita kabidhiwa kwa Shirika la ZSTC na kwa maana hiyo, litakabidhiwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi ametueleza kwamba suala la jengo la ZSTC lilioko Dar-es-Salaam liko chini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Nyumba na hivi sasa wamefanya mazungumzo ambayo yanaendelea na vile vile ametueleza kwamba kuna hatua ambazo bado zimebakia.

Je, Mhe. Waziri ni hatua gani ambazo zimebakia zenye kuhitaji utekelezaji na lini tunategemea kukamilika hatua hizo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, katika mazungumzo kuna mambo mengi, yaani hatua nyingi zinazungumzwa. Lakini katika jengo lile za *ZSTC* hawapo peke yao, wako wapangaji wengine ambao wana muda kabla ya kutoka ndani ya nyumba ile.

Kwa hivyo, hatua zilizobaki ni kusubiri wapangaji wengine wamalize mikataba yao na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Nyumba, halafu *ZSTC* ndipo wahalalishiwe jengo lile. Kwa maana hiyo, sitaweza kumwambia hapa lini tunatarajia kukabidhiwa jengo lile, lakini matumaini yetu kwamba haitachukua muda mrefu kukabidhiwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa muda mrefu Wajumbe wako wamekuwa na kilio kikubwa juu ya deni la *ZSTC* kwa serikali.

Hivi sasa tayari *ZSTC* wameshalipwa deni lile na kwa kuwa nyumba ilioko Dar-es-Salaam ni mzigo mkubwa kwa sababu kodi ni kubwa inayolipwa. Kwa nini hatuamui kuachana na nyumba hiyo na kujenga nyumba mpya kwa ajili ya afisi ya kisasa ya *ZSTC*.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Mjumbe amechanganya maswali mawili kwa moja, lakini nitajibu moja ambalo linalohusu nyumba hii.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kujibu katika Baraza lako tukufu kwamba *ZSTC* baada ya kupata fedha ingeweza kujenga nyumba nyengine tukaachana na hii. Lakini aina ya biashara inayofanywa na *ZSTC* pale Dar-es-Salaam inafaa sana kwa eneo lile ambalo wapo, vyenginevyo hivi sasa *ZSTC* wakatafute kiwanja Kimazichana, yaani nje sana ya mji ndiko viwanja viliko. Kwa hivyo, si vizuri kujenga kule wakati biashara ile inafanyika vizuri pale katikati ya mji, yaani ni eneo na aina ya biashara inavyofanyika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Wakati jengo hilo tunasubiri maamuzi na kukabidhiwa kwa *ZSTC*. Je, Mhe. Waziri hili jengo tunataka kupewa bure au kuuziwa. Ikiwa tunataka kuuziwa ni kiasi gani cha fedha zinatakiwa kwa jengo hilo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa kwa sababu hatujafikia mwisho wa mazungumzo hatujajua nyumba ile kama tutauziwa au tutakodishwa kwa muda mrefu. Kwa hivyo, nitashindwa kusema nyumba ile tutauziwa kwa kiasi gani. Lakini hakika hatutapewa bure kwa sababu sio mali yetu.

Nam. 100

Leseni za Biashara

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui – Aliuliza:-

Hivi sasa kuna utitiri wa taasisi za kutoa leseni Zanzibar na taasisi hizo hufanya leseni kuwa ndio njia ya mapato.

(a) Mhe. Waziri huoni kuwa hii sio njia sahihi ya kudhibiti na kurekebisha biashara na wafanyabiashara.

(b) Huoni kwamba wingi wa taasisi zinazotoa leseni unachangia kupoteza mapato ya serikali.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna taasisi nyingi zinazotoa leseni za kuendeshea biashara hapa Zanzibar zikiwemo Baraza la Manispaa, *ZRB*, Kamisheni ya Utalii, *ZIPA*, Halmashauri za Wilaya na nyenginezo.

Kutokana na hali hiyo wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Mrajis Mkuu wa pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi inaendelea na mchakato wa kufanya mapitio ya sheria ya utoaji wa leseni.

Lengo ni kuweka mfumo mzuri zaidi wa utoaji leseni za biashara, ambapo leseni zote za kuendeshea biashara zitatolewa katika mfumo utakaoonekana unafaa, ili kudhibiti mapato, kuondosha usumbufu kwa wafanyabiashara, kwa

kuondoa urasimu wa upatikanaji wa leseni pamoja na kuweka takwimu za uhakika na taarifa zao za kibiashara. Kazi hii inafanyika chini ya Mradi wa *BEST* kwa ufadhili wa Benki ya Dunia na inaendelea vizuri.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba haionekana kama litakuwa jambo la busara kuweka ukusanyaji wa fedha katika chombo kimoja. Lakini kwa kuwa fedha hizi taasisi zinazozikusanya huwa zinazitumia kwa kuendeleza shughuli zilizomo kwenye taasisi zao. Kwa hivyo, haionekani baada ya kukusanywa na hicho chombo kimoja baadaye kila taasisi iliyokuwa ikikusanya fedha ile wakarejeshewa, kwa ajili ya kuendesha shughuli zao katika taasisi.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika jibu mama kwamba tunaangalia mfumo utakaofaa kwa ajili ya kuendesha jambo hilo. Kwa kweli si wazo baya ambalo limetolewa na Mhe. Mjumbe na *system* aliyoizungumza ni ile ya *retention*. Kwa maana hiyo, inawezekana kabisa katika kila taasisi ambayo iliwajibika kupata fedha hizi wakarejeshewa asilimia fulani ya fedha kwa lengo la kuendeshea kazi zao.

Nam. 21

Hali ya Usafi katika Wodi za Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Denge Makame – Aliuliza:-

Mazingira ya usafi katika baadhi ya Wodi za Wagonjwa katika Hospitali ya Mnazimmoja usafi wake hauridhishi hasa magodoro yake ambayo yamechakaa.

Je. Mhe. Waziri, wizara yako inachukua hatua gani za haraka kurekebisha hali hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibu swali nichukue fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kukalika kitu hicho kitukufu na hii ni ishara kwamba akina mama tunaweza. Vile vile nipongeze Uongozi wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweka akina mama wawili ambao ni Makatibu Mezani. Kwa hivyo tunapongeza sana na leo ni mambo mazuri humu Barazani *(Kicheko/Makofi)*.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi baadhi ya vifaa vya Hospitali ya Mnazimmoja ni vichakavu yakiwemo baadhi ya magodoro, vitanda pamoja na vifaa muhimu vya kutendea kazi. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Idara ya Hospitali ya Mnazimmoja kimsingi imeliona suala hilo na mengineyo, imo mbioni kurekebisha hali hiyo ikiwemo kufanya taratibu za kutia *covers* mpya magodoro pamoja na kutafuta fedha za kununua magodoro mapya.

Aidha katika kuimarisha haiba ya Hospitali hiyo ya Mnazimmoja imeanza hatua za kuzipaka rangi wodi zote na hali ya fedha inaporuhusu itaendelea kutatua tatizo moja baada ya moja hatua kwa hatua.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Katika kujua kero na mapungufu mbali mbali dhidi ya wagonjwa wetu kwenye wodi hizo. Je, Mhe. Waziri anafanya ziara mara ngapi kwa mwaka, ili kujua mapungufu na kero mbali mbali zilizotokea ndani ya wodi hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka ziara naweza kufanya hata mara 40 kwa mwaka katika Hospitali yetu ya Mnazimmoja pamoja na maeneo mengine. Kwa sababu Hospitali ya Mnazimmoja ndio kioo cha Wizara ya Afya na mahala pale hutakiwi kupanga utaratibu maalum, yaani kila tunapohisi kwamba twende Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya kuangalia kero mbali mbali basi tunakwenda *(Makofi)*.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti tunakwenda mara nyingi sana na wala hatujaweka kumbukumbu, lakini utaratibu tuliojipangia kila wakati kutembelea hospitali hiyo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nami niwapongeze Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa jitihada ambazo wanachukua kuona kwamba wanabadilisha baadhi ya vitu ambavyo ni vikongwe, kwa mfano vitanda na magodoro kwa ajili ya wagonjwa wetu.

Swali langu ni kwamba hivi karibuni niliwahi kutembelea eneo la Hospitali ya Mnazimmoja na kuona vitanda vingi vikongwe ambavyo vimewekwa sehemu. Sasa hali ile kwa mujibu wa Sheria za Serikali hasa ya Fedha na Manunuzi ni mali ya umma.

Je, utaratibu wao uko vipi kwa vifaa kama vile, yaani utaratibu wa kuviuza au kupiga mnada na watu kuweza kununua, ili mali ya serikali isiweze kuharibika namna kama ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba vipo vitanda kama hivyo ambavyo vinakuwa vikongwe huwa vinawekwa mahala. Utaratibu unaotumika huwa vinaangaliwa vile vilivyokuwa afadhali kidogo basi kufanyiwa ukarabati, kupakwa rangi na baadaye kurejeshwa kwenye wodi, ili viweze kusogeza siku huku tunatafuta nyengine.

Hata hivyo, kwa vile vilivyochaa sana utaratibu wa kupigwa mnada pamoja na kuuzwa upo. Kwa hivyo, kama vipo basi tutawahimiza wahusika, ili walifanye hilo jambo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mimi naelewa kwamba si kwa makusudi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuviacha vitanda na magodoro kuwa vibovu na wala havipendezi. Lakini hata hivyo wizara hutakiwa ifanye juhudi ya kuomba fedha serikalini pamoja na kwa wafanyabiashara, kwa ajili ya kuondoa kadhia hiyo.

(a) Je, Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii kwa mwaka 2009/2010 imetenga kiasi gani ili kupunguza tatizo hilo.

(b) Kwa upande wa wafanyabiashara wizara ipange utaratibu wa kuwapelekea barua za maombi, kwa ajili ya kutoa msaada katika hospitali hii, iwe inapendeza mapaa pamoja na vitanda, maana mapaa mazuri, lakini vitanda na magodoro havipendezi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kutenga fedha kiasi gani ni vigumu hivi sasa kumwambia kwa mara moja. Lakini napenda nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba bajeti ijayo tutaweka kifungu kizuri sana, kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda vizuri yakiwemo magodoro pamoja na vitanda.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tumepata vitanda pamoja na magodoro 10 vyote vipya kutoka *NMB* kupitia Mhe. Mohammed Ibrahim Sanya ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe alifanikisha suala hilo *(Makofi)*.

Vile vile tumepata vitanda pamoja na magodoro 22 vyote vipya hivi karibuni kutoka Kitengo cha *Family Planning* tunamshukuru sana Dk. Hanuni Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, vyote hivyo tumeviweka kwenye Wodi ya Wazazi. Kwa kweli suala hili tunalifanyia kazi na tukijaaliwa tutafanikiwa *(Makofi).*

Nam. 22

Maabara ya PHL, Pemba

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Maabara ya *PHL* iliyopo Pemba, ni sehemu inayotumika kwa tafiti mbali mbali za magonjwa. Iwapo maabara hii itatunzwa vizuri, bila ya shaka itawasaidia wananchi wetu kufahamu matatizo mbali mbali ya maradhi yanayowakabili.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa kuzingatia umuhimu wa maabara hii, wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maabara hiyo inawasaidia wananchi wetu ipasavyo?

(b) Je, kuna wataalamu wangapi wanaofanya kazi katika maabara hiyo?

(c) Kwa kuzingatia tatizo la kukimbiwa na wataalamu kutokana na ufinyu wa maslahi. Je, serikali ina mikakati gani kuhakikisha wataalamu waliopo wanalipwa vizuri, ili waendelea kuhudumia maabara hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti kwa idhini ya yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye vifungu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa maabara hii katika kuwasaidia wananchi, wizara kupitia *PHL* na kwa kushirikiana na wadau imefanya tafiti (*Operational Researches*) na kuibua miradi mbali mbali iliopelekea utoaji wa huduma kwa jamii, huduma hizo ni pamoja na:-

- Mradi mkubwa wa maji umetekelezwa kwa awamu mbili, ambazo zimepelekea ukarabati wa visima, uwekaji wa bomba mpya za maji, hivi karibuni mradi wa maji wenye jumla ya shillingi millioni 270 ulizinduliwa Wilaya ya Chakechake ikiwa ni sehemu ya mradi huo.

- Hivi sasa chini ya mradi huu wa maji, walimu kutoka skuli 35 za Pemba pamoja na jamii iliyozunguka skuli hizo wanafaidika na elimu juu ya maji salama (*Safe Water*), ambayo inatoa uelewa juu

ya madhara ya kutumia maji yasiosalama na mbinu za kuepuka madhara hayo.

- Uchunguzi wa maradhi ya Kifua, *PHL* inatumiwa kama maabara ya rufaa kwa uchunguzi wa kifua kikuu na makohozi (*Sputum)* kutoka hospitali za Unguja na Pemba huletwa hapo kwa uchunguzi wa upandikizwaji (*Culture).*

- Utafiti wa Maradhi ya Kipindupindu, Chanjo ya Maradhi ya Kipindupindu uliotolewa kwa vijiji vya Chumbuni, Karakana na Mtopepo kwa Unguja na Kengeja, Mwambe na Kojani kwa Pemba.

- Minyoo na Kichocho, tafiiti zilizofanywa zimedhihirisha kuwepo kwa kiwango kikubwa cha Kichocho na Minyoo miongoni mwa wanafunzi wa skuli za Pemba na baadhi ya zile za Unguja. Hivi karibuni 15/02/2010 litafanyaika zoezi la upimaji wa mikojo kwa skuli za Unguja na Pemba, zoezi ambalo litaambatana na utoaji wa dawa za kichocho na Minyoo kwa wanafunzi husika.

- Katika mwezi huu wa Januari *PHL* imeanzisha uchunguzi wa maradhi mbali mbali, ambayo hayawezi kufanyika katika Hospitali za Wilaya na kwa sasa madaktari wanapeleka na *Specimen PHL* kwa uchunguzi.

- *PHL* ni taasisi Shirikishi ya Shirika la Afya Duniani. (*Word Health Colarating Center*), jambo ambalo ni faida kubwa kwa jamii ya Kizanzibari, kwani imekuwa ni rahisi kupata misaada ya kiafya na kijamii kutoka katika shirika hilo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuna wataalamu 20 wazalendo wa taaluma mbali mbali, ina wataalamu 6 wa muda mrefu kutoka nje na pia kuna wataalamu wengi kutoka nje huwa wanakuja kwa vipindi vifupi vifupi kulingana na muda wa miradi wanayoifanyia kazi.

(c) Kwa bahati nzuri *PHL* tatizo la kukimbiwa na wataalamu sio kubwa. Hata hivyo, serikali kupitia wizara yangu iko makini sana kuona kuwa wataalamu waliopo hawakimbii kwa kupewa motisha mbali mbali ikiwa ni pamoja na :-

(i) Kutoa fursa mbali mbali za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi.

(ii) Kuboresha maslahi yao kwa kuwapa marupu rupu (*Top up Allowance*) kutoka katika miradi inayoibuni au kuendeshwa hapo katika maabara.

Mhe. Ame Ussi Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. katika jibu lake mama amesema kwamba tuna wataalamu 6. Je, haoni kwamba ipo haja kuongeza wataalamu wengine kwa sababu jamii kila siku inakua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kweli tumesema kwamba tunao wataalamu 6 hivi sasa kutoka nje. Lakini wapo wataalamu wengine wa ndani na mbali ya hao wanaokuja na kurudi. Kwa hivyo, hivi sasa idadi hii inatosha na tutakapoona kuna haja ya kufanya hivyo, basi ushauri wake tutaufanyiakazi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naomba niongeze kidogo baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. kwanza wataalamu wazalendo ni 20 na hawa 6 ni wataalamu wa kigeni, ambapo kuna miradi kwenye *PHL* inafanyika pale. Kwa hivyo, hawa wataalamu 6 wamekuja na miradi yao.

Kwa mfano Dk. Kamala, Dk. Ben na Dk. Lorenz wao wanafanya Mradi wa *Cholera* na *Typhoid*, Dk. Sunil na Dk. Muthu wao ni kutoka *John University* wanafanya Mradi wa Malaria, *TB* na *HIV* na Dk. Jovern yeye ni mtaalamu wa *HMIS*. Kwa hivyo, pengine wataalamu wa kigeni wataongezeka kwa mujibu wa miradi iliyokuwepo *PHL*, lakini wazalendo wapo na wanafanyakazi zao bila ya matatizo na tunaendelea vizuri *(Makofi).*

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwamba tunao wataalamu kutoka nje. Lakini juzi Mhe. Mjumbe alipokuwa akiuliza swali kuhusu *Ultra Sound* alitwambia wapo wataalamu na wanawasomesha wazalendo. Je, kwa mradi huu ambao ameuzungumza Mhe. Waziri wa *PHL* hawa wataalamu hawawafundishi walazendo tulionao.

Vile vile nimevutika kwamba wataalamu hao wanayo miradi tofauti ikiwemo *Cholera* katika utafiti maana yake *Cholera* bado inaendelea mtaalamu huyu amefikia hatua gani. Kwa sababu *Cholera* haipungui Zanzibar na inakuja vipindi ambavyo havitabiriki, yaani si Masika wala Kaskazi *Cholera* ipo. Je, katika uchunguzi wake mtaalamu amefikia hatua gani.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli swali la Mhe. Mjumbe ni kubwa sana. kwanza je hawa wananchi wa Zanzibar wanafaida, wanafaidika sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu wale wataalamu waliopo pale wanafanyakazi sambamba na wafanyakazi wetu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa hivyo wanatoa taaluma ya moja kwa moja.

Vile vile tunawapeleka wafanyakazi wetu kusoma nchi za nje kutoka *PHL*. Kwa mfano, hivi sasa wengine wako *London School of Higgins and Tropical Medicines* wanafanya *PhD*, wengine tunaowapeleka. Italy na sehemu nyengine mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, hii kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni *Word Health Colarating Center* (*WHO*), kila baada ya muda wanakuja wanafunzi kutoka dunia nzima pamoja na walimu wao na Wataliana na wengineo ni kama Kituo cha kuwasomesha wataalamu kutoka nje na ndani ya Zanzibar. Kwa hivyo, taaluma inakwenda vizuri.

Kuhusu *Cholera* tumetoa chanjo kwa baadhi ya maeneo kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hawa wataalamu wetu wanaangalia vipi nguvu ya chanjo zile namna gani zinafanyakazi mpaka leo wote waliopata chanjo hawajapata *Cholera*. Isipokuwa *Cholera* wamepata wale ambao hawakupata chanjo. Kwa maana hiyo, tunafanyakazi vizuri na tunaendelea bila ya matatizo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, ni kweli jitihada za waziri na wizara kwa jumla ni kusomesha wataalamu ni kubwa na inaonekana. Vile vile jitihada za kuwapa mafunzo ya ndani nayo inaonekana. Lakini tatizo kubwa ni maslahi ya wafanyakazi hao na kwa sababu hivi sasa wanafanyakazi katika miradi basi twabaan kuna kitu kidogo ambacho wanapata pamoja na mshahara wao.

Je, Mhe. Waziri wizara yake imejipanga vipi kuona kwamba inajitayarisha kwa maslahi ya kutosha kwa wafanyakazi hawa, ili miradi hii ikimalizika wawe na moyo wa kufanya kazi Zanzibar au vyenginevyo watakwenda pahala ambapo kuna hali nzuri ya kimaslahi.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, pale Maabara ya *PHL* wapo wafanyakazi wa aina mbili, yaani wapo wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na pia tunao wafanyakazi ambao tumewaajiri kwa mujibu wa miradi inavyoendelea. Sasa unapokuja mradi wale wafanyakazi ambao hawakuajiriwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wanapata *allowance* au malipo maalum kwa mujibu wa ule mradi, na wale wa Wizara ya Afya tunawalipa mshahara wao na top *allowance* juu, yaani wanapata marupurupu kwa mujibu wa ule mradi uliokuwepo pale. Kwa hivyo,

wanafaidika na isitoshe tumeshatayarisha *scheme of service* na tumeshaipeleka serikalini na wote hawa utaalamu wetu wamezingatiwa na mambo yakiwa mazuri na wao watafaidika.

Nam. 57

Matengenezo ya Uwanja wa Amani

Mhe. Ame Ussi Juma (Kny: Mhe. Ali Abdulla Ali) - Aliuliza:-

Uwanja wa Amani umefanyiwa matengenezo makubwa ya mfano na hivi sasa unapendeza sana kama mpya.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa umeme wetu ni wakukatika katika suala la genereta la dharura kwa matumizi ya uwanja limezingatiwa.

(b) kitaifa Kwa kuwa pia Uwanja wetu huwa tunafanyia sherehe mbali mbali za na gwaride. Je, suala hili limezingatiwa ili uwanja wetu usiharibike mapema.

(c) Je, Hoteli ya Uwanja wa Amani itahusika na matengenezo ya uwanja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nichukue fursa hii kukupongeza kwa dhati kabisa kwa kiti ulichokikalia ambacho naweza kusema ni kiti ambacho kimekuchukua vizuri na Mwenyezi Mungu akuzidishie na akuondoshee hasada.

Pia napenda kukupongeza wewe pamoja na gazeti letu la Zanzibar leo likiwa na picha yako ukurasa wa mbele kabisa likiwa limekutoa kwenye kiti hicho ulichokikalia. Hongera sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 57 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Uwanja wa Amaan umefanyiwa matengenezo makubwa na unapendeza sana kama uwanja uliozaliwa upya na unaweza kushindana na viwanja vyengine vingi vilivyokuweko ulimwenguni.

(a) Mhe. Mwenyekiti, bila kujali tatizo la umeme lililojitokeza hivi karibuni katika mpango wa matengenezo ya Kiwanja cha Amaan pamoja na mkataba ambao tuliosainiana na Serikali ya Watu wa China ulihusisha na uwekaji wa jenereta la dharura kwa matumizi ya Uwanja

wa Amaan na hilo jenereta tayari sasa hivi limeshawekwa na limeshaanza kufanyiwa majaribio mbali mbali kwa kuwasha hizo taa nyakati za usiku.

Mhe. Mwenyekiti, ninafuraha kulijuulisha Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa uwanja upo katika ngazi ya mwisho ya makabidhiano kati ya Serikali ya Watu wa China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wakati wowote tunatarajia kutoa tarehe ya kufungua rasmi uwanja huo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ukweli kuwa kucheza gwaride na kupitisha magari mazito katika Kiwanja cha Amaan kulichangia sana kuharibu majani ya kiwanja pamoja na mpira wa kukimbilia yaani (*titan*) ambao mchezo wa resi za mbio ulikuwa ukifanywa katika mpira huo, hivi sasa uwanja umeshawekewa *titan* mpya kabisa ambao wanasema wataalamu katika Afrika ya Mashariki na Kati ndio *titan* ya mwanzo tena kuwekwa kwa sababu ina *layer* tatu hiyo *titan* iliyokuweko hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inatafuta njia mbadala ya kuona kuwa inatafuta sehemu nyengine yakufanyia sherehe mbali mbali za kitaifa zinazoshirikisha gwaride na matumizi ya magari mazito. Imeundwa kamati rasmi na wizara yetu ya kutazama maendeleo mbadala pamoja na kutafuta sehemu hiyo ambazo sherehe hizo zitatarajiwa kufanyika na maeneo mbali mbali yameshaanza kutazama ikiwemo eneo la Maisara.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Hoteli ya Uwanja wa Amaan haikuhusishwa katika matengenezo hayo ya mkataba na Serikali ya Watu wa China au mkataba wa uwanja uliofanyiwa kwa msaada huo. Hata hivyo, Serikali inafanya mpango mwengine wa kuhakikisha kuwa Hoteli ya Uwanja wa Amaan inafanana na mazingira ya uwanja wenyewe na hivi sasa tayari wizara imeanza mazungumzo na wawekezaji binafsi wenye uwezo wa kuiendesha hoteli hiyo kibiashara, bado tunawakaribisha wawekezaji wengine wenye nia ya kutaka kuiendesha hoteli hiyo kibiashara.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niipongeze hoteli hiyo jinsi ya matengenezo yalivyo na nimeshuhudia kwa sababu nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na pia niwapongeze wizara kama hii kule Tanzania Bara nao wamefanya uwanja mzuri unafanana na wetu lakini wao mzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu zaidi lilikuwa ni habari ya umeme na nasikia sina hakika kwamba unapoendesha mchezo hasa nyakati za usiku umeme mwingi unakwenda na gharama inakuwa kubwa sana, na ukizubaa hupati faida unapoendesha mchezo huo.

a) Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa siku kama mchezo unakuwa wakati wa usiku uwanja wetu utatumia *kilo watts* ngapi za umeme na zitakuwa na malipo ya kiasi gani.

b) Kama uwanja huu utakuwa unabeba uzito wa watu ambao hawatolingana na gharama za umeme utakaokwenda. Je, itakuwa ipo haja ya kuendesha mashindano ya mpira wa miguu nyakati za usiku kwa kiwanja chetu cha Amaan.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunashukuru pongezi zimetufika bahati nzuri leo timu yangu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo nzima ipo hapa ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi wa Michezo pamoja na Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo ambaye pia alikuwa Meneja wa Uwanja wa Amaan. Kwa hiyo pongezi hizo naamini mheshimiwa zimefika na sisi tunaishukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa sababu imekuwa na mashirikiano ya karibu mno na wizara yetu katika kipindi chote hiki pamoja na ripoti hii ambayo tumeipokea na tutaijadili baadae.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hizi taa zilizowekwa hapa kila *bulb* wanasema inatumia *kilo watts 2000* kila *bulb* moja na pale kuna *bulb* zaidi ya 80. Kwa hiyo ni *kilo watts* za kutosha lakini kwa gharama za kuwasha taa kwa haraka haraka ni kati ya shilingi laki tatu hadi laki nne kwa mchezo mzima kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa mchezo, zikiongezeka zile dakika 90 kwa dakika 30 nyengine pamoja na upigaji *penalt*, kwa hivyo gharama hizo zinaweza kufikia shilingi laki tano kwa umeme wakati huo.

Naamini uwanja huo hautokuwa unatumika kwa michezo midogo midogo nyakati za usiku ila zile mechi kubwa kama vile Yanga na Simba au mechi za timu za nje zitakapokuja kucheza na sisi katika Kombe la Mabingwa Afrika. Nasikitika sana kwamba Zanzibar tumekosa nafasi ya kutosha ya kuwaona wenzetu wa Mafunzo na Miembeni mwaka huu wakicheza mechi za Kombe la Shirikisho na Kombe la Club Bingwa Afrika kwa sababu mechi hizo zote zilifanyika Dar es Salaam.

Lakini kwa kipato kilichopatikana kwa siku hiyo moja katika viwanja hivyo vilivyochezwa Dar es Salaam nimeambiwa ni zaidi ya shilingi milioni 40. Kwa hivyo, kujibu swali lako naamini kwamba shilingi milioni 40 kama

tutakapoingiza kwenye uwanja wetu tukitoa laki tano bila shaka faida itakuwepo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matengenezo makubwa ya Uwanja wa Amaan yanaendelea vizuri sana na kwa kuwa uwanja huo hivi sasa unapendeza vizuri sana. Je, Mhe. Naibu Waziri ahadi ya kuvifanyiwa matengenezo kama hayo yaliyoahidiwa kwa Uwanja wa Gombani Pemba imefikia hatua gani ikiwa ni pamoja na utiaji wa taa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru kwa swali lake, naweza kusema kwamba Uwanja wa Gombani hivi sasa tayari umeshakamilisha hatua za awali za kutia ile *transformer* kubwa na waya wa umeme tayari umeshawekwa. Hivi sasa tunamsubiri mtaalamu wa kutia zile taa ambazo tayari zimeshafika Pemba na zimeshakabidhiwa hapo awali na *Al-Youseif Foundation*. Zile taa zinahitaji utaalamu maalum wa kuzitia kwa sababu wanasema wenyewe tukizitia hivi hivi kienyeji kwa kutumia mafundi wetu ambao hawana utaalamu wa taa za uwanja basi vivuli vitakuwa vinne vya wale wachezaji. Kwa hivyo, kila mchezaji akenda utakuwa unaona watu wanne wanacheza kwa wakati mmoja, ndio maana tunawasubiri hao wataalamu watie hizo taa.

Pili matengenezo mengine yataendelea kama tulivyofanya katika ile *running track* tulitia ile lami nyepesi kwa kuanzia awali lakini matengenezo mengine yatakuwa yanaendelea kadri kipindi kitakapokwenda. Lakini naomba niseme kwamba Uwanja wa Amaan ulijengwa na Serikali ya Watu wa China hapo awali na pia ufadhili huu umetoka Serikali ya Watu wa China.

Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wa Gombani ni Serikali ya Watu wa Korea, labda kama Mchina tukimuomba wafadhili hawezi kutengeneza uwanja ule kwa ufadhili. Kwa hivyo, ufadhili wake utatokana na Serikali yetu wenyewe kwa sababu Wakorea sasa hivi wameacha kutupa msaada katika nyanja ya michezo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali mola la nyongeza lakini mheshimiwa naona kama kiti unakiogopa unakaa mbele tu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niipongeze wizara kwa kweli uwanja umejengwa vizuri sana na mimi kila siku huwa napita pale wakati naelekea afisini. Lakini hivi karibuni nilipopita nilikuta kuna punda watatu haoni kwamba punda wale wanaweza wakaharibu mandhari ya uwanja huo.

Mhe. Mwenyekiti, pia watatumia mbinu gani ya kudhibiti punda wasiingie kwa sababu punda hawendi kucheza mpira pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho ya Uwanja wetu wa Amaan kumewekwa *fence* mpya na *fence* hiyo nadhani nyote mtakuwa mmeishuhudia ni nzuri na ya kisasa na ni ya vyuma hatukutaka kutumia ukuta na mambo mengine kwa sababu ni *fence* za viwanja viko katika *standard* ya kimataifa zinakuwa *fence* kama hiyo iliyokuwepo Uwanja wa Amaan.

Mhe. Mwenyekiti, pale sasa hivi tunatumia walinzi mbali mbali wakiwemo walinzi wa JKU kutokana na vifaa vya ujenzi vilivyokuwepo vya kampuni hiyo ya Watu wa China. Ni kweli eneo lile ni maarufu kwa masuala ya punda lakini nadhani mashirikiano itabidi tupate ya kutosha kutoka kwa Masheha wa eneo hilo ili kuzuia. Hivi sasa askari wetu walinzi wanafanya kazi ya kuzuia wale punda kuingia ndani ya eneo hilo kwa sababu baada ya kumaliza kazi ya ndani sasa tunaelekea katika kazi ya viwanja vile viwili vya nje pamoja na agizo la Mhe. Rais la kutaka kujenga uwanja wa *indoor* pale nje. Kwa hivyo, naamini katika hatua hizo zote tutaimarisha ulinzi zaidi ili kuzuia punda hao wasiwemo katika eneo hilo na tunajua kwamba hawachezi mpira wao.

Nam. 34

Mapato Yatokanayo na Minara Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Shirika la Bandari Zanzibar linajitahidi kuimarisha miundo mbinu yake ikiwemo minara, kwa lengo la kuimarisha huduma na kuongeza mapato.

(a) Kwa mwaka mmoja minara yetu huchangia kiasi gani cha fedha

(b) Zipo taarifa kuwa Zanzibar hupata asilimia 40.6 (40.6%) ya mapato yatokanayo na minara; je, taarifa hizo ni kweli, na ni taasisi gani inayokusanya mapato hayo na kufanya huo mgao.

(c) Ni minara ipi ya Zanzibar ambayo hutoa huduma za Kimataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

a) Kwa mwaka mmoja minara yetu huchangia kwa wastani wa shilingi milioni miatatu na hamsini (350,000,000).

b) Taarifa ya kuwa Zanzibar hupata asilimia 40.6 ya mgao wa mapato yatokanayo na minara ni za kweli. Taasisi zinazokusanya mapato hayo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari za Tanzania (*TPA*) kwa upande wa Bara na Shirika la Bandari (*ZPC*) kwa upande wa Zanzibar. Utaratibu unaotumika ni kuwa meli hulipia mara moja pale inapoingia kutoka nje na hulipia sehemu inayoingia mwanzo (Bara au Zanzibar). Makusanyo hayo kwa pamoja hujumuishwaa na kugaiwa kwa asilimia 40.6 kwa upande wa Zanzibar na 59.4 kwa upande wa Tanzania Bara.

c) Minara inayotoa huduma za kimataifa ni Kigomasha, Matumbini kwa upande wa Pemba na Minara ya Nungwi, Mwana wa Mwana, Mangapwani, Pungume, na Mnara wa Chumbe kwa Unguja. Aidha, pamoja na minara hiyo mikubwa ipo minara inayosaidia vyombo kutoka na kuingia bandarini (*transit*) kwa upande wa Unguja ni Kiungani juu na chini, Maruhubi juu na chini na Bet-el-Ras juu na chini na kwa Pemba ni Mkoani juu na chini. Vile vile minara mengine inayotumika ni ule wa Beit-el-Ajaib ambao upo katika Kituo Kikuu cha Mawasiliano ya Baharini cha Unguja. Kwa ujumla minara hiyo iko 17 ambayo hutoa huduma za kimataifa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba niulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa amekiri kwamba Mnara wa Kigomasha ni miongoni mwa minara ambayo hutumika kimataifa. Ni kwa nini hadi leo hajachukua juhudi za kufanya matengenezo katika eneo lile angalau kuweka choo cha kutumia walinzi na watembezi kama watalii kwa ajili ya kuboresha mnara ule.

b) Mapato haya ya asilimia 40.6 nyinyi kama wizara mnaridhika vipi kwamba ndio mapato halisi na hatimae mkakubali kwamba ndio mapato yanayopatikana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kabla ya wenzangu wote nikushukuru kwa kukalia kiti hicho. Mhe. Mwenyekiti, Mnara wa Kigomasha si kwa ajili ya kutembelea na watalii ni kwa ajili ya kuongoza meli na kuleta usalama baharini. Pia katika mnara huo tunayo nyumba ya wafanyakazi wetu ambao wako pale wanaishi, kwa hivyo bila shaka na choo kipo, ingawa sio cha kileo.

Kuhusu suala jengine kwamba tunaridhika vipi na mapato haya. Kwanza historia ni kuwa mgao huu ulianza wakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

iliyovunjika kwamba upande wa Bara wanachukua asilimia 50.4 na Zanzibar ni asilimia 40.6. Kwa hivyo, tunaridhika kwa sababu mfano kama sasa kama Afisi ya Naibu Waziri makusanyo yanakusanywa kwa pamoja kwa kila mwezi halafu unafanyika mgao, na sisi Zanzibar tunapendelea mgao huu kwa sababu kwa mfano, 2008 tulichokusanya kwa Zanzibar na mgao tulioupata sisi ni milioni 29.

Lakini fungu tulilolipata kutoka kwa upande wa Bara ni shilingi milioni 323, mwaka 2009 sisi tumekusanya shilingi milioni 175 na Bara shilingi milioni 300. Kwa hivyo, ukiona hii asilimia 40 kwetu sisi tunaomba iendelee kwa sababu tunapata kingi kule kuliko tungelikusanya sisi mara mbili au mara tatu kwa sababu kule zinaingia meli nyingi. Kwa hivyo, nafikiri hili bado ni jambo jema na naomba liendelee hivi hivi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huu Mnara wa Kigomasha ni mmoja ya mnara unaotumika kimataifa na mnara huu ninavyoelewa mimi ni mnara mmoja ambapo umejengwa zamani sana.

Je, huu Mnara wa Kigomasha umeshafanyiwa matengenezo mara ngapi na ulitarajiwa kuishi kwa muda wa miaka mingapi bado mpaka sasa hivi uko jadidi au una matatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, huu mnara una miaka mingi sana ni miongoni mwa minara ya mwanzo kabisa. Lakini Shirika letu la Bandari tumekuwa na utamaduni wa kuufanyia marekebisho au matengenezo mara kwa mara na mara ya mwisho tulikuwa tunatengeneza taa ya mnara kuibadilisha kutoka hatua ya zamani na kuweka ya kisasa. Lakini mnara huu nafikiri haukupewa nafikiri miaka 50 au 60 ya kuishi kwa sababu unatengenezwa nafikiri una miaka mingi ya kuishi na kila kunapotokezea tatizo huwa tunautengeneza na uko katika hali nzuri, mimi mwenyewe nimeshapanda kuliko mara nne mpaka kileleni. Kwa hivyo, mimi naujua vizuri sana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kweli nimefarajika sana kusikia minara ina mapato na faida kubwa na faida hiyo sio ya pesa lakini hata kuongoza zile meli za kimataifa. Mwaka juzi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi katika kutembelea minara moja ya matatizo ilikuwa ni ukatikaji wa uwekaji wa taa katika minara ukiwemo wa Kigomasha. Kilichosababisha hilo zilikuwa zile *system* za zamani za taa hizo haziendi na wakati.

Je, katika kipindi hiki ambacho mimi si mjumbe marekebisho gani yamefanywa na mafanikio gani mmefanikiwa nyinyi Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi juu ya kuziweka taa hizo zote katika hali ambayo inaridhisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya minara yetu taa zake zinatusumbua na tumebadilisha mfumo wa uwekaji taa kutoka zile za zamani mpaka mpya. Kwa Pemba Mnara wa Matumbini umesharekebishika nafikiri taa yake sasa hivi iko salama isipokuwa taa ya Kigomasha ilikuwa inawaka na halafu inaharibika, lakini watu wetu walifunga kambi wakawa wanatengeneza. Mhe. Mwenyekiti, kampuni moja ya Uingereza ndio ambayo walituletea taa hizi lakini baadae walitwambia tununue seti nzima nyengine kubwa tukasema hiyo ni kupoteza pesa za serikali. Kwa hivyo kuna kampuni nyengine ikatukubalia kutuletea vile tulivyotaka natarajia taratibu zinaendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya tatizo hili kuna tatizo jengine ambalo linatukabili kwa minara ni lile ambalo ile minara midogo aliyoitaja Naibu Waziri ambayo watu wanajenga na wakijenga inakuwa ile minara midogo watu hawaioni vizuri wenye vyombo. Kwa hivyo, ile nayo ni muhimu nawaomba wananchi wote watusaidie kutokujenga sawa na minara yetu ili tuweze kufanya kazi zetu vizuri na meli ziweze kuingia katika bandari zetu kwa usalama na amani.

Nam. 35

Barabara ya Regeza Mwendo – Bububu

Mhe. Ame Ussi Juma - Aliuliza:-

Barabara ya Regeza Mwendo kuelekea Bububu, imepasuka pasuka na kufanya nyufa katika maeneo ya Meli sita Kianga, likiwemo eneo la Afisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi ya Wilaya ya Magharibi. Katika hali ya kawaida, inaweza kufahamika kwamba nyufa hizo zimesababishwa na kiwango duni cha ujenzi wa barabara hiyo, ambayo ni mpya ukilinganisha na barabara nyengine.

(a) Je, Mhe. Waziri, dhana hiyo ni kweli.

(b) Wizara yako imechukua hatua zipi za kurekebisha nyufa hizo.

(c) Je, nyufa kama hizo zimetokezea kwa barabara ipi nyingine Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Ni kweli kuwa barabara ya Regezamwendo kuelekea Bububu imepasuka pasuka na kufanya nyufa katika baadhi ya maeneo kadhaa ya barabara hiyo, nyufa hizo inawezekana zilitokana na kasoro za kitaalamu katika kushughulikia maeneo yenye kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji barabara imechukua hatua ya kuziba baadhi ya nyufa hizo pamoja na kuzichunguza ili kuona kama zimesita au bado zinaendelea.

Baada ya kugundua kuwa nyufa hizo zimesita kuendelea wizara yangu itaendelea kuziziba nyufa zilizobaki kitaalamu zaidi ili kuondoa kasoro hizo zisitokee tena. Aidha, nyufa nyengine kama hizo zimejitokeza katika maeneo ya barabara nyingi zenye udongo wa aina hiyo. Barabara zenye mipasuko kama hii ni barabara ya Makunduchi – eneo la Muyuni na eneo la Mtende, Barabara ya Kidimni – Kitope, Barabara ya Mahonda Donge–Mkokotoni na Tunguu–Kinyasini na Kinyasini-Kiwengwa.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nakupongeza pamoja na hayo nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wakati anazitaja barabara ambazo zina nyufa kwa bahati mbaya sana hakuitaja barabara ya Mtuhaliwa-Chokocho ambayo imepewa jina la Mapinduzi Road haidhuru kule inakokwenda sio mapinduzi, halafu barabara inayotoka Mkanyageni-Shidi vile vile ina nyufa na nimeripoti kwa wizara inayohusika lakini kwa bahati mbaya hapa hakuitajwa.

Je, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuwakumbusha yeye hawa watendaji wake walioko Pemba akazifuatilie hizi nyufa za barabara hizi au kuwa na lengo la kuziba ukuta badala ya ufa.

Mhe. Naibu Waziri wa (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mhe. Mwakilishi tunauchukua na tutaufanyia kazi kuona kwamba maeneo hayo yote ambayo ameyataja kwanza tunakwenda kuyaona na pia tutayafanyia matengenezo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ametaja barabara chungu nzima zina nyufa kwanza haoni kuwa ni aibu. La pili katika utengenezaji wa barabara tunajua tunapita *stage* nyingi miongoni mwao ni udongo wa barabara au wa sehemu

ambayo inapitishwa barabara hupelekwa kwenye maabara na kuchunguzwa namna gani ma-*engineers* waweze kutengeneza barabara hiyo.

Je, hatuna wataalamu wa kutosha au sahihi wanaopeleka ripoti mbaya kwa ma-*engineers* wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, juzi tulijibu swali kama hili na tulieleza hatua ambazo tunachukua katika ujenzi wa barabara. Hizi barabara alizosema Naibu Waziri wangu nyingi sio za jana au leo, kwa sababu kama hiyo ya Regezamwendo ina zaidi ya miaka 15 tangu kujengwa. Tulieleza juzi kwamba barabara inatemea mambo mengi kama uzito wa magari yanayopita, udongo na mambo mengine.

Lakini nalihakikishia Baraza hili kwamba, makampuni yote ambayo yanajenga barabara kuna wataalamu na sisi tunao wataalamu na tuna maabara ya kupima udongo na mambo mengine kabla ujenzi wa barabara kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Waziri. Kipindi cha maswali na majibu kimekwisha sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kuwatambulisha kwenu kuwa tuna wageni hapa leo watoto wa Skuli ya *Zanzibar Junior Academy* iliyoko Mbweni, wao wamekuja pamoja na wakufunzi wao, niwatambulishe kwenu nawaomba wasimame.

Karibuni sana, wako katika mafunzo na wanafunzi hawa wanadhaminiwa na Jumuiya moja ambayo inaongozwa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Karibuni sana na tunawakaribisha mjifunze. Sasa tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Jana tulikuwa tukimsikiliza Mhe. Moh'd Ali Bakari na hakuwahi kumalizia. Sasa karibu uendelee nakupa dakika kumi.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutuwezesha kuifikia siku hii ikiwa bado tuko hai, lakini nakushukuru na wewe pia kwa kunipa muda wa ziada ili niendelee na mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mswada huu una dhamira njema sana, kwa mazingira ya nchi yetu na hali ilivyo hivi sasa duniani. Kadiri ya matatizo

yanavyojitokeza ndivyo kadiri mwanadamu anavyopaswa kubadilika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, napata mashaka makubwa sana kabisa juu ya mswada huu na hatimaye sheria. Kuna mambo yalitupita sana na tukayaacha yakenda yanavyokwenda na sasa tumeona umuhimu wa kuyapangia sheria. Lakini hatukuangalia pia mazingira tunayoyapangia sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomalizia jana kusema kwamba watu wetu ni wanyonge na tunatofautiana sana vipato. Kwa sababu suala hili la uvuvi liliachwa kila mmoja akavua apendavyo na ajuavyo. Leo limetuathiri kiasi kwamba unapotaka ulitungie sheria moja kwa moja basi lina ugumu wake katika utekelezaji.

Kwa hali hii kutokana na watu jinsi walivyozowea katika suala la kuvua, Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi sijajua nini hasa wizara ukiacha hizo nyavu za jarife wanazowapa watu ni nyavu nyengine wanazoziona kwamba zinafaa ili watu wawe nazo na waendelee na kazi hiyo na iwe si uharibifu wa mazingira.

Lakini hivi karibuni Mhe. Subeit Khamis Faki, Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni alikuwa na nyavu zake za mtande za macho madogo madogo zimekamatwa na hadi leo hajapewa, sijui ni kwa nini. Lakini hapa Malindi nyavu kama hizo maboti yote ndio yalizonazo na ndio wanazovulia. Sasa sijui ni wapi nyavu hizi zinafaa na maeneo gani hazifai kuvulia.

Mhe. Mwenyekiti, lililo kubwa zaidi katika suala hili la kuangalia wananchi wetu kama kweli tunawaangalia wananchi wetu katika kuwakomboa katika hali ya unyonge walionao, unyonge wa kupindukia mipaka na kuwaweka angalau katika maisha ya matumaini. Mimi nadhani tungewapatia vifaa kwanza vinavyohitajika, wanavyovikubali wizara na serikali kwamba hivyo wavitumie katima maisha yao ya kila siku, halafu ndio tuwapangie sheria. Kwa sababu ukimpangia sheria mtu na kitu ambacho hanacho kwa kweli utamuathiri.

Nitoe mfano kama pale Tumbe, Wavuvi wetu wanaovua nyavu za kukokota ni wengi. Sasa mimi Ali Moh'd Bakari ni Mwakilishi wao wamenichagua nimo humu ndani, halafu nije niwapangie sheria au nikubali kupitisha sheria ya kuwafanya wao wakamatwe, akitokea mmoja akaniuliza wewe si ulikuwemo mule? Mimi nisemeje? Nitakuwa sina jibu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waziri ana nia njema sana ya kukabili hali zote mbili ama upande wa serikali na upande wa jamii, mimi nadhani kwa sababu wanayo hii Idara ya Uvuvi ambayo inatoa maboti na vifaa vingi vya uvuvi basi nadhani ule ushauri wangu wa kwamba hizi nyavu au maboti wasipewe vikundi na badala yake wapewe wavuvi wenyewe. Kwa sababu vikundi wakati mwengine vinakwenda na kujuana, mimi namjua waziri au

naibu waziri, namjua mkurugenzi nitaunda kikundi changu nitakwenda kufanya *lobbing* naye pale atanipa nyavu. Lakini napata zile nyavu kwa sababu tu ya kujuana na kwa sababu ya mambo yangu mengine. Tunawaacha wavuvi ambao ni wanyonge na ambao wanafanya kazi ile na wanajulikana halafu nakuja kupewa mimi.

Nadhani bado hatujawasaidia, kwa sababu tunawajua walimo tuwapitieni kwanza halafu tutake kujua ni wangapi, wanavua vipi, halafu tuwashauri namna ya kuvua. Kwa sababu si kila nyavu yenye macho madogo ni haramu ni aina ya uvuvi tu, ni ile aina ya uvuvi tu ndio unaokuwa haramu lakini si zile nyavu na uvuvi wake.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba uvuvi wa gesi, bunduki na chupa ni haramu na zinapigwa vita. Lakini linalonishangaza mimi ni kwamba uvuvi wa chupa hizi kwanza mnauona kila siku na watu mnawajua, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyekamatwa kwa uvuvi huo.

Mhe. Mwenyekiti, lililo kubwa zaidi ni kwamba hapa Unguja pale Darajani na maeneo mengine ndipo palipo na maduka haya ambayo hawa wavuvi wanaovua haramu wanaleta hivyo vifaa. Lakini mnawaacha halafu mnakwenda kumtungia sheria mtu wa pili, yuyle anayeziingiza hapa nchini anakuwa hana tatizo. Sasa mimi nadhani katika sheria hii ingepiga marufuku kwanza uingizwaji wa vitu hivi kama vile tunavyopiga marufuku madawa ya kulevya kuingia nchini mwetu pamoja na utumiaji wenyewe.

Pia tupige marufuku uingizwaji wa hizi nyavu ambazo hazifai kwa sababu ukishaziingiza nyavu hivi Mhe. Mwenyekiti, lazima watu watazinunua na watazinunua kutokana na unyonge wao. Watu tunavyotofautiana kipato yule mtu wa kipato cha chini atakwenda kutafuta kile kitu ambacho kitamsaidia katika kuendesha maisha yake hata kama hakifai.

Mimi nadhani katika jambo hili Mhe. Mwenyeikiti, ni vyema sana kuyapitia maduka na kuangalia vifaa wanavyovileta ili kuwapunguzia hawa watu wetu matatizo. Kwa sababu wakishakwenda kununua maana yake tunawatia katika matatizo na kuyaacha maduka haya yaendelee kuwepo tutatafsiri kwamba labda kuna wakubwa wana ubia au haya maduka ni yao wanaagiza kwa sababu ni maduka yako katika uso wa macho yetu.

Kwa kweli nashukuru sana kuona Idara ya Uvuvi inajitahidi na inapiga hatua sana kabisa katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata vyombo vya kisasa. Lakini Mhe. Waziri mimi nataka nijue na naomba sana unieleweshe. Ni nyavu za aina gani zinazohitajika kupatikana hatimaye hawa wavuvi wavue iwe ni halali. Kwa sababu kwa kuwa watu ni wanyonge

watazipata vipi, na kama hawanazo na hawana njia ya kuzipata wafanye nini? Kwa sababu nyavu walizonazo ni hizo ambazo zinapigwa vita na hazifai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani utaratibu wa kuwapangia sheria ni jambo moa, lakini pamoja na matumizi yake ni kitu chengine. Kaw hivyo, lazima tuangalie kwanza utaratibu wa kuwapatia zana za uvuvi na kuweza kufanya kazi zao kila siku halafu ndio tuje tuwatungie sheria. Kwa sababu haya mambo tumeyaacha siku nyingi za nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda pale Mombasa, Kenya bahari ipo na watu wanavua, lakini kwa sababu wao waliweza kuya-*maintain* mambo yao mapema pale humkuti mtu akivua samaki mdogo, wala humkuti mtu akivua uvuvi wa gesi wala bunduki, ni kwa sababu wao tayari kila mmoja mtu anajichuna anajua kwamba hapa panatakiwa uvuvi gani, hata hawa watu wetu wanaotoka katika visiwa hivi wakenda madagoni kule Kenya wanafuata *system* ya wale wenyewe pale walivyo kutokana na uvuvi wao. Kwa sababu wao wanafuatilia vizuri.

Wizara ya Kilimo, Mfugo na Mazingira ni wizara ambayo kwa wizara zote ina wataalamu wengi zaidi, lakini ukienda katika kila maeneo wizara hii kwa kweli haifanyi vizuri zaidi isipokuwa labda hii Idara ya Uvuvi. Licha ya kwamba waziri juzi tu kagawa mahonda mengi, lakini yeye anaomba, anatafuta, jitihada yake yeye anafanya lakini watendaji wengine kwa kweli wanashindwa kutimiza wajibu wao.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi nataka kwanza aje anambie nyavu gani zinazotakiwa na watu wetu watazipata vipi, japo kwa mkopo ili kusudi waendeleze kazi hizo.

Halafu hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nina nia ya kuunga mkono nitaunga mkono, lakini nataka niambiwe kwanza ni nyavu za aina gani na zitapatikana wapi. Kwa sababu nataka nikiunga mkono niunge jambo ambalo litakuwa na maslahi na wao, nisije nikaunga mkono sheria ambayo halafu wao nitawatia kitanzi baadae waje wanihukumu mimi, keshokutwa nahitaji kuja tena hapa Barazani. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakukaribisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wewe ujitahidi utumie dakika kumi. Wachangiaji mpaka sasa hivi wako kumi na mbili, kwa hivyo, tujitahidi kwa sababu Mhe. Waziri tunategemea atafanya majumuisho asubuhi hii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikupongeze kwa kukalia kiti hicho, lakini Mhe. Mwenyekiti, ukikaa kwenye kiti usogee nyuma kidogo angalau kikujae.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri. Katibu wake pamoja na watendaji wake wote wa wizara yake kwa kutuletea mswada huu wa sheria ambao utatuokoa katika kutuondolea umasikini kwa njia ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nitaanza kidogo kwa jumla jumla, japo umenipa dakika kumi lakini nitazitumia hizo hizo ilina wenzangu wapate kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, mengi wenzetu wameshaanza kuchangia, lakini na sisi ukiona tunarudia yale yale basi utuachilie kwa sababu tunatilia mkazo. Kwa sababu kuna mambo mengine lazima tusaidie kuyatilia mkazo ili wizara nao waweze kuyafanyia kazi vizuri.

Kwa kweli uharibifu wa bahari umekuwa mkubwa sana, na ndio maana wenzetu wakaona walete sheria hii ili kupunguza maasi ya uharibifu wa habari. Mimi Mhe. Mwenyekiti, kama ukanda wa kwangu kule Kiwengwa japo niliambia sina bahari, lakini mtu hajui tu, kule tunayo bahari kwa Jimbo la Kitope nina bahari kuanzia Fujoni, Kiomba Mvua mpaka Kiwengwa. Na ukanda huo kwa kweli wanajitahidi sana, wana kamati zao, lakini kuna mambo ambayo kamati hizo hushindwa kufanya kazi na mwenyewe Mkurugenzi anaelewa sababu gani zinashindwa kufanya kazi vizuri ni kutokana na vitendea kazi.

Kwa sababu sasa hivi wizara ikubali ikitaka isitake, kuna *system* za vyombo, unapopewa habari kuna jamaa tayari wanahamia huko wanataka kuharibu bahari sasa leo wewe una boti lako la nanga au *horse power* 20 kwa kweli huwakuti. Lakini wizara ikubali kabisa kama tuna nia ya kuleta mswada huu wa sheria mzuri tu, basi wajiandae na vitu hivyo, *speed boat* lazima ziwepo, tukiwanazo *speed boat* basi tuhakikishe masuala hayo hayatokuwepo tena hapa katika kisiwa chetu. Kwa sababu kisiwa hiki ni mzunguko wa bahari na wataalamu wametizama sana jinsi gani umasikini unaweza ukaondoka kwa haraka haraka ni kwa njia ya uvuvi na ndio maana Mkurugenzi wetu anastahili sifa. Nikisema anastahili sifa ni kutokana na pahali pake pa kustahili sifa, amejitahidi katika huu Mradi wa *MACEMP* kwa kuwasaidia wavuvi kuondolewa umasikini.

Pamoja na hayo niseme sifa zaidi hii kukidhi haja au kulinda pesa za wafadhili kuzitumia kwa wakati unaokubalika na mpaka fedha nyengine zikabaki na kaongezwa na nyengine. Hii ni moja ambayo changamoto kubwa sana, mimi sijasikia wizara nyengine kama zipo basi na wao wasinilani nitawapongeza, lakini hili lazima niseme ukweli. Kwa sababu kuwa bado tunaambiwa tuna hii

MACEMP ya pili au ya tatu, hii ni hongera kubwa sana, kutokana na utendaji wake mzuri aliowasaidia hao wavuvi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utendaji wake huo mzuri kidogo sasa nijaribu kuingia katika vifungu ili kuweza kusaidia kwa haraka haraka. Niko katika ukurasa wa 14 katika kifungu cha 2 Utoaji wa Leseni.

Mhe. Mwenyekiti, hapa wanasema kuna waziri anaweza kuweka vigezo vya leseni na kuweka viwango mbali mbali vya ada. Sasa hapa ningemuomba Mhe. Waziri kwamba havikuoneshwa vigezo hivyo vya aina gani, sijaona humu au kama vimo inawezekana labda kwa kuwa leo sikuvaa miwani. Basi ningemuomba si vibaya Mhe. Waziri kwa kuwa tunataka hili suala kulitengeneza vizuri basi atwambie, kwa sababu inawezekana waziri siku hiyo kahamaki tu inawezekana akatoa vigezo ambavyo vinamuathiri yule anayekata ile leseni.

Hapa mimi ningeomba kidogo akanisaidia, akija anifafanulie ili na mimi niweze kufurahika zaidi na niweze kuwaeleza wananchi wangu ni jinsi gani ambavyo vigezo hivyo vitaweza kuwasaidia wananchi wetu kupata leseni kwa wingi.

Halafu ukurasa wa 15 kifungu cha 15(5), leseni inayotolewa chini ya sheria hii haitahamishika. Unajua kila na tafsiri yake, sasa haitahamishika mimi nashindwa kufahamu, kwa maana hiyo haitahamishika sitaweza kukaa dago Bara? Labda mimi imani yangu inanijia hivyo, kuwa hii leseni haivuki maji hapo, haitambulikani kwa kwenda Bara, hiyo ndio tafsiri yangu. Kwa sababu kila mtu na tafsisi yake. Mimi kwetu Kaskazini inawezekana lugha ikawa nyengine. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri anieleweshe vizuri hii, haitahamishika kivipi, kuwa ita-*round* hapa hapa tu kati ya Kizingo, Kiwengwa, na kwengineko hatoweza kuvuka Bara. Sasa hapo kidogo naomba anisaidie.

Halafu tukija katika kifungu cha 17 tunaambiwa mtu yeyote hatatumia uvuvi wa juya, hii hatatumia sijui ndio kwa mujibu wa sheria za wanasheria au vipi, lakini naona hapa atafute neno rahisi tu, hili linanipa mashaka na mimi katika Kiswahili changu. Hatatumia, hii siifahamu vizuri, hatatumia uvuvi wa juya ndio sawa sawa nakubaliana nayo, uzio, bunduki na mishale, nakubaliana nalo hilo, lakini hebu tutafute neno liweze kumsaidia mtu mara moja tu kuwa hatatumia.

Sasa hatatumia kidogo inanishangaza labda Mhe. Mohamed Ali Salim (Mula) anaweza akanisaidia hii lugha. Kwa sababu hii hatatumia kidogo naona inanipa shida, tungetafuta neno jepesi la kusema kwamba hatotumia au hatatumia.

Hapa ningemuomba Mhe. Waziri kidogo aje kunifariji kunipa sentesi ambayo ninaweza nikaizungumza kwa ufupi tu ikaleta maana.

Tukija ukurasa huo huo kwenye kifungu cha 18, kwa madhumini ya kufanya utafiti au mambo yanayohusiana nayo mtu yeyote au chombo kitapeleka, kinaendelea. Sasa na hapa pia, unaona lugha hii, chombo kitapeleka, kitapeleka nini chombo? Inamaana kile chombo kita-*runing* wenyewe, kitakwenda kujipeleka, sasa ndio miujiza iko hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba na sentensi hii anisaidia Mhe. Waziri. Chombo kitapeleka ombi la leseni kwa waziri. Mhe. Mwenyekiti, kidogo mimi nachanganyikiwa na hiki Kiswahili, kuwa chombo kimeainishwa tayari, mtu yeyote, sawa, au chombo kitapeleka. Sasa na mimi ningesaidiwa huu utaalamu ili kuona ni jinsi gani ya kuweza kuchangia vizuri kwa sababu sifahamu kwamba chombo kitajipeleka wenyewe kwa waziri.

Ukurasa wa 17 naomba na hili Mhe. Waziri anieleze, kifungu cha 22 kwamba, "Mtu yeyote hataruhusiwa kukamata au kushusha samaki, kuuza, kupokea au kumiliki samaki yoyote". Hapa nina wasi wasi mmoja, kaka yangu hapa jana alieleza Mhe. Abass Juma Muhunzi kuhusu wananchi wanaotaka kufuga samaki. Na mimi niseme ukweli jimbo langu kule sehemu za Fujoni mpaka Kiombamvua, kuna kikundi nacho tayari nimefika mpaka kulipa pesa za *survey* ili waweze kufuga samaki, lakini mpaka leo hawakupita kabisa hao wahusika.

Tumekwenda mpaka wale wazee wakanambia Mheshimiwa sasa hivi viatu vishalika, kwa sababu mwendo umekuwa ni mrefu mafanikio yake yamekuwa madogo kabisa. Sasa hili nalo tuliangalie kuwa hivi sasa mimi nataka kufuga, kwa mfano nimekwenda kwa Mhe. Muhunzi amenipa vitoto vya samaki ili na mimi nikaanzishe mradi ule, ina maana hapa sheria itanikamata, hebu tuangalie hapa, lakini kwa nia nzuri tu, sikuwa na maana kwamba nivichukue vitoto vile ili niende nikaviharibu hapana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kifungu hiki nacho anisaidie ili nisije nikafanya kosa na mimi kwa kuwa lengo zuri la wananchi nikataka kuwaondolea umasikini kwa njia ya ufugani wa samaki.

Lakini vile vile namwambia Mhe. Waziri tayari ukanda huo wamejitolea na wameshatoa pesa zao za kufanyiwa *research* hiyo lakini mpaka leo hawajakamilishiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo kwanza niishukuru sana wizara hii na shukurani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Uvuvi, kutokana na kazi zake nzuri Mwenyezi Mungu ambariki pia Mwenyezi Mungu Inshaallah na yeye atamleta

huku *backbencher*. Ahsante sana na mimi nauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kukupongeza na nilipongeze Baraza kwamba leo tunaongozwa na kinamama. Naomba pia kutoa shukurani kwamba naona fahari nimekusomesha leo umekuwa Mwenyekiti wangu kwenye Baraza. Hongera sana. Kwa mwalimu ni fahari kuona wanafunzi wake wamefanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nilikuwemo kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na tuliijadili sheria hii kwa urefu, neno kwa neno kwa kiasi kikubwa. Kama walivyosema wenzangu nimpongeze Mhe. Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi ni mtaalamu anayeelewa kazi yake na anafahamu hasa anaposema anasema nini na huo ndio uzuri wa utaalamu.

Tukapata tena bahati Mhe. Mwenyekiti, ya semina na moja katika kitu ambacho Mhe. Mkurugenzi aliona fahari kutwambia ni kwamba jamani jioneeni fahari tuna samaki wengi kweli. Tuna samaki wengi, lakini data hazioneshi kwamba samaki hao tunawavua. Sasa katika hali ya mjadala wangu mimi sitokwenda sana kwenye sheria nadhani itakuwa kidogo ushauri. Bahati mbaya au nzuri wenzangu mimi ni mtu wa ma-*data.* Hizi ni *slide* alizotuonyesha Waheshimiwa Wajumbe wakati wa semina.

Kuna *slide* pale mwaka 2000 wavuvi ni laki tisa, elfu tisa mia nane na tano Kaskazini ‘A’ nikiwemo Juma Duni niliyezaliwa kwenye familia ya uvuvi. Micheweni kuna elfu tatu mia tisa na kwa jumla wavuvi ni wengi na kila anayesimama hapa Mhe. Makame Mshimba sasa hivi kaka kitako na yeye ana wavuvi, Mhe. Ali Moh’d Bakari ana wavuvi wale wenzangu kutoka Pemba, inaonekana kwamba ni moja katika sehemu kubwa sana ya maisha ya watu wa Zanzibar.

Sasa wavuvi ni wengi, mali baharini ni nyingi, lakini haionekani kutusaidia. Hili *Zanzibar Economic Bulletin* nilitoa juzi hapa hapa ndani, inaonesha kwamba mchango wa uvuvi ni asilimia 4.6 tu kwenye pato la taifa. Lakini nasema *about 99 percentage of the average annual fish cash, around twenty thousand tons is consume be locally.* Tunawala wote, *only one percentage* ndio tunasafirisha.

Mwani unazaliwa mwingi na *data* hapa zinaonesha hasa kwamba kuna aina mbili na ile moja ndio unazaliwa mwingi lakini bei yake ndogo. Kuna ule wenye bei kubwa uzalishaji wake mdogo. Sasa jamani sheria imekuja, sheria ya udhibiti ni vizuri, aina ya uvuvi ni udhibiti, juya huwezi kuvua, uzio huwezi kuvua na kadhalika. Leseni ni kawaida ya utaratibu wa kufanya kazi wa mali za

serikali ni udhibiti, adabu zilizowekwa ni udhibiti na hawa masikini njia zao ndio hizo hizo.

Mhe. Mussa Aboud Jumbe anajua zaidi lakini nikiuliza jamaa zangu kutengeneza boti moja ya uvuvi katika huu wa *tradition*, sidhani kwamba inapungua shilingi milioni tano, ile kubwa ukiacha vile vidudu vinavyoitwa vidingi, halafu upate karabai, upate nyavu huo mtego unaoambiwa. Nyavu juzi nilipita nikauliza pande moja shilingi mioni moja laki mbili.

Kwa hivyo, ukitaka mtego wa pima mia wazee wangu wanasema, unahitaji mapande sita mpaka manane si chini ya shilingi milioni nane, ukitaka kununua boti ya injini iwe ya nje ile ya *horse power* 4 lakini petroli ndio tunaijua siku hizi wanatia ndani, lakini ile ya ndani kuipata nayo si chini ya shilingi milioni tano. Sasa hawa masikini ni masikini kwa sababu ni masikini na kwa sababu uwezo wa kujitoa kwenye umasikini hawana. Lakini sheria inawaadhibiti, ni vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichotaka kukieleza ni kwamba, nilivyosikiliza yote haya na kuzitizama hizi *data* zilizotolewa katika vitabu mbali mbali, niliitizama bahari kama mgodi wetu. Wenzetu wana mgodi wa dhahabu Geita, wana almasi pale Shinyanga, sisi tuna mgodi wa dhahabu ya samaki lakini hatujachimba. Na ushahidi huo umetolewa na Mkurugenzi wa Uvuvi hapa juzi, anasema ukiacha haya maji ya ndani, hapa hapa ndani tu, dagaa, vibua, changu, chewa wa kutega wale yaani hata zile meli 12 acha huko kwenye mgodi mkubwa ambao ingekuwa tunachimba dhahabu, acha kule mita 200 unazokwenda na *grader* na mashine. Hapa penye hizi meli 12 ambazo tunatumia *troll* hata hapo hatujafika. Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema walikwenda kupima damu wazee wakasema nyinyi wenyewe mnataka kusaidiwa damu.

Kwa hivyo, mimi ninachosema kwamba bahari hatujaitumia lakini uchumi wetu unategemea karafuu. *Data* zinaonesha hapa kwamba karafuu nazo zinapata matatizo. *Data* za Benki Kuu nilikokwenda na wenzangu hizi hapa wanatwambia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar umesaidiwa na watalii ndio nambari wani. Sasa watalii siku wanayosikia tu kumetokea tatizo lolote Zanzibar hawaji na kwa sababu ni watu, ni uamuzi wa mtu kwa hivyo si wa kutegemea.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mhe. Waziri na wale watu wa fedha naona babu yangu Mhe. Mwinyihaji Makame hayupo hapa ni kwamba tuwazuie wasiharibu lakini tumewatayarishaje mbadala. Hili Mhe. Mwenyekiti, nina uzoefu kwamba ninasafiri nakwenda Mwanza katika shughuli zangu za kisiasa. Moja katika tatizo kubwa ambalo wananchi wa Mwanza wanaoishi

kwenye *Lake Victoria* na Bukoba ni vita kati yao na serikali. Lugha ya kule nadhani wanaita mikokoro, huwa wananyang'anywa, wanakamatwa, zinachomwa moto nimeshazikuta rundo kubwa zinachomwa moto. Sasa unawauliza mnafanya nini? Wanasema tufanye nini na haya ndio maisha yetu, tunafanya japo kwa magendo.

Sasa wanafanya kwa magendo halafu mnawakuta wako barabarani na samaki kwenye vikapu wanavizia magari kwa sababu hawaruhusiwi kwenda wakaonekana na samaki wachanga.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu huu naueleza hapa kwa sababu nimeukuta dhahiri tatizo ni nini. Tatizo ni kwamba serikali kule ilipoona mambo yanakwenda vibaya katika uvuvi wakawazuia, lakini hawakujiandaa hawa jamaa tunaowazuia mbadala wake watafanya nini.

Sasa sisi tunapitisha sheria hii, zuia. Kwenye maeneo maalum yale ya *marine park*, uzio na juya zuia. Kuna mradi mmoja naambiwa upo unasaidia lakini mimi sina hakika Mhe. Waziri atanisaidia atakapoleta *data*. Kwa muda huo ni wavuvi wangapi waliosaidiwa, wanasaidiwa lakini ni vikundi vichache tu.
Sasa ushauri wangu ni kwamba sheria inapita, tutazuia kwa faida ya kuacha samaki wakue wanapovuliwa wasiwe wachanga. Lakini kwenye samaki hatwendi, twendeni kwenye samaki.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Faki Shaali jana ananambia kiasi mwezi mmoja Pemba kule lilitokea samaki moja limeshachoka kukaa huko maji makubwa anasema linafika hapa na kule. Likawa haliwezi kuogelea jamaa wakalifunga makamba wakalisogeza kwenye mikoko wakalifunga na mikoko. Nasikia ilikuwa neema kila mmoja akawa anakata, wenye gari za ng'ombe, wenye gari za punda. Kwa hivyo, ina maana kule juu madudu yako hatuyafuati.

Mhe. Mwenyekiti, nisichukue muda zaidi niende kwenye Idara ya Uvuvi ambayo sijui kwa nini inaitwa idara, Mhe. Waziri na wataalamu akina Mhe. Abubakar Khamis Bakary watasema hapa. Mimi nadhani ukishaliweka neno idara kwenye sheria umeshaifunga hii itabaki idara, wakati nahisi inahitaji jina kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitengo cha kuzuia, kitengo cha *research.* Kuwe na kitengo angalau tuweze kuvua kwa *troll. Troll* ni sawa sawa na meli ya MV Mapinduzi na meli ya MV Maendeleo. Kama tumeweza kuinunua meli ya MV Maendeleo basi tunaweza kununua *troll.*

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mswada huu umezingatia vipengele vyote

muhimu ambavyo vinahitajika kwa wakati huu hasa. Naanza ile hoja ya Kufuta Sheria Nam. 8 ya mwaka 1988 na kuweka sheria mpya. Kwa kweli inakidhi haja. Mimi nitakuwa kama wale wanaopiga *Fat-ha* kwanza wakaitikia Amin kabla ya kusoma hiyo ya *Suratil Fat-ha* yenyewe. Kwa hivyo, mimi kabla ya kuanza nasema kwamba mswada huu nauunga mkono mia fil mia.

Mhe. Mwenyekiti, tukianza ukurasa wa 12 kifungu cha 5 "Kazi za Idara". Sehemu hii utakuta katika lugha ya Kiswahili kidogo kuna utata mmoja ambao ningeomba uwekwe sawa na naomba kunukuu:-

Kifungu cha 5 (1):

> "Kukuza, kuendeleza, kudhibiti na kufuatilia shughuli zote za uvuvi na mambo yanayohusiana nayo kwa madhumuni ya kuwa na usimamizi bora katika uvuvi wa kienyeji na viwanda".

Sasa hivi viwanda ndio hapana ufafanuzi mzuri. Lakini katika lugha ya Kiingereza kimetiwa hapo *artisanal and semi-industries*. Jambo hilo nilikuwa nikitaka niliweke sawa hapo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Zanzibar bado tunafanya shughuli za uvuvi za kienyeji sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi mpaka leo siku ninayofurahi hutoka nikenda nikavua. Ukenda ukivua kule unachukua samaki yeyote, ukipata kinengo, kishwara haya, mdogo mkubwa wote unapakia tu ndio umeshapata wewe.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi nilikwenda nchi za nje huko Ulaya tukenda tukavua. Kule samaki wanahifadhiwa, ukipeleka mshipi tu basi tayari wanakula. Sasa ukishakuvua pale unampeleka samaki wako anapimwa, ikiwa hakufika kilo 5 anarudishwa kwenye maji. Aka! Mbona nyinyi samaki mnawatupa, anasema hapa bwana samaki kama hajatimia kilo 5 ukifika hapo nje utakamatwa. Samaki wote wanapimwa kwa mujibu wa urefu wao na uzito wao.

Ndio mwanzo wa kusema kwamba mimi kule Zanzibar nikipata kishwara cha nguru nakitia katika chombo kumbe ilikuwa ni makosa makubwa sana. Siku hiyo ndio nikasoma kwamba kweli wenzetu wana sheria nzuri na wanazifuata. Yule mvuvi akishakumvua samaki na kumtoa ndoana yake anamtoa asimchane mdomo ule ili asije akawa hawezi kula.

Kwa hivyo sheria hizi Mhe. Mwenyekiti, si ngeni, ni sheria ambazo zipo na zinatumika na kutokana na hali hiyo ndio maana ukawaona wenzetu ukitia mshipi tu samaki anakula. Kwa sababu samaki wako wengi, hawaharibiwi, hawavuliwi samaki wachanga, hakuna uharibifu wa aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kutokana na kuzingatia mambo yote muhimu katika sheria hii na kwa kweli yatatusaidia sana huko siku zinazofuatia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama miaka 12 hivi nyuma nilikuwa katika *Chamber of Commerce* kule tukaja tukapata ripoti ya uvuvi wa wenzetu kule Mwanza. Tukaangalia tukaona wale jamaa wanaweza kusafirisha samaki wa dola 66 mpaka 70 milioni kwa mwaka. Tukasema sisi kisiwa cha Zanzibar tumezungukwa na bahari kila upande tunasafirisha samaki kiasi gani kwa mwaka, hakuna. Samaki wakavu wao pia wanasafirisha lakini katika kisiwa chetu cha Zanzibar hakuna hasa usafirishaji wa samaki.

Mhe. Mwenyekiti, nikagundua kuna kiwanda kimoja kilijengwa huku cha kulea na kukuza hawa kamba wakubwa *(lobsters)* ambao walikuwa na soko kubwa kupelekwa Ufaransa. Ni mradi uliogharimu kiasi dola laki 5. Wale jamaa wakati wa kusafirisha samaki kupeleka Ufaransa ilibidi lazima wapate kibali, kuna *code number* ya kibali ambacho kipo Tanzania Bara. Walikwenda mbio wale mpaka wakachoka kile kibali hawakukipata na kwa hali hiyo kwa sheria za *EU* bila ya kutumia hii *code number* wakashindwa kuwapeleka wale kamba kule Ufaransa. Kwa hivyo, kile kiwanda na yale mazalisho ya wale kamba kilikufa hapo hapo, jamaa wakaondoka wakenda zao kwa sababu biashara ndio hakuna.

Kwa hivyo, mimi ningeomba kwanza ili tuweze kufaidika na bahari yetu lazima tuwe na uvuvi wa kibiashara na tuwe na viwanda vya biashara vya kuweza kuhifadhi na kusindika samaki wakavu, samaki wabichi na kuweza kusafirisha. Vile vile tuwe na mpango wa kuweza kufuga.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano Thailand, ukifika kule wale jamaa wanafuga pweza, likitoka pweza lina kilo zake hasa, unaliogopa wewe lile pweza likitoka. Wanafuga pweza, wanafuga *prawns*, wanafuga samaki aina zote na kwa kweli kitoweo hakina *season* kule. Kwa hivyo, upepo ukivuma jamaa kitoweo kipo, kuna dharuba kitoweo kipo. Ilitokea Tsunami kule lakini kitoweo hakikuwa ni matatizo kwa hivyo ufugaji unasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kilichokosekana Zanzibar hatuna maabara ambayo itaweza kuthibitishwa kilimwengu kwamba kifaa hichi kina nembo fulani kwamba bidhaa hii ikitoka hapa itakuwa *acceptable* katika nchi nyengine. Zanzibar hapana maabara na si kwa hili tu lakini kwa kila sekta.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo linatusumbua katika sehemu ya uvuvi ni taasisi ya utafiti. Taasisi ya utafiti mimi bado sijaiona na kwa kweli hili ni suala

muhimu sana. Utakuta Mkurugenzi anajitahidi kueleza, anafanya kazi zake nzuri, lakini kama hapana taasisi ya mambo ya uvuvi kwa kweli hali hiyo itakuwa mbaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka miaka ya nyuma hapa Zanzibar palikuwa na taasisi fulani waliweka mpaka *Aquarium* pale Malindi. Kwa kweli watalii wengi walikuwa wanakwenda pale wanaangalia na hiyo ni moja katika kivutio cha utalii. Ukenda Singapore kuna *Aquarium* kubwa sana ambayo inaingiza watalii zaidi ya laki tatu kwa mwaka. Sasa utaangalia ni kiasi gani cha fedha ambacho kinaingia.

Mhe. Mwenyekiti, mengine yaliyokosekana hapa Zanzibar hakuna chuo cha uvuvi, hakuna mfuko wa uvuvi, wavuvi wote hawa hawapatiwi mfuko wa kuweza kuwasaidia kufanya kazi zao. Pia wavuvi wa Zanzibar hakuna *storage facilities* za kuweza kuwasaidia, hakuna masoko yenye kukubalika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniwie radhi kidogo, siku moja tulikuwa katika Hoteli ya *High Hill* pale Kilimani ndio mwanzo mwanzo tunaanza mambo ya utalii. Akaja mzungu mmoja pale mimi nimekaa na yule mmiliki wa hoteli alikuwa Ndugu Said Chauchau, akatuuliza hiki chakula sisi mnachotulisha hapa mmenunua kule soko la Darajani, ile nyama ndio tunayokula hapa. Akaambiwa ndio ile, akasema basi *I'm sorry, I'm packing now and I'm going,* siwezi kukaa tena hapa, ikiwa wageni mnatulisha nyama ile hii ni hatari kubwa sana.

Sasa siku ile mimi nikaanza kuamka kidogo. Ukenda Malindi pale samaki wananadiwa ufukweni, maji ya makaro juu yanatoka yanatiririka yanakwenda kule ambako samaki wametupwa chini wananadiwa na sote sisi tunanunua samaki hapo. Watalii wanakuja mpaka pale wanachukua *film.*

Siku moja palikuwa pana mnada yule jamaa akatia bei, baada ya kutia bei anaambiwa toa pesa akafungua suruali ya kwanza, suruali ya pili, suruali ya tatu, suruali ya nne yule mtalii anamchukua *film.* Wale wazungu wapo pale wanachunguza wanaangalia. Hali ya lile soko samaki wanaponadiwa ni chafu sana, ukenda mbele kidogo huku kuna mafunza wanatoka katika samaki wa juzi na juzi yake yale machango. Ukitaka kwenda huko sokoni urojo mweusi wa makaa, harufu mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, hii haitoi sura nzuri kwa masoko yetu mpaka watalii wakaweza kuamini kula chakula ambacho kimetoka katika soko kama hilo. Kwa hivyo, yangekuwepo masoko yenye kukubalika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni uokozi wa wavuvi. Wavuvi wanapata matatizo yoyote yale lakini taratibu za kuwaokoa ni ndogo sana na hali hii haiwapi faraja wavuvi na inawaweka katika hali ya wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mambo mengi sana ya kuzungumza lakini bahati mbaya kwenye taka taka za kumwaga pwani huko. Sote tunafikiri kama kule pwani ndio jaani kwa kumwaga taka zetu. Siku moja walikuja wazungu wameshuka boti na makapu ya taka wanatafuta jamani jaa liko wapi la kumwaga taka. Basi wale jamaa wakasema, nyinyi mnatoka pwani taka mkazitupe huko huko pwani mnakuja kutupa huku juu. Kwa sababu hatujui kwamba kumwaga taka pwani ni kuharibu mazingira na kuharibu samaki.

Kwa hivyo, naomba tui-*support* wizara hii na idara hii tuweze kuuza samaki wetu kwa ajili ya chakula na utalii, pomboo, kasa na kadhalika na kukuza mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache bahati mbaya muda ni mfupi sana, naomba kuunga mkono mswada huu mia fil mia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba tujitahidi tuchangie kwa ufupi kwa sababu tunatakiwa leo tufanye majumuisho asubuhi hii ili jioni tuendelee na hoja za kamati.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza kwa kukalia hicho kiti hapo. Wanawake tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, maneno mengi yameshasemwa ambapo wenzangu waliosema walikuwa wanasema hili limeshasemwa, uvuvi wa bahari kuu kibiashara limeshasemwa kwa hivyo sitokuwa na haja ya kulisema. Lakini mimi nasemea kwenye mikandaa (mikoko).

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli sehemu za kandaani kama tunavyoita kule kwetu Pemba basi hizi zimeharibiwa sana. Mfano wangu mzuri sana uko hapa pwani mbovu Kinazini. Hapa maji yakitoka utafikiri pale ni jaa la kutupa mifuko, ile mifuko iliyotupwa zamani mpaka leo ipo, tuliambiwa kwamba hii inaleta athari. Kwa hivyo, mpaka leo ipo na kwa sababu tunaambiwa sehemu za mikandaa ni mazalio ya samaki na viumbe vyengine hai vya baharini, basi kutokana na ile mandhari iliyokuwepo pale ya mifuko mingi ya plastiki hapa hapazaliwi tena samaki, samaki hawaji tena hapa kuzaliwa. Kama wanakuja basi kwa sababu ya sumu ya ile mifuko wanakufa. Sasa ile faida ya kuwepo

mikoko pale Kinazini haipatikani kwa ajili yaku-*feed* ile bahari kuu kule iliyoelekea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoiomba wizara hii ishirikiane na Manispaa wafanye mipango ya kusafisha lile eneo la mikoko pale Kinazini na sehemu nyengine kama ziko zilizoathirika na mambo haya basi ziweze kusafishwa ili samaki waweze kupata mazalio yao.

Mhe. Mwenyekiti, bado samaki wadogo wanavuliwa lakini wanavuliwa kwa sababu ya unyonge. Mimi nilikuwa nikifanya kazi redio na nilikuwa mfanyaji wa vipindi hivi vya mambo ya kilimo na uvuvi. Huyo bwana aliyekuwepo siku hizo Mkurugenzi nimeshamsahau jina lake namjua kwa sura tu. Huyo alikuwa anafuatilia sana juu ya kuvuliwa samaki wadogo, lakini alikuwa anashindwa kwa sababu wakishakuvuliwa sheria zenyewe zilikuwa hazikukaa vizuri, kwa hivyo alikuwa hata hajui afanye nini. Lakini nadhani sasa hivi sheria zimekaa vizuri, tuwaelimishe basi wavuvi athari ya kuvuliwa samaki wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda na Kamati katika bandari moja iliyoko Pemba kichochoroni huko, pale Chake-Chake ukishakupita Mchanga wa Kwale unateremka chini huko mabondeni. Kwa kweli tukenda unaona huruma vile visamaki viduchu vichanga, vitasi, vichangu vilivyotupwa. Vimetupwa kwa sababu haviliki lakini ndio vimeshavuliwa kutoka baharini vimeshakufa havifai tena. Kwa hivyo, tumevidhulumu vile visamaki kwa uhai wao na tumejidhulumu sisi wenyewe maana samaki wale tungeliwaacha kule baharini wangekua na baadae tukapata samaki wazuri.

Kwa hivyo, hii elimu itolewe kwa wavuvi wetu wanaokwenda baharini. Si wavuvi tu, watoto wanaokaa kando kando ya bahari hizi pia nao wana mtindo wa kuvua samaki wadogo wadogo hawa waliokuja kuzaliwa kwenye kandaa. Wao wanakwenda na mishipi yao au na vipakacha vyao wakiwakuta hao wanawaokota wanawatia ndani ya pakacha. Huu ni uharibifu, kwa hivyo watu wote wanaokaa Songosongo ya bahari wao pamoja na watoto wao waelimishwe juu ya athari ya kuvua vijisamaki hivi vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, uchafuzi wa bahari na utupaji wa taka kaueleza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui sina haja ya kurudia tena. Vile vile tatizo moja nililonalo sasa hivi ni kupotea kwa samaki Zanzibar. Kuna aina mbali mbali ya samaki wameanza kupotea hapa Zanzibar wakiwemo kolekole ni kidogo tu waliopo, mkundaji nao wanapotea potea ni wachache tu waliopo na wengine wengi wanapotea.

Sasa wakati umefika wa kurejesha hizi aina za samaki kwa sababu sio kama wamepotea kabisa lakini wapo wachache. Kwa hivyo, mamlaka hii kwa

kushirikiana na taasisi nyengine za ufugaji wa samaki wawafundishe wananchi kufuga samaki hawa wadogo wadogo, yaani hawa wanaoanza kupotea ili baadae warejeshwe baharini. Au tuwe tunafunga basi kama watu wa Kusini wanavyofunga pweza kwamba samaki wa aina hii sasa hivi ni marufuku kwa Zanzibar kuvuliwa, kama tunavyopiga marufuku kasa kilimwengu.

Sasa na sisi ndani ya nchi tukiona aina ya samaki inaanza kupotea basi tuipige marufuku japo mabavua manne kwanza wasivuliwe ili wazaliane na kuwa wengi, wazuri na wakubwa halafu tuendelee kuwavua. Lakini kuna samaki tukifanya masikhara kidogo basi wanapotea hawa Zanzibar na ni samaki ambao tunawapenda sana.

Mhe. Mwenyekiti, zamani wakati wa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi aliwahi kuweka Skuli ya Fidel Castro kuwa ni skuli ya Kilimo na akaweka Skuli ya Lumumba kuwa ni skuli ya Uvuvi kwa sababu palikuwa hapana matayarisho mazuri hii *curriculum* haikuendelea mbele. Lakini nje ya skuli basi kuna haja ya wizara hii inayoshughulika na mambo ya uvuvi pamoja na wakulima, wakulima wameshawekewa chuo, lakini wavuvi au mtu anayetaka kusomea mambo ya uvuvi basi aende katika chuo hiki asome. Ni muhimu sana kuwa na chuo Zanzibar kwa ajili ya kusomesha watoto wetu, ili wao watakapokua wasivue kama wanavyovua wazee wao uvuvi wa kizamani ambao hauna tija kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine hivi sasa kwa sababu hatuna chuo na nimesema kule juu kwamba wavuvi basi wapewe elimu ya uvuvi wa kisasa wafuatwe huko huko vijijini waliko. Wafanyiwe japo semina ndogo ndogo hapo hapo chini ya miembe, huko huko katika sehemu zao za kazi, basi wafundishwe namna ya kuvua kisasa katika hayo hayo maji ya ndani tunayovua hivi sasa kwa kupata kitoweo. Wafundishwe namna ya kuvua kisasa sio uvuvi ule ule wa kizamani tu uendelee. Japo vyombo vyao ni vidogo lakini wakenda baharini basi warudi na samaki ambao ni wazuri.

Mhe. Mwenyekiti, zamani jamaa zangu wa Kikojani bahari ilipokuwa haijachafuka wao walikuwa wanajua kwamba ukenda mwamba fulani basi unapata changu watupu, akiingia mwengine basi inakuwa kosa. Lakini sasa bahari imechafuka basi wakenda huko baharini na wao wanatuletea mchanganyiko tu wa samaki wengine hata hawajakua vizuri bahari zinaharibika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna huu uvuvi haramu wa nyavu za macho madogo, watu wengi ndio nyavu wanazozitumia hizi. Sasa kama tunataka kubadilisha watumie nyavu zinazostahiki basi wanyang'anywe nyavu hizo haramu lakini wakati huo huo wapewe nyavu halali ili waweze kuendeleza mbele maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, halafu utafiti wa kisayansi ufanywe kujua uharibifu uliofikiwa baharini na namna gani tutairudisha hali ya bahari yetu kuwa nzuri na tuweze kuvua samaki kama wazee wetu walivyokuwa wakivua zamani.

Mhe. Mwenyekiti, mengi ninayo lakini muda ni mfupi, ahsante kwa hayo machache.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Nina mambo mawili nakiri mwenyewe kwamba nitasema kidogo na *wallahi* hutonihimiza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nakiri kwamba ninaona raha kuwa mwanafunzi wangu uko hapo juu na mimi niko huku. Naona raha sana, naona furaha, natafahari, raha ninayoiona hainunuliki kwa pesa, maana yake hata nikiwa na pesa nikitaka kununua raha namna hii *wallahi* siioni. Ninavyoiona kwako wewe na Mhe. Juma Duni Haji, naona raha sana *wallahi*.

Sisi walimu wa zamani tulikuwa hatuibi kitu, mimi niliwahi kuiba mara moja tu chaki nikatia katika viatu vyeupe basi, chaki nyeupe nikaivuruga nikatia katika viatu vya raba. Lakini raha yetu wanafunzi wetu mpate, kwa hivyo nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema mengi lakini nitasema kidogo kwa sababu nimeahidi. Nimefurahi kwamba Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ni mtu *muhitahid*, ni mtu anayejiamini kama alivyosema Mhe. Juma Duni Haji na anakijua anachokinena na akisema unatamani kumsikiliza. Anapata *mass* sana kusikilizwa shamba kwa sababu ya *presentation* yake, lugha yake na namna anavyojumuisha jamii. *He could be a very good politician* angetaka lakini asiwe, namna anavyowa-*win* jamii katika kuwasomesha.

Kwa hivyo, somo la samaki na awareness ya samaki na bahari imenyanyuka kiasi kikubwa sana. Imenyanyuka kwa picha, imenyanyuka kuwajulisha watu. Wengi sisi tumeanza kuona *beauty* ya bahari yetu, *gardens* ziliomo katika mafunzo yake na namna ya samaki waliomo. Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana katika hii yote.

Lakini nilitaka kumuuliza na kumwambia na kumuomba kwamba katika utafiti mimi *wallahi* sijui, kama nyinyi mnajua nyamazeni kimya. Hawa samaki hawawezi kufanyiwa *cross breeding*. Nimeona *cross breeding* ya nchi kavu imefana sana. Nimepata kusikia kwamba wako aina ya samaki wanamwaga

mayai sijui kama ya *male* au ya *female* halafu anapita samaki *male* yanakuwa *consumed* ndio inakuwa *mating* imefanywa.

Lakini huyu huyu kanionesha picha samaki wako katika majabali kama wanafanya mating *wallahi* mimi sifahamu ipi ndio inayo-*produce* samaki. Mmoja anatoa mayai mwengine ana-*consume* na samaki wanazaliwa, au wako aina ya samaki wanafanya *mating*. Ikiwa hivyo ndio kweli basi haifanywi *cross breeding* ya samaki. Hawezi kufanya *experiment* ya *cross breeding.*

Nataka ku-*imagine* kwamba nduaro ikifanywa *cross breeding* na chewa au na kanadi atatoka samaki wa aina gani, atakuwa mtamu, mkubwa, au atakuwa vipi. Maana yake ninafuata nilivyosomeshwa mimi. Mimi nimesoma *budding* na *grafting* tumeona raha. Katika *budding* unachukua muembe wa aina hii na muembe wa aina hii, au mmoja unaukata unabakisha mmoja ndio mzuri au mwembe mmoja utowe embe kumi na mbili. Skuli tumefundishwa sijui *grafting* ile unachukua mchungwa na mdimu unafanya na nimewahi kuona mlimau una malimau na machungwa katika kusomeshwa. Je, katika samaki haiji hiyo, maana yake ikija nataka ku-*imagine* sasa changu wanazaa changu, wanafanya *mating* au wanamwaga mayai na mayai ya changu lazima ayaokote changu hawezi kuyaokota chewa likatoka samaki ambalo halijulikani namna yake. Nimetaka kujua hii. Hilo moja.

La pili nimetaka kutoa mfano wa *cross breeding* ya hapa. Sisi hapa haikuwa ajabu huyu kumuoa huyu na huyu kumuoa huyu na kilichopatikana na *a sort of cross breeding.* Waafrika waliowazaa Wahindi *product* yake nime-*prove* ni *first class*. Walioana kwa hiyari yao wala hapakuwa na kuoana kwa nguvu hapa, palikuwa na kuoana kulikohimizwa ili jamani tupate kuwa na jamii nzuri, tupate jamii isiyotengana na tupate jamii iliyofahamiana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Thabiti Kombo alimuoa mama wa Kihindi, *product* hii hapa mtu *intelligent,* mkubwa, *a true businessman*, katanda kila pahala *very intelligent.* Akimwambia mtu kitu anakubali akitaka asitake, kajaaliwa na mdomo huo *is a good product*.

Mhe. Mwenyekiti, wa pili ni marehemu Ahmed Said kamuoa mama wa Kihindi, kama mnawaona kina Simai wale, wote ni watoto *intelligent, business minded* na wako *smart* katika kila kitu.

Ibrahim Makungu kamuoa mama wa Kihindi mwengine *product* yule nadhani anaitwa Hussein, ana mahoteli na hivi sasa yuko Pemba ana shughulika na mambo ya hoteli na kawa anajitegemea na kila kitu. Katika samaki hakuna basi tukapata samaki lenye nofu kubwa. Maana yake hiyo nimetoa mifano midogo

sana, nyinyi nyote mnaijua mingi zaidi. Mnaijua mingi kuliko hii na *product* zake zote zimekuwa namna hii.

Sikuambii hawa mapapasi wengine wamepata mapapasi wenziwe, maana si watalii ni vishuka wamepata na wamezaa *product* anakuja mtoto *cad berry* rangi yake inakuwa ni *cad berry* na rangi ya *cad berry* ni adhimu, *is not black, is not white is cad berry*. Rangi ya *cad berry* kila mmoja anaipenda. Mhe. Mahmoud anaipenda *cad berry*, haipendi hiyo *white* aliyokuwa nayo anaipenda *cad berry* na watoto wanakua *health*, wazuri na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi Waswahili tukioana na Waswahili tunapata kitu kama hicho bila shaka, lakini nakuja katika *cross breeding*. Sasa ikiwa inawezekana kufanya majaribio ya *cross breeding* kama inafanywa *drafting* na *binding* basi nadhani tutaweza kupata *product* iliyokuwa nzuri.

Halafu jengine ninalotaka kukuuliza, kule Funguni wale jamaa zetu wa Kichina, ambao nao pia kuna Mchina mmoja kamuoa mtoto wa sijui Mheshimiwa, basi watoto wake wote *intelligent*. Mhe. Maua Daftari sijui kamuoa nani? Wana tambi, maduka ya *petrol* na kila kitu kwa sababu ni *product* zao nzuri sana na watoto wote wazuri. Kwa hivyo, nataka kukuuliza wale walikuwa wakikusanya mapezi ya papa? Hawa papa hawa, walikuwa wao wanataka mapezi tu! Nyinyi kuleni papa wenu na walinunua kweli kweli je, yalikuwa yakifanyiwa nini? Fisheries hawayajui wao wakayataka wakanunua.

Halafu kuna ule uvuvi wa majongoo nao yanafaida gain? Supu yenyewe tunakunywa sisi au inauzwa nje? Basi mbona hatukusanyi hatushughuliki na wavuvi wa jongoo wapo, hayafugwi na kufanywa kila kitu Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti ninataka nije kujibiwa vizuri na Mhe. Waziri kama ni *possible* kufanya *cross breeding* ya samaki. Maana yake *cross breeding* ya watu tumeiona.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati nakupeni mfano mmoja mzuri. Walikuja watu wa *fisheries* hapa Unguja mwaka 1965 au mwaka 1966 wakaonana na marehemu Mzee Karume, wakaenda wakaonana naye hasa na wakamwambia hivi. Mheshimiwa tumekuja bahari ya Zanzibar ni nzuri, ina aina kwa aina ya samaki wazuri tena wa namna ambayo kwengine hawapatikani. Tumekuja tunafikiria kuja kufanya *cross breeding* na utupe ruhusa kabisa. Aliyeniambia mimi ni mwandishi wa habari aliyekuwepo siku hiyo, sisemi *story*. Akamsikiliza, mwisho akamwambia, haya nimekusikieni, sisi tumeendelea zaidi mbele tunafanya *cross breeding* ya watu Muhindi anamuoa Mswahili *product* inakuwa kubwa, Mwarabu anamuoa Muhindi *product* inakuwa kubwa,

sisi tumeendelea kwa *cross breeding*. Nyinyi tuambieni njia ya kuwafua *tuna* tukapata *foreign.* Wakateremka ngazi wale wakaenda zao.

Kwa hivyo, ilikuwepo hiyo *cross breeding* hao watu waliokuja wa *fisheries* walitoka Dar es Salaam hapo wakaja kufanya. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hii hoja, na napenda kusema kwamba haya mawili niko *curious* kweli kweli kujibiwa kwa sababu nimeiona *cross breeding* ya hapa nchi kavu imefana sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nitajaribu kwenda haraka haraka kwa sababu ya muda. Lakini hata hivyo naomba kidogo univumilie.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu kwanza naomba twende katika kifungu cha 2 ambacho kinasema kwamba 'sheria hii itatumika Zanzibar'. Sasa mimi naomba hii irekebishwe kidogo ili ionekane kwamba katika hiki kifungu cha 2 sheria hii itatumika Zanzibar pamoja na yale maji yake ya ndani na ile *exclusive economic zone,* ili tuweze kukinga wale watu wengine ambao wanaweza wakatumia *exclusive economic zone*.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo lakini baadae kidogo nitaelezea ni kwa sababu gani.? Lakini katika kifungu cha 4 nilikuwa na wasi wasi kidogo, ambacho kinasema;

Kifungu cha 4

"Kutakuwa na idara itakayojulikana kama idara ya uvuvi",

Halafu kuna kazi za idara na kuna mkurugenzi wa idara ambaye ameteuliwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri sio lazima sana kuiainisha idara ya uvuvi, kwa sababu kwa mujibu wa katiba kifungu cha 55, Rais anao uwezo wa kuunda idara yoyote na ndio maana kuna idara nyingi hapa na wala hatuziweki katika sheria. Ingekuwa hii sheria tunataka kuifanya mamlaka ambayo ndio kitu kizuri zaidi, basi naamini tungeweza zaidi kusema kutakuwa na mamlaka na mkurugenzi tukampa nguvu zake ambazo tunaweza kumpa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapo itapingana. Maana yake unaposema kutakuwa na mkurugenzi ambaye atakuwa Afisa Mtaalamu katika fani ya uvuvi na halafu mkurugenzi atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa idara. Sasa ukishakusema hivi katika sheria, ina maana hawezi tena kuja katibu mkuu akaja akamuingilia katika idara yake, kwa sababu hapa tumeshamuidhinisha kisheria kwamba yeye ndiye mtendaji mkuu. Kwa hivyo, ni tofauti na idara nyengine ambazo zile zote

zimewekwa kikatiba na waziri au Waziri Kiongozi ndiye mwenye mamlaka ya mwisho katika idara za serikali. Kwa hivyo, hilo ni moja muhimu ambalo nafikiri tungeweza kulitafakari.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ukija katika kifungu cha 14(1) ambacho hiki ni muhimu sana na naomba Mhe. Waziri, na nimefurahi kwa sababu Mhe. Waziri Kiongozi yupo. Kifungu cha 14(1) kinasema kwamba;

Kifungu ch 14(1)

> "Chombo chochote cha uvuvi kinachofanya kazi katika maji ya ndani, maji ya nchi na eneo la ukanda wa uchumi wa Zanzibar bila kujali ukubwa wake au njia ya uendeshaji ni lazima kikatiwe leseni".

Sasa tatizo linalotokezea hapa ni kwamba ukanda wa uchumi wa Zanzibar umetajwa katika sheria hii, lakini ukanda wa uchumi wa Zanzibar hapo wala haueleweki. Kwa sababu katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ime-*define* eneo la Zanzibar na katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 ime-*define* eneo la Jamhuri ya Muungano zote ukanda wa uchumi haupo, haupo kwa sababu gani. Kwa sababu huu ukanda wa uchumi *exclusive economic zone*, ulikuja mwaka 1988 katiba zote mbili zimeshatungwa. Kwa hivyo, mwaka 1988 ilipokuja hii ikawa Zanzibar kwa mfano katika kifungu cha 2 cha katiba kinasema;

Kifungu cha 2

> "Eneo la Zanzibar ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba na visiwa vidogo vidogo vilivyoizunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar".

Sasa hii inakwenda mpaka 12 *nutrical miles* tu, zile *territorial water* na Jamhuri ya Muungano ndio hivyo hivyo. Lakini ilipokuja ukanda wa uchumi azimio hili la *united nation* 1988 wenzetu Tanzania Bara wakafanya haraka haraka hii sheria ya *territorial sea and exclusive economic zone*. Kwa hivyo, sheria hii wao wakaichukua wote ule ukanda wa uchumi kwa mujibu wa azimio hili la *exclusive economic zone.* Sasa baada ya kulichukua ina maana kwamba hata Zanzibar hawawezi kufanya chochote mpaka wapate ruhusa kutokana na sheria hii ya mwaka 1989 na mbaya zaidi ni kwamba sheria hii iko katika wizara ya mambo ya nchi za nje, kwa sababu imesema wazi kwamba *minister for foreign affairs*.

Kwa hivyo, utaona sheria hii inatawaliwa na waziri wa mambo ya nchi za nje. Kwa hivyo, hata ile *exclusive economic zone* haiwahusu watu wa kilimo wala

haiwahusu watu wa wizara ya maji na nishati, kwa sababu iko katika wizara ya mambo ya nchi za nje. Lakini na mbaya zaidi utaona katika kifungu hiki katika sheria hii kifungu cha 8 ni kwamba huyu waziri wa mambo ya nchi za nje atazungumza na *director of land survey* katika *ministry* inayohusiana na *lands* ya Tanzania, ili kufanya *demarcations* ya maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo sisi kusema kweli itakuwa hatuna letu kisheria. Nini cha kufanya Mhe. Mwenyekiti, ili kujiokoa katika tatizo hili. Ndio hapa nikasema kifungu hiki cha 2 cha sheria kwanza tuseme kwamba sheria hii itatumika Zanzibar pamoja na maji yake ya ndani pamoja na *exclusive economic zone.* Hiyo ya kwanza.

Lakini ya pili wakati wowote Mhe. Mwenyekiti, tutakapobahatika kufanya marekebisho ya katiba yetu, ni lazima eneo la Zanzibar tuli-*redefine* ili kuwa-*accommodate* suala hili ambalo ni muhimu sana. Kwa hivyo hilo Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu kwa sababu hata tumesema kwamba mafuta ni ya kwetu na vitu vingine vitakavyoonekana katika *economic zone* ile ni ya kwetu. Lakini hawa wenzetu wakija wakiwa wagumu kidogo, *minister of foreign affairs* ndio mwenye dhamana, na ndiye atakayefanya mambo haya yote. Kwa hivyo, kwa kuokoa hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba ni lazima tuyaone hayo ili tuweze kurekebisha kwa faida yetu na kwa faida ya vizazi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka, katika kifungu cha 17 kinazungumzia suala la vitu ambavyo vinakatazwa kuwanavyo mtu. Lakini katika kifungu cha 17(2) hakija zungumzia kama vitu vile vitaonekana ndani ya nyumba ya mtu. Kwa hivyo, mimi nafikiri sheria hii ya kifungu hiki kingerekebishwa, ili hata vile vitu ambavyo vimepigwa marufuku katika sheria, lakini vikaonekana katika nyumba basi navyo vitakuwa ni matatizo na muhusika atakuwa ni mkosa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuharakisha basi nilikuwa nasema kwamba kifungu cha 6 cha sheria ambacho kinazungumzia mkurugenzi, basi tukitizame tena katika mantiki ile ya kwamba idara zimo katika katiba tayari na ni idara hii tu ambayo imepewa nafasi hiyo na suala hilo linampa nguvu zaidi mkurugenzi ambapo kama tunataka kufanya hivyo, basi bora tufanye mamlaka.

Pili ni hili suala la *exclusive economic zone* ambalo halimo katika sheria hii, basi tuliweke katika sheria hii ili angalau tuweze kuwanacho cha kuanzia. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umeshaanza kunitizama nakushukuru. Ahsante sana.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na nakupongeza kwa nafasi hiyo ambayo ni fahari kwetu sisi wanawake katika Baraza hili. Kwa sababu ya muda Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda niende

moja kwa moja katika mchango wangu ambao kwa kweli ufafanuzi wake ni huu ambao Mheshimiwa kiongozi wangu wa upinzani ameutoa.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii au mswada huu uliopo mbele yetu kwa asilimia mia kwa mia, lakini nilisema kwamba katika mchango wangu huu sheria hii naungana na wale wote ambao walisema kwamba imechelewa. Imechelewa kwa sababu sasa kumekuwa na changamoto kubwa mbele yetu kama ufafanuzi ambao uliotolewa na kwa bahati wenzetu wametangulia kutunga ile sheria yao ya nambari 22 ya mwaka 2003, kidogo inakuwa haikuzingatia kwamba kuna Zanzibar, walikuwa wamejikumbizia kila kitu. Kwa hivyo, ufafanuzi zaidi Mheshimiwa kiongozi wangu wa upinzani ameshautoa, kwa hivyo nisingependa hapa niendelee zaidi. Lakini mantiki imepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hiyo ndio ile ambayo wengine tulikuwa tunapendekezo kwamba hata katika ile kamati yetu ya kuzungumzia mambo haya, basi watu kama Mhe. Abubakar si watu wa kuachwa, kwa sababu tunaangalia faida na maslahi ya nchi na sio itikadi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu ambao nitakuwa nakwenda zaidi kijumla jumla, naangalia suala zima la hii *economic zone* na jinsi ambavyo uvuvi wetu tuliokuwanao. Wengi wametangulia kusema kwamba hata hii maili 12 *nautical miles* bado hatujazikava. Lakini mimi nadhani hilo halitokuwa tatizo sana. Zaidi nilikuwa napenda kuona kwamba baada ya marekebisho mazuri ambayo Mheshimiwa kiongozi wangu wa upinzani ameyapendekeza, basi tuone ni jinsi gani tunaweza kuutumia ukanda huu ili kuweza kupata faida kwa nchi.

Miongoni mwa faida nilikuwa napendekeza kwamba kama kifungu cha 5(f) katika ukurasa wa 3, kuwena utafiti pia wa kujua aina za samaki ambao wamo na si samaki tu, lakini kuna rasilimali nyingi. Kwa hivyo, huu utafiti uwepo ili tuweze kujijua kwamba tuna hazina kiasi gani katika shamba hili la bahari.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tuangalie suala zima kama ambavyo imeelezwa humu katika kifungu cha 13 kuhusiana na ridhaa ya maandishi kwa mgeni. Kwamba mgeni atakapotaka kufanya uvuvi katika eneo hili basi kuwe na ridhaa ya maandishi. Mimi nasema isitoshe tu kuwa ni ridhaa ya maandishi, lakini kuwe na makubaliano ya kugawana mapato. Kwa sababu hili eneo ni letu, mtu akitaka kuja kufanya anayoyataka kufanya basi tukubaliane kuwa unapokuja kuvua katika eneo hili hatimaye basi tugawane hayo mapato kwa asilimia. Sasa tutatizama wenyewe kama tayari tumeshajiwekea viwanda vya kuweza ku-*process*, kama tutachukua shehena ya samaki na ku-*process* katika

viwanda vyetu, halafu tutowe kama ni bidhaa za Zanzibar ama tutasubiri kupokea mafedha kama hili jambo pengine hatujajiandaa vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo Mhe. Abass Juma Muhunzi jana alilisema kwamba wenzetu Bara wameuchukua mwaka huu wa fedha wakaupa *slogan* ya kwamba kilimo kwanza. Mimi ninakubaliana naye sana kwa upande wa Zanzibar kwa sababu tuna ardhi ndogo, lakini tuna eneo kubwa la bahari, basi tuweke *slogan* ya kuwa na uvuvi kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia na tukajiwekea mikakati mizuri kama serikali na tukajipanga kwamba tutaitumia vilivyo kwa kuwa na viwanda na mambo mbali mbali ambayo wenzangu waliotangulia wameshayazungumza, basi nadhani tunaweza tukaona jinsi gani nchi yetu inaweza kujivunia suala zima la kuwa na bahari na kwamba tunaitwa kisiwa na tukaweza kuwa na maisha mazuri pamoja na mafanikio makubwa kwa kupitia bahari na mambo mengine kama utalii yakawa ni nambari 2 na nambari 3 yakaja mambo ya kilimo, ambacho kwa kweli ardhi yetu ni ndogo na hali halisi ya kimazingira inavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilitaka kuzungumzia suala la uchafuzi wa mazingira ya bahari. Nakumbuka tulivyooneshwa na mkurugenzi ambaye na mimi naungana na wenzangu kumpongeza kwa kazi zake nzuri pamoja na watendaji wake. Kuhusu suala zima la ujenzi wa mambo ya jet kwa wale wawekezaji waliokuwa na mahoteli. Hili ningependekeza kwamba kutokana na athari ambazo zinaonekana, wale waliojenga jet basi tuone utaratibu wa kupiga marufuku yale ma-jet ambayo hayafai na ambao wanahisi wana haja ya kuendelea nayo, basi wawekewe masharti maalum na namna ya kujenga jet kama ambavyo tulioneshwa hapa katika semina. Mhe. Mwenyekiti, kumbe inawezekana kujengwa jet lakini zikawa na maumbo maalum ambayo yanakubalika.

Jengine ni suala zima la wavuvi ambao wanatumia nyavu. Hata kwa zile nyavu ambazo zinakubalika Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina pendekezo kwa sababu ya kuweka mazingira ya bahari vizuri basi wakajulikana na labda mvuvi anapogundua kwamba nyavu yake imepotea, basi pakawa na sehemu maalum ya kuripoti haraka ili yakaweza kutafutwa. Tumeona athari ya nyavu ambayo imepotea miaka mingi iliyopita jinsi ilivyoharibu mazingira ya kule baharini. Kwa hivyo, nilikuwa naona kuwa hilo lisiwe tu ni jambo la kusubiri tukatafuta mtaalamu kuja kuitoa na katika kufanya hivyo pia kuna maharibiko ya namna moja au nyengine, basi iwe ni suala la kufanyiwa kazi mapema ili kuepusha athari ambazo zinatokea.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili kwa haraka haraka napenda pia kutaka kujua zaidi kuhusu kisiwa kinachoitwa Latham Island, kama sikosei wengine wanakiita Fungumbaraka. Ilielezwa hapa kwamba kuna rasilimali nyingi za juu na chini, kwa sababu chini kuna mambo haya ya matumbawe mazuri mazuri na mabustani ya kupendeza na samaki wengi, lakini juu kuna ndege wa aina nyingi sana ambao wanapatikana katika kisiwa hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napenda sana Mhe. Waziri atueleze katika suala hili wanafanya vipi, kwa sababu wengine wanazungumzia utata kwamba kisiwa kile ni chetu au si chetu. Lakini kwa mujibu wa tulivyofuatilia na kusikia mengi yakizungumzwa ni kwamba hiki kisiwa ni cha Zanzibar, na tangu kabla ya utawala wetu yaani kabla ya Mapinduzi ilikuwa kisiwa hicho hata mfalme alikuwa anakwenda kila baada ya wakati na anakwenda na kuweka bendera pale. Hayo yalifanyika hata baada ya Mapinduzi. Kwa hivyo, ningependa kuona kwamba haki, mali na rasilimali za Zanzibar hazipotei. Kwa hivyo, hili lingefuatiliwa na tukaelezwa haswa kwa uhakika mambo haya yanakwendaje?

Mhe. Mwenyekiti: Malizia mheshimiwa.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante. Katika hilo sambamba Mhe. Mwenyekiti, ningependekeza pia kuwe na ulinzi ambao utaweza kuona mambo mengi ambayo yanatokezea mara kwa mara tunasikia wanakuja watu kutoka nje wanavuna rasilimali zetu wanaondoka, lakini kuna mambo mengi ambayo yanatokea na tunachokuja kugundua baadae huwa ni maharibiko ambayo tayari yameshatokea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda Mhe. Waziri aje kuniambia sasa kuhusiana na suala zima la kile kifungu cha 22 cha kuvua samaki wadogo. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui hapa ameeleza vizuri, wenzetu wakivua anapimwa ikiwa hajatimia anarudishwa. Lakini huku kwetu nadhani hilo jambo kidogo linamtihani, sasa usimamizi wake utakuwaje katika kuweza kuona tunahifadhi samaki wadogo nao waweze kuishi kule baharini mpaka wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nina mambo mengi sana, lakini nashukuru kwa kupata haya machache. Kwa hivyo, naunga mkono mswada huu nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Ame Ussi Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nategemea *Inshaallah* nitachunga huo muda. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na sisi wajumbe sote tuliohudhuria hapa. Pia naungana na wenzangu kukupongeza wewe kwa dhati kwa kukalia kiti hiki.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo niende kwenye wizara nayo niitupie pongezi zake kwa jitihada zake za kuona nini tufanye hapo mbele kwa kupitisha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi pia nampa mkurugenzi pamoja na watendaji wake kwa kuweza kusimamia na kuratibu sheria hii ambayo tunaizungumza hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa yale majimbo ambayo yana wavuvi wengi sana na tunaotumia bahari kwa wingi. Ukiangalia katika vijiji vyangu vyote au shehia, basi kila shehia ina bandari yake. Kwa hivyo, tunafarijika sana kwa shehia hii ambapo ikipita na kuanza kutumika rasmi basi tutafarijika kwa sababu wakulima wetu ni wa baharini wengi, kama walivyosema kwenye semina kwamba tunalima baharini. Kwa hivyo, sisi ni wakulima wa baharini kuliko wakulima wa juu, ukizingatia ardhi yetu ni ya mawe.

Mhe. Mwenyekiti, bandari au madiko tunayo mengi Kigunda, Kendwa, Jomba, Kisanakali Kikokwe, Kidoti, Fukuchani na kwengineko. Hizo zote ni bandari nategemea mkurugenzi anazifahamu kwa vizuri sana. Ukija kwenye mitego, pamoja na mengi ambayo wenzangu wameshazungumza, lakini tukizingatia hasa kwa upande wa mitego, bado mitego hiyo ya uvuvi kwa sehemu zetu ni kidogo, wavuvi wengi na mitego hawana. Kwa hivyo, ikija sheria hii Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja na sisi tupate hiyo mitego kabla haijapita sheria, ina maana watu watakuwa wameshajitayarisha na kupata uvuvi ule ambao unatakiwa usiokuwa haramu.

Mhe. Mwenyekiti, pia ukiangalia katika sheria hii imezungumza mengi, kuna masuala ya uvuvi huu wa bahari kuu ambao tayari wenzangu wameuelezea kwa kina. Lakini mimi nataka nizungumzie kitu kimoja, kuna kifungu hapa kimezungumza katika ukurasa wa 11 katika mstari wa 5, ambao unazungumzia mgeni, maana yake ni mtu ambaye si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au shirika ambalo halikusajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kusema kwamba mtu yeyote ambaye ameshazungumzwa mgeni hakusajiliwa Zanzibar. Kwa hivyo, nafikiri watu wa Zanzibar wanasajiliwa Zanzibar, lakini sasa watu hao hao wanajaribu kwenda kuvua kule kwa wenzetu na vyombo vyao. Lakini wakifika kule pamoja na kuonesha zile stakabadhi zao ambazo ni za kusajiliwa lakini bado wanapata matatizo wanaambiwa kwamba nyinyi hizi hatuzitambui msajili upya. Kwa hivyo, ningeomba idara kwa kushirikiana na serikali basi ikaone kwamba tatizo hili na hawa wa Zanzibar kama ni Watanzania wanapokwenda kuvua kule basi waeleweke kwamba wamekwenda kuvua kama ni sehemu zao. Watu wengi wa kwetu wanaokwenda kuvua katika dago wanapata tabu hizo sana za

kusumbuliwa na inabidi wasajili upya kule Tanzania Bara, sasa na hili nalo lionekane.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kusema ni kuwa pia tuna mikoko nayo ni moja katika mazingira. Kwa hivyo, suala hili nalo wizara kwa kupitia idara yake wangepanga taratibu za kuona kwamba wanatoa ramani ya kila kijiji au ya kila shehia ambayo inamiliki mikoko ile ambayo tayari hivi sasa kuna vijiji ambavyo vinasajili. Kwa hivyo, kujua eneo hili ni la watu wa shehia fulani na tayari wameekeza kwenye masuala ya mazingira katika mikokoto. Hili nalo liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, swali jengine juzi kwenye semina kuhusu suala la Uvuvi wa Bahari Kuu. Mkurugenzi alionesha hapa makatibu ambao wanasimamia na mmoja akiwa ni Katibu wa Jimbo langu.

Kwa kuwa Mkurugenzi hakuweka ubaguzi wa aina yoyote kwa inavyozungumzwa. Kwa sababu yule katibu wetu ambaye amechaguliwa na wananchi ni miongoni mwa wanachama wa CUF, lakini watu wamemkubali kwamba ni katibu wao tena anafanyakazi kwa mashirikiano *(Makofi)*.

Kutokana na hali hiyo basi Mkurugenzi aliwaambia huyu atatufaa kwa sababu yeye ni mzaliwa wa huku Nungwi. Nadhani wengi wamemkubali pamoja na makatibu wenziwe.

Jambo jengine ambalo nataka kusema ni kwamba kutokana na sheria hii basi kwanza itolewe elimu kwa hizi Kamati za Uvuvi, waone jinsi gani ya kuweza kujipanga katika suala zima la uvuvi. Kwa sababu zipo kamati lakini bado hawajaelewa hasa kwamba wao mipaka yao katika kufanyakazi hizi, wengine ni wajumbe na hawajafahamu nini wanachotakiwa kufanya, kwa sababu tunakutana nao.

Nadhani ikizingatiwa hivyo nategemea baada ya kupita mswada huu wa sheria itakuwa kila mmoja atakuwa amejiweka vizuri katika kufanyakazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka sana anataka nisichukue muda wako niende kwenye Sehemu ya Tano kuhusu Hatua za Uhifadhi, kifungu kinasema Kitengo cha Uhifadhi wa Bahari. Kwa kweli, kitengo hiki kuna haja ya kupatiwa vifaa, kuwa na usimamizi mzuri baada ya kusimama sheria hii.

Jambo jengine la mwisho ni kuhusu kutumia baruti au sumu, hapa vile vile kuna haja ya kutolewa elimu ya kutosha kwa wavuvi, ambayo itawasaidia kujua madhara ya hizo baruti pamoja na sumu. Kwa sababu hivi sasa tunao wavuvi ambao tukiacha hao wa baruti, wapo wanaotumia mishare, utupa

wanatia kwenye pango kwa ajili ya kuwalewesha samaki na matokeo yake wale samaki wanakufa. Sasa hawa watu wanahitaji kupata elimu nzuri kwa ajili ya kuepusha uharibifu wa samaki wadogo *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nasema kwamba mimi pamoja na wananchi wa Jimbo la Nungwi tunaupongeza mswada huu pamoja na kuunga mkono kwa asilimia mia moja *(Makofi).*

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kukupongeza kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo adhim, tena inadhihirisha wazi licha ya kuwa mwanagenzi inaonekana kiti hicho utakimudu vizuri zaidi *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende haraka kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia na yangu mimi ni machache na zaidi itakuwa ni maswali kwa Mhe. Waziri kuliko kuuchangia mswada wenyewe, kwa ajili ya kupata uelewa mzuri.

Zanzibar kwa muda mrefu tangu wakati ule wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki ya kwanza imekuwa ni Makao Makuu ya Chuo cha Sayansi ya Bahari. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kuwa Chuo hicho bado kipo, kama kipo basi naomba aniambie Mhe. Waziri ni machango gani ambao tumeupata na kufaidika nao kama Zanzibar katika chuo hicho.

Katika mswada huu anatarajia ni mchango gani ambao tutaupata kutoka kwenye chuo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa Sheria ya Uvuvi ukiutizama kwa ndani, basi unaona hauleti yale matumaini makubwa sana ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa jumla. Nadhani zaidi nia yake ni kusimamia uvuvi ndani ya nchi, ambapo kwa kiasi kikubwa ni uvuvi wa kienyeji na kulinda rasimali za baharini.

Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri kama kuna matayarisho yoyote ya sera ambayo yanalenga kukuza uvuvi, ili uwe ni moja ya pato la taifa kama vile tunavyopata pato la utalii.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, haijawahi kutokea Mhe. Zahra Ali Hamad kuchangia kwa muda mfupi kama hivi, lakini najua anaheshimu muda. Kwa hivyo, ningewaomba na wengine wajitahidi kama Mhe. Mjumbe

nadhani tutaweza kuwapatia nafasi wote walioleta majina kwa ajili ya kuzungumza *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami nitakwenda haraka *Inshaallah* na wala sitaki niseme sana lakini naomba nikupongeze kama walivyokupongeza wenzangu.

Baada ya hapo nataka moja kwa moja niende kwenye mswada na jambo la kwanza ambalo nataka niliulizie kwenye kifungu cha 7(b) cha mswada kuhusu mimea maji, lakini katika tafsiri ya mimea maji inasema ni mimea inayopatikana katika maji. Sasa katika maji ya bahari iko mimea na vile vile baridi, yaani ya mito na mengineyo iko mimea. Kwa hivyo, nadhani tungetofautisha na kusema hapa katika maji ya bahari.

Lakini nikisogea mbele kidogo kwenye kifungu cha 7(d) kuhusu usafirishaji wa samaki. Kwa kweli dhana hii ya usafirishaji sina hakika kuwa imekusudiwa ni usafirishaji wa nje ya Zanzibar au nje ya nchi ya Tanzania. Kwa sababu wapo wanaovua na kwenda kuuza Kigamboni, sijui na wao wanaingia katika usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye kifungu cha 8(2) kama kawaida yangu kuna mambo mengine huwa yanabadilisha maana. Kwa hivyo, naomba paingizwe kituo kidogo katika mstari wa pili baada ya wakila rasilimali, yaani hapo kuwe na kituo hicho na halafu ndio iendelee uwezo wa wastani, kwa sababu kituo hicho ndicho kitakacholeta maana halisi ya kifungu hiki.

Kwenye kifungu cha 9 (1) (d) ambacho kinazungumzia kuhusu kuweka kikomo juu ya kiwango cha ukubwa wa umri, sifa na kadhalika za samaki wakuvuliwa. Mhe. Mwenyekiti, hapa niungane na Mhe. Mjumbe mmoja aliyezungumzia kwamba mtu anaweza kuwa anafuga samaki na anataka hawa samaki wadogo kwa ajili ya kwenda kuwatia kwenye bwawa lake iwe ni sehemu ya mifugo.

Je, akija akiwachukua si atakamatwa au kuna utaratibu gani utakaowekwa kwa mtu ambaye anataka kufuga samaki jinsi ya kujipatia samaki wadogo na kuwatia kwenye bwawa lake bila ya kukamatwa.

Vile vile hapo hapo kwenye kifungu cha 9 (1) (f) kuhusu kuzuia uharibifu na uchafuzi wa maji ya Zanzibar. Kwa kweli sijui maji ya Zanzibar yamekusudiwa yote ya ndani, nje pamoja na bahari kuu, kwa sababu hakuna *definition* ya maji ya Zanzibar, kwani yapo maji ya aina nyingi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kwenye kifungu cha 10 kuna maji ya ndani ya maji ya nchi. Kwa hiyo, hapa naomba na hii ya moja iondoke na iwe maji ya

ndani halafu kuwe na kituo kidogo na hii ya iondoke na iwe maji ya nchi na kuendelea.

Lakini kwenye kifungu hicho cha 10(2) kuna kukubaliana na masharti ya amri hiyo. Nadhani ingekuwa vizuri ikawa akubali masharti na sio akubaliane, kwa sababu kukubaliana mpaka kwanza mupatane ndio mkubaliane na hapa hakuna kupata akubali tu, ikiwa amekubali sawa na akikata basi.

Kifungu cha 11 kuhusu Habari ya Udhibiti wa Uvuvi wa Kienyeji. Swali langu je, tuna lengo la kuwa wavuvi wa kienyeji wasivue tena, kwa sababu tunataka kuudhibiti uvuvi wa kienyeji usitumike. Kama si hivyo, basi kifungu hiki kitengenezwe angalau kielekee kuwa wavuvi wa kienyeji wataelekezwa wavue kwa kutumia uvuvi wa aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 13 kinachohusiana na mgeni. Nafikiri kwa kuwasaidia wananchi wetu, basi tungelifanya huyu mgeni anayekuja kama ikiwezekana akashirikiana na mwenyeji katika suala hili.

Kwenye kifungu cha 14 (4) (b) kuhusu muuombaji atakubaliana. Nadhani nayo pia ingekuwa atakubali *(Makofi).*

Vile vile kwenye kifungu cha 14 (4) (c) kuhusu masuala ya leseni ambayo yatafuata Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Zanzibar. Kwa sababu hiyo Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Zanzibar siijui basi naomba niijue tu, hiki kitumbwi kidogo anachovulia mtu mmoja peke yake kitakidhi mahitaji ya sheria hiyo, maana yake huyu tutamfanya asivue tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuomba umalizie.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi kwenda mbio, lakini mambo ndio kama yalivyo. Kwa hivyo, naomba nimalizie kwa kusema mswada huu si mbaya, isipokuwa kuna mambo madogo madogo ambayo yangehitaji yaangaliwe na kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kuwa mimi naunga mkono mswada huu pamoja na marekebisho yake yaliyokwishafanywa na yatakatofanywa *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana na sasa tumsikilize Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin na Mhe. Said Ali Mbarouk hayupo. Kwa hivyo, natagemea tumalizie na Mhe. Ali Denge makame na kuna Mheshimiwa Mjumbe mmoja atanisamehe ambaye ni Mhe. Hija Hassan Hija, lakini Mhe. Ali Denge Makame itategemea na atakavyochangia Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kushiriki katika shughuli za Baraza lako tukufu.

Pili nachukua nafasi hii kukushukuru pamoja na kukupongeza kwa kukamata nafasi hiyo *(Makofi)*.

Vile vile napenda kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea mswada huu ambao utaweka masharti mazuri ya kuendeleza uvuvi pamoja na hifadhi ya bahari yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 12 kuhusu masuala ya madiko. Kwa kweli madiko yanaelezwa kwenye mswada huu kwamba yatakuwa chini ya wizara. Hivi sasa madiko ni moja kati ya chanzo cha mapato cha Halmashauri za Wilaya. Je, wakati huo yatakapokuwa chini ya wizara utaratibu huo utaendelea au ndio Halmashauri za Wilaya itakuwa zimeshanyang'anywa na chanzo hiki cha mapato katika shughuli zao.

Kwenye hayo madiko, hali ya madiko kama alivyoelezea Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwamba ni mbaya sana, kwa kweli hairidhishi kuendesha biashara ya samaki katika sehemu hizo. Sasa sijui wizara baada ya kupita sheria hii itachukua hatua gani za kuyaimarisha madiko hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 ambacho kinaelezea juu ya utoaji wa leseni kwa vyombo vya uvuvi vya kigeni katika maji ya ndani. Sasa katika utoaji wa leseni huo vyombo vya kigeni kwa maji ya ndani ya Zanzibar, basi nashauri kwamba idara ichukue hatua ili kudhibiti utoaji holela wa vibali hivi, ili kuwa mwanya na wavuvi wa kienyeji kuweza kushiriki au kuendelea na shughuli zao za uvuvi katika maji hayo ya ndani.

Nikiondoka hapo ninende kwenye kifungu cha 18 (3) cha mswada huu kinachoelezea juu ya adhabu atakayopewa yule ambaye amefanya kosa. Lakini adhabu hapo haikutajwa, yaani imeandikwa tu kwamba kutakuwa na adhabu atakayopewa mfanyaji kosa huyo. Kwa hivyo, nadhani ingekuwa vyema adhabu yenyewe ikaainishwa kama ni ya faini na kifungo au vyote viwili kwa pamoja.

Kwenye kifungu cha 19 (1) ambacho kinazungumzia kuanzishwa kwa kitengo. Sasa kitengo hiki kinachotajwa kwenye kifungu hiki basi ningependa kujua kitaongozwa na nani na huyo atakayeongoza kitengo hicho atatakiwa awe na sifa za aina gani.

Vile vile kifungu cha 23(3) kimeelezea juu ya kukamatwa vifaa na kuzuiliwa. Nauliza vifaa hivyo vitavyokamatwa na kuzuiliwa kwa muda gani na hatimaye itakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na kifungu cha 31(4) ambacho kinaelezea mambo mbali mbali. Nadhani ni vyema kwenye kanuni pangekuwa na kifungu kinachokataza uingizaji wa vifaa ambavyo vimepigwa marufuku, kwa sababu kama vifaa vilivyopigwa marufuku bado vitaachiwa kuingizwa nchini, basi wavuvi wataendelea kuvinunua na kuvitumia. Kwa hivyo, ili kuzuia ni vyema kwenye utungaji wa kanuni kukawa na kifungu kinachozungumzia upigaji wa marufuku wa uagiziaji wa vifaa hivyo.

Tukiangalia kwenye mswada huu hauoneshi namna gani ya kumsaidia mvuvi wa kienyeji na kuwaendeleza. Sasa nifikiri ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi atueleze vipi wamekusudia muendeleze mvuvi wa kienyeji, ili angalau aweze kuingia kwenye maji ya nchi.

Kwa sababu hivi sasa takriban wavuvi wetu wote wanatumia maji ya ndani na kidogo ambao ni wachache sana, ndio wanaoingia katika maji ya nchi na kwenye ukanda wa uchumi ndio hakuzungumziki, yaani hakuna kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuishauri wizara kwa sababu kila kitu mtu anachotaka kukifanya lazima awe na utaalamu, sasa bila ya utaalamu jambo hilo unalokusudia kulifanya, basi huwezi kuliendeleza vyema. Kwa hivyo, ili uweze kuliendeleza vyema ni lazima uwe na utaalamu wa kuendesha jambo hilo.

Sisi tunakusudia kuimarisha uvuvi katika nchi yetu. Kwa maana hiyo, ninashauri wizara ikafikiria kuanzisha Chuo cha Uvuvi, ili kiweze kuwasaidia wavuvi wetu kuwa na utaalamu wa uvuvi wa kisasa na kuondokana na ule wa kienyeji.

Vile vile hivi sasa kumejichomoza suala.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuomba umalizie.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Ahsante. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na naunga mkono hoja *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Denge Makame pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija mtatusamehe, ili tuweze kumwita Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira na baadaye tumwite Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa ajili ya kufanya majumuisho *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia naomba kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili tena ni mwanamke *(Makofi)*.

Aidha napenda kumshukuru Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi), vile vile napenda kumshukuru Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira) kwa michango, fikra, maelekezo pamoja na maoni mazuri waliyotupatia katika kuchangia mswada huu wa sheria *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mkono wa rambirambi kwa Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira) kwa kufiwa na mtoto wake na Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, amin.

Vile vile naomba kuwashukuru pamoja na kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naanza kujibu hoja za baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa jumla kama ifuatavyo:-

Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira) kuhusu hoja ya marufuku ya kukamata samaki wachanga na tunahamasisha ufugaji wa samaki. Upigwaji marufuku ulioelezwa katika sheria ya kukamata samaki wachanga ni pamoja na kumuua na wala sheria hii haitamzuia mwananchi kukamata samaki wachanga kwa ajili ya ufugaji *(Makofi)*.

Mhe. Abass Juma Muhunzi kuhusu hoja ya takwimu za uchangiaji wa uvuvi ni ndogo sana. Uvuvi huchangia asilimia ndogo ya pato la taifa kwa sababu usafirishaji wa mazao ya baharini kwenda nchi za nje ni ndogo kulinganisha na matumizi ya ndani ya nchi. Miongoni mwa mazao ya baharini kwa wingi ni pweza, ngisi, kamba kochi, kaa na chaza.

Hoja sheria haikuainisha kwa kuwatambua Makatibu wa Kamati Tendaji. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii mpya imewataja Makatibu wa Kamati Tendaji pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Shehia kwenye tafsiri na afisa mwenye mamlaka. Aidha utambulisho kamili wa watendaji hao imewekwa kwenye kanuni za kanda husika.

Mhe. Haji Mkema Haji sheria haijaonesha ushirikiano na taasisi nyengine. Mhe. Mwenyekiti, hatua za kuingia kifungu kitakachotoa nafasi kwa idadi hii kuingia katika mashirikiano na taasisi nyengine tutakichukulia hatua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu hayo mafupi kwa sababu na mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Bububu ambalo ninalo wavuvi katika shehia zangu zote nne, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo langu la Bububu naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Kwa hivyo, naomba nimuachie Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, kwa ajili ya kuja kumalizia *(Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa uwasilishaji wako wa kitaalamu. Sasa tunamkaribisha Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kufanya majumuisho ya michango mizuri sana ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Kabla sijaendelea naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba michango yao ni mizuri na yote ambayo wametuelekeza pamoja na kutushauri, tumeipokea na tutajitahidi kuifanyia kazi.

Isipokuwa mambo mengine itabidi tushirikiane na vyombo kama vile Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kadhalika. Lakini kwa ufupi tutajitahidi kadri tunavyoweza kuyashughulikia masuala yote ambayo yamechangiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imechangiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu 20 naomba niwataje kabla sijaanza kujibu hoja mbali mbali kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin — Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi,
2. Mhe. Assaa Othman Hamad — Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira,
3. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi,
4. Mhe. Omar Ali Shehe,
5. Mhe. Ali Abdalla Ali,

6. Mhe. Rashid Seif Suleiman,
7. Mhe. Haji Mkema Haji,
8. Mhe. Abass Juma Muhunzi,
9. Mhe. Ali Moh'd Bakar,
10. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk,
11. Mhe. Juma Duni Haji,
12. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui,
13. Mhe. Najma Halfan Juma,
14. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi,
15. Mhe. Abubakar Khamis Bakary,
16. Mhe. Zakiya Omar Juma,
17. Mhe. Ame Ussi Juma,
18. Mhe. Zahra Ali Hamad,
19. Mhe. Mohammed Ali Salim na
20. Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin.

Kwa kweli wote tunawapongeza sana kwa michango yao mizuri sana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla michango ya Waheshimiwa Wajumbe ukiiweka kwa asilimia mia basi naweza kusema kwamba zaidi ya asilimia 90 ilikuwa ni maelekeo pamoja na ushauri, kwa ajili ya kuifanya hii sheria yetu iwe nzuri zaidi.

Lakini pamoja na hayo nitajaribu kujibu zile hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza tukianza na Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) kwa mujibu ya waraka wake huu ambao tumejaribu kuupitia kwa kina kabisa na yote kama nilivyosema ametushauri.

Kwa mfano, suala la ujenzi wa jeti ambalo limezungumzwa sana na hili kwa kweli ni moja katika jambo ambalo tunatuumisha vichwa. Lakini tutajitahidi kushirikiana na wenzetu wahusika kama vile Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi kupitia Kitengo cha *ZIPA* kuweza kuona mambo haya yanashughulikiwa ipasavyo visitolewe tu vibali kila mtu anayetaka kujenga geti basi aruhusiwe. Kwa hivyo, hili tutakuwa waangalifu zaidi katika suala haya.

Mhe. Mwenyekiti, amesema kwamba huu uvuvi wa haramu ameuzingizia sana na wajumbe mbali mbali pia walilizungumzia suala hili. Kwa kweli haya tutayashughulikia ipasavyo. Pia amesema kuwajua wavuvi wote wa kienyeji na wageni hili ni moja katika kazi yetu sisi na vile vile ni kazi ambayo ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa sababu wao ndio wanaohusika kusajili hivi vyombo vyote vya baharini, lakini tutashirikiana na wizara hiyo kuwajua wavuvi wangapi pamoja na vyombo vyao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine limesemwa hapa kwamba kuna vifungu vidogo vinavyoainisha tulivyovigawa kwa wajumbe kwa mfano kama mabadiliko haya yaliyokuwa yamefanywa amesema kwamba lazima tuzisimamie vyema sheria zetu hizi tunazozitunga ili zilete maana halisi. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndio dhamira yetu kubwa sana ndio tukaleta mswada huu wa sheria hii mpya ili tuweze kwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe kwanza nashukuru kunipatia nafasi hii ya kufanya majumuisho kutokana na michango, nawapongeza wajumbe wote. Pia naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa mchango wake mzuri kuhusu pongezi zilizotolewa kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wizara na wafanyakazi wenzangu hasa waliohusika na mswada huu Idara ya Uvuvi tumezipokea nakushukuruni sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tunaomba kusema kwamba hatua ya mwanzo kwa mfano wizara kuwa na Chuo cha Uvuvi hivi sasa hiki Chuo chetu cha Kizimbani ambapo tumepitisha sheria yake hapa hapa kwa kweli katika *syllabus* yake uvuvi umo. Kwa hivyo, hili suala tutalitafakari kuwa ipo haja kuwa na chuo peke yake cha uvuvi tu au kiendelee kuboreshwa hicho hicho basi tutatizama vipi tuimarishe somo la uvuvi katika Chuo chetu cha Kizimbani au tujenge chuo maalum. Kwa hivyo, hilo tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mfuko wa fedha katika sekta ya uvuvi ni matumaini yangu kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi imeweka mikakati mizuri ya kutatua matatizo ya kukidhi haja ikiwa pamoja na kutoa mkopo kwa walengwa. Mfano tafauti ikiwemo Mradi wa *MACEMP* ambao hutoa misaada bure kwa walengwa. Wizara imo katika hatua ya kuandaa utaratibu wa kuwapatia wakulima na wavuvi mikopo ya bei nafuu kupitia Benki ya Vijijini na pia kupitia kwa wahisani wa maendeleo ya jamii. Tunategemea kupata mradi mpya ambao utawasaidia wakulima na wavuvi katika maeneo ya miundombinu ya masoko, fedha na kuongeza thamani ya mazao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba hoja ya kuwa Tanzania Bara ina sheria mbili zinazosimamia sekta ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kuwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna sheria mbili zinazosimamia uvuvi, sheria ya kwanza Nam. 22 ya mwaka 2003 ya Idara kwa upande wa Tanzania Bara na ya pili sheria Nam. 8 ya mwaka 1988 ya idara tuliyoitarajia kuifuta kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Bahari Kuu ya mwaka 1998 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikutekelezeka kutokana na mapungufu waliyokuwa nayo pamoja na kwamba baadhi ya mapungufu hayo

yamefanyiwa marekebisho na wataalamu kutoka pande mbili za muungano. Bado tunaendelea na mchakato wa maandalizi na baadae sheria hiyo itawasilishwa kwenye Baraza lako ili ipate ridhaa na utekelezaji wake utakuwa kwa Zanzibar na Tanzania Bara na sio Tanzania Bara peke yake kama inavyofahamika. Suala hili amelisema sana Mhe. Abubakar tunamshukuru kwa hivyo na sisi tumeliona hilo tumo katika mchakato na mara tu mambo yote yakimalizika tunaahidi kwamba tutaleta hapa katika Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ni kwamba sheria haioneshi ni vipi waziri atadhibiti uvuvi wa kienyeji. Jibu ni kwamba kifungu cha Nam. 7 kinampa uwezo Mhe. Waziri anayesimamia uvuvi kutangaza katika gazeti rasmi masharti ambayo yenye umuhimu ikiwa ni pamoja na shughuli za uvuvi. Hivyo maana halisi ya neno udhibiti ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe kuwa ndani ya maeneo ambayo wavuvi wanaruhusika kuvua kwa kufuata taratibu za kanuni na vigezo vitakavyokubalika katika utoaji wa leseni kama ilivyoelezwa katika kifungu 14 (3) cha sheria hii.

Aidha, Mhe. Waziri anayesimamia uvuvi atakuwa na uwezo kamili wa kupokea malalamiko yote yaliyomo ndani ya sheria hii pindipo muhusika atatendewa kinyume cha taratibu zilizowekwa ndani ya sheria hii atakuwa na uwezo kamili wa kupeleka mashtaka yake katika vyombo vya sheria.

Mhe. Mwenyekit, hoja nyengine ilikuwa kwamba msimamizi na utaratibu uliowekwa katika kifungu cha 15 (6) napenda kusema kwamba taratibu zote zilizoelezwa katika kifungu hicho zitaweka wazi kupitia kanuni itakayotungwa na Mhe. Waziri.

Pia kulikuwa na hoja ya kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu matumizi ya bahari kwa ajili ya uvuvi baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa maoni ya kuwa hakuna mpaka maalum wenye maeneo ya EEZ. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba sheria ambayo hivi nimewasilisha kwenu ni sheria ya Zanzibar ambayo imejielezea wazi katika kifungu cha 2.

Mhe. Mwenyekiti, leseni za uvuvi katika ukanda wa uchumi EEZ haitokuwa na tatizo lolote kwa upande wa pili wa Muungano mpaka Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakapoanza rasmi utekelezaji wake. Hivi sasa tunayo mapendekezo tu ya sheria ya uvuvi wa bahari kuu ambayo itawasilishwa baadae kwenye Baraza lako tukufu kwa ajili ya kupata ridhaa ya wajumbe. Aidha, itakaporidhiwa na Mhe. Waziri anayesimamia uvuvi ataweka wazi utaratibu wa utoaji leseni katika bahari kuu kwa taasisi itakayokabidhiwa dhamana hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpa pole Mhe. Waziri Kivuli Mhe. Asaa kwa kufiwa na mtoto wake Mwenyezi Mungu amlaze pahala pema peponi, amin.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi naomba niwajibu kwa pamoja kutokana na kwamba hoja zao zinalingana. Hoja yao ilikuwa ni kupiga marufuku uingizaji wa vifaa vya uvuvi haramu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba vifaa vingi vya uvuvi haramu bunduki, mshale, uzio na kadhalika hutengenezwa kienyeji hapa hapa nchini. Upigaji wowote wa marufuku wa uingizaji wa nondo, mbao, malighafi utaasiri sekta nyenginezo. Mhe. Mwenyekiti, upigaji marufuku wa uingizaji wa chupa za gesi nchini utaasiri sekta ya utalii kwa wale ambao wanaopiga mbizi (*divers*).

Mhe. Mwenyekiti, nyavu za macho madogo hutumika kwa kuvulia dagaa, vibua na samaki wa jamii kama hizo katika maeneo yaliyoko nje ya maeneo ya hifadhi. Hivyo, wizara haikupiga marufuku nyavu za macho madogo kwa sababu ni halali kutumika katika maeneo yaliyokubalika. Hii kwa kweli nina wajibu waheshimiwa wengi walitaka kujua ufafanuzi juu ya suala la uvuvi kama huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia ni marufuku kukamata samaki wachanga na tunahamasisha ufugaji wa samaki. Ni kwamba marufuku yaliyowekwa katika sheria ya kukamata samaki wachanga ni pamoja na kumuua, sheria hii haitamzuia mwananchi kukamata samaki wachanga kwa ajili ya ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif Suleiman amesema kwamba kutokana na takwimu za samaki za Benki ya Dunia zilizoweza kupatikana uvuvi unachangia asilimia 1 tu ya pato la taifa na kiwango kidogo cha protini ya samaki kwa watu. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar sekta ya uvuvi inachangia kwa wastani wa asilimia 5.2 ya pato la taifa. Aidha, kutungwa kwa sheria hii mpya ni miongoni mwa hatua muhimu zitazohitajika katika kuhakikisha kiwango cha protini kwa wananchi kutokana na mazao ya baharini yanaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abass Juma Muhunzi amesema kwamba takwimu za uchangiaji za uvuvi ni ndogo sana. Napenda kufahamisha kwamba uvuvi kuchangia asilimia ndogo ya pato la taifa kwa sababu usafirishaji wa mazao ya baharini kwenda nchi za nje ni ndogo ukilinganishwa na matumizi ya ndani ya nchi. Miongoni mwa mazao ya baharini yanayosafirishwa kwa wingi ni pweza, ngisi, kamba, kaa na chaza.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa soko la samaki ni kwamba kweli katika Mradi wa MACEMP kuna mpango wa ujenzi wa soko la kisasa la samaki. Kwanza kabisa napenda kumuhakikishia kwamba hakuna fedha zozote za Mradi wa MACEMP Zanzibar ambazo zimerejeshwa bila ya kutumika. Fedha hizo za ujenzi bado zipo na mpango wa ujenzi wa soko hilo bado upo. Kinachozingatiwa hivi sasa ni upatikanaji wa eneo litakalokubalika kitaalamu, hivi sasa utaratibu umeshakamilika wa kumpata mchoraji kwa ajili ya ujenzi huo huko Tumbe Kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haikuwahi kuingia makubaliano na Serikali ya Japan juu ya ujenzi wa soko la uvuvi huko nyuma. Linaloendelea hivi sasa tuko katika hatua za awali za kufanya makubaliano na Serikali ya Japan katika ujenzi wa soko katika Kisiwa cha Unguja.

Mhe. Haji Mkema Haji yeye amesema kwamba sheria haijaonesha ushirikiano na taasisi nyengine. Napenda kujibu kwamba hatua za kuingiza vifungu kitakachotoa nafasi katika idara hii kuingia katika mashirikiano na taasisi nyengine tutachukua hatua.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kujibu kwamba mapendekezo ya sheria niliyowasilisha itachukua tahadhari hiyo ingawa bado kuna mambo ya msingi yanahitaji kufanyiwa kazi kwa ajili ya kufikia lengo hilo. Mambo yenyewe ni kama yafuatayo:

1. Huduma za baharini ziimarishwe.
2. Huduma za kuhifadhi, kusarifu na kusindika ziimarishwe.
3. Huduma ya usafiri wa anga na baharini ziwe zina uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abass yeye alisema kwamba sheria haikuanisha au kutambua Makatibu wa Kamati Tendaji. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii mpya imewataja Makatibu wa Kamati Tendaji na Wajumbe wa Kamati za Shehia kwenye tafsiri ya afisa mwenye mamlaka. Aidha, utambulisho kamili wa watendaji hao umewekwa kwenye kanuni husika.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ulikuwa ni uvuvi wa *semi industrial* hapa Zanzibar haipo. Mhe. Mwenyekiti, napenda kusema kwamba sekta ndogo ya uvuvi huo hapa Zanzibar ipo na kampuni zinakata leseni za uvuvi wa aina hii. Hata hivyo, meli nyingi za uvuvi wa aina hii hukata leseni Tanzania Bara kwa sababu kutaka kuvua aina ya kamba wadogo wadogo ambao hupatikana kwa wingi zaidi katika maeneo ya Lindi na Mtwara Kusini mwa Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumaliza kwa kusema kwamba ikiwa kuna hoja ambazo sikuzijibu katika hatua hii basi naomba kusema kwamba tumezichukua na tutazifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis alikuwa anataka kujua habari ya *cross bridge* katika samaki. Ni kwamba suala hili linafanyika katika nchi zilizoendelea kwa daraja ya aina ya samaki watokanao na jamii moja. Bado hakuna utaratibu wa kufanya *cross bridge* kwa jamii za aina tofauti kutokana na sababu tofauti za kitaalamu ambazo tafiti zake bado zinaendelea katika nchi zinazoendelea. Pia kuna mambo ya kuzingatia ya kitaalamu mfano chembechembe za *gins* na jamii ya samaki itakayopatikana kutokana na *cross bridge* haitokuwa na athari kwa jamii nyengine za samaki zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abubakar alitaka kujua kwamba kifungu cha kuundwa Idara ya Uvuvi na kazi za Mkurugenzi. Napenda kujibu kwamba kuhusu kifungu cha kuundwa idara hiyo hii imewekwa kutokana na uzito na umuhimu wa suala la uvuvi kwa lengo la kujulikana kwa idara hiyo ndio itakayokuwa msimamizi mkuu wa mambo ya uvuvi. Utaratibu huu si mgeni bado unafanyika kwa taasisi mbali mbali zinazotoa huduma kwa jamii. Kwa mfano, Sheria ya Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nimejaribu hoja mbali mbali kwa zile ambazo sikuzijibu napenda kuwahakikishia wajumbe kwamba tumezichukua kwa uwazi kabisa na tutazichukulia hatua mara tu baada ya kumaliza kikao hiki moja baada ya moja. Pia nawashukuru Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kuchangia vizuri tangu katika semina hadi hii leo michango yao yote ilikuwa mizuri na yote ilikuwa ya kujenga. Kwa hivyo, mapendekezo na ushauri waliotupa tumepokea na tunawahakikishia kwamba tutayafanyia kazi ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitia kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Kifungu cha 1 Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
Kifungu cha 2 Matumizi

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba katika kifungu cha pili kinasema sheria hii itatumika Zanzibar na nimesema kwa mujibu wa *definition* tulizonazo za Zanzibar ni ile sehemu zote za visiwa pamoja na yale maji ya ndani na ile *twelve nautical miles* hakuna ule ukanda wa uchumi. Kwa hivyo, ili kuweza kuipata hii na sheria yetu imeshaitambua kwa hivyo naomba tuongeze kuwa sheria hii itatumika Zanzibar pamoja na maji yake yote ya ndani na ukanda wa uchumi ambao Zanzibar inaumiliki.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, tumekubaliana na pendekezo la Mhe. Abubakar.

Kifungu cha 2 Matumizi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA PILI
UTAWALA

Kifungu cha 4 Idara ya Uvuvi.
Kifungu cha 5 Kazi za idara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6 Uteuzi na kazi za Mkurugenzi.

SEHEMU YA TATU
UENDELEZAJI NA UDHIBITI WA SEKTA YA UVUVI

Kifungu cha 7 Waziri anaweza kudhibiti kazi za uvuvi.
Kifungu cha 8 Mipango ya usimamizi na maendeleo.
Kifungu cha 9 Hatua za usimamizi.
Kifungu cha 10 Waziri anaweza kutangaza maeneo ya udhibiti.
Kifungu cha 11 Uhifadhi wa kazi za uvuvi.
Kifungu cha 12 Uanzishwaji wa madiko.
Kifungu cha 13 Ridhaa ya maandishi kwa mgeni.

SEHEMU YA NNE
UTOAJI WA LESENI KWA SHUGHULI ZA UVUVI

Kifungu cha 14	Utoaji wa leseni kwa vyombo vya uvuvi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 15	Masharti ya jumla ya utoaji wa leseni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 16	Leseni nyengine kwa ujumla.
Kifungu cha 17	Juya, uzio, bunduki yam shale, vifaa vya umeme na vyombo vya kuzamia.
Kifungu cha 18	Idhini ya kufanya utafiti wa kisayansi.

SEHEMU YA TANO
HATUA ZA UHIFADHI

Kifungu cha 19	Kitengo cha uhifadhi wa bahari pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20	Njia za uvuvi zilizokatazwa.
Kifungu cha 21	Matumizi ya mitego iliyokatazwa.
Kifungu cha 22	Kuvua samaki wachanga.
Kifungu cha 23	Uwezo wa afisa aliyeidhinishwa.
Kifungu cha 24	Samaki wanaokamatwa wanaweza kuuzwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25	Mtu aliyekamatwa apelekwe Mahakamani.
Kifungu cha 26	Kuachiliwa vyombo vya uvuvi kwa dhamana.
Kifungu cha 27	Kufilisi na kuagizwa mitego iliyokatazwa.

SEHEMU YA SITA
MAKOSA NA ADHABU

Kifungu cha 28	Adhabu ya kuvua kwa kutumia baruti na vitu vya sumu.
Kifungu cha 29	Adhabu kwa kumzuia afisa aliyeidhinishwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 30	Adhabu kwa makosa yanayohusiana na leseni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 31	Adhabu kwa makosa mengineyo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 32	Malipo ya faini kwa mgeni pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA SABA
MASHARTI MENGINEYO

Kifungu cha 33	Msamaha.
Kifungu cha 34	Kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 35	Kutatua makosa ya nje ya Mahakama pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 36	Kufuta sheria Nam. 8 ya mwaka 1988 na uhifadhi.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kukubali bila ya mabadiliko yoyote sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nawahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nawahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa mashirikiano mlionipa asubuhi hii ya leo na naomba mashirikiano haya yazidi kuendelea. Pia kuna taarifa kuhusu msiba alioupata Mhe. Asaa amenileta taarifa hapa kwamba ajali hiyo ambayo imemkuta ni mtoto wa kaka yake imetokea katika Barabara ya Mkapa pale Magogoni ambapo wanawake wawili wamepatwa na ajali hiyo mmoja ni mtoto wa kaka yake kwa jina anaitwa Mchanga Hamad Othman na yeye ni Mhe. Asaa Othman Hamad kwa hiyo kwa niaba yetu waheshimiwa tunampa pole kwa msiba huo uliomkuta inshaallah Mwenyezi Mungu atamjalia yeye pamoja na wengine subra. Naomba kuahirisha kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

RIPOTI ZA KAMATI

Kamati ya Fedha na Uchumi

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, ufuatao ni Muhtasari wa Ripoti ya Kazi za Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema zake za kuendelea kuwa hai tukiwa wazima na afya njema, na leo kutukutanisha tukiwa na furaha na ari mpya ya kuwatumikia wananchi wetu.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi yanayohusiana na Ripoti ya Kazi za Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2010, ukiwa ni mwaka wa mwisho wa Baraza lako la Saba kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010.

Naomba nikushukuru tena kwa kuniteua kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamati yako ya Fedha na Uchumi kwa mara ya pili. Kwa bahati kwa kipindi hiki, wajumbe wezangu uliowateua kwa kauli moja wakanichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati.

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa uamuzi wao huo wa busara wa kuniamini kuwa kiongozi wao. Aidha, uthibitisho wao ilikuwa ni

mashirikiano ya dhati kabisa ambayo wamenipa kwa kipindi chote tulichokuwa tukifanya kazi ulizotuagiza.

Michango na ushiriki wao katika kazi ilikuwa ni changamoto tosha kwangu, lakini pia ni faraja katika uongozi wangu huo na ushauri, busara na mawazo yao yalikuwa kichocheo cha ufanisi wa kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kukamilisha shukurani zangu bila ya kuwapongeza Makatibu wetu wa Kamati, walifanya kazi nzuri za kuratibu na kutoa ushauri wao kwa kutumia uzoefu na taaluma zao walisaidia sana mafanikio ya kamati yetu.
Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ali Abdalla Ali	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Assaa Othman Hamad	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Abeid Faraji	Mjumbe
5.	Mhe. Said Khelef Ali	Mjumbe
6.	Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	Mjumbe
7.	Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	Mjumbe
8.	Mhe. Juma Duni Haji	Mjumbe
9.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
10.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	Mjumbe
11.	Ndg. Amour Moh'd Amour	Katibu na
12.	Ndg. Maryam Hussein Rajab	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii adhimu kutoa shukrani zangu za dhati na za pekee kwa Mhe. Juma Duni Haji kwa kuteuliwa kwake, pia kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kumteua kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi. Kwa kipindi kifupi alichokuwepo kwenye kamati, mchango wake, busara na hekima zake zimeonekana. Ijapokuwa alipata muda mfupi lakini alijifunza na kuzoea kama kwamba amekuwepo kwa muda mrefu.

Kwa kutumia nafasi hii, niwape pole familia ya marehemu Mhe. Soud Yussuf Mgeni aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Wawi ambaye ulimteua kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Soud hakuwahi kufanya kazi katika kamati hii na mauti yakamchukua. Mwenyezi Mungu ailaze pema roho ya marehemu. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa wizara zinazosimamiwa na kamati hii, Makatibu

wao Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji wao kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyaonesha kwa kamati. Japo kulikuwa na matatizo madogo madogo, lakini michango na uwezo wao pamoja na mashirikiano yao yamepelekea ukamilifu wa kazi hii tunayoiwasilisha leo.

1.0 Kazi za Kamati

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeweza kufanya kazi zake za kawaida Kisiwani Pemba wiki mbili, Kisiwani Unguja kwa wiki tatu na Tanzania Bara kwa takriban wiki moja. Kwa kweli, Mhe. Mwenyekiti, muda tuliopewa wa ufuatiliaji wa mawizara umekuwa ni mdogo, hivyo hautoshi kabisa kufuatilia na kuzimaliza taasisi na idara mbali mbali zilizomo katika wizara husika.

Kamati ya Fedha imeshindwa kufanya kazi katika baadhi ya Taasisi na Idara za Serikali wizara husika kwa kukosa muda. Kawaida kamati hupewa wiki mbili tu kwa kila awamu. Muda wa wiki mbili kwa kila awamu ni mdogo sana, hivyo, kamati inaomba pia suala hili litizamwe upya ili kuweka mazingira mazuri ya Kamati hizi za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na kuhakikisha zinafuatilia kikamilifu utendaji wa wizara.

Kamati ya Fedha na Uchumi imepangiwa wizara tatu ambazo ni Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Wizara hizi tatu ni wizara nyeti na zenye mlolongo mrefu sana wa idara na taasisi.

3.0 Utaratibu wa Kazi

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeweza kupokea taarifa za utekelezaji za wizara na kuona hali halisi ya utekelezaji wa shughuli za kila siku. Kamati pia ilitoa maoni mbali mbali kuhusu kazi zinazofanywa na Taasisi za Serikali baada ya kuona upungufu. Mafanikio na kufikiwa na kutokufikiwa kwa malengo yaliyopo kwa baadhi ya taasisi za mawizara.

4.0 Maoni kwa Ujumla

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla tatizo linalozikabili wizara zetu ni suala zima la Bajeti, ambalo limekuwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa kila siku wa kazi za mawizara. Bajeti haitoshelezi kabisa mahitaji ya wizara kwani Bajeti imekuwa ikitolewa kutokana na ukomo wa bajeti (*Ceiling*), hivyo ni vigumu kuendana na mahitaji halisi ya vipaumbele vya wizara husika.

Halikadhalika, wizara zimekuwa zikilalamika sana kuhusu kuchelewa kwa matumizi mengineyo ya fedha (*other charges*). Jambo ambalo ama huchelewesha kufikiwa kwa malengo au kutotekelezeka kabisa baadhi ya kazi zilizopangwa.

5.0 Yaliyojitokeza

5.1 Wizara ya Fedha na Uchumi

Mhe. Mwenyekiti, kamati hii imeweza kufanya ziara zake za ufuatiliaji wa kazi kama kawaida katika taasisi za Wizara ya Fedha na Uchumi kwa upande wa Unguja, Pemba na Tanzania Bara na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa idara hizo. Kamati ilipokea malalamiko, ushauri na changamoto Mbale mbali zinazokabili taasisi hizo.

Kwa kujali sana muda, nadhani haitakuwa busara kuweza kuzitaja idara moja moja, kwani tayari maelezo yetu yameshaandikwa kwenye vitabu vya ripoti ambapo naamini kabisa Waheshimiwa Wajumbe wamepata nafasi nzuri ya kuvisoma.

Hata hivyo, naomba uniruhusu nizitaje baadhi tu, kwa msisitizo kutokana na ukubwa wa changamoto zilizopo.

- **Tume ya Pamoja ya Fedha**

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha imekuwa katika hali ngumu tangu kuanzishwa kwake na imekosa mwelekeo kwa kuwa kazi nyingi ilizopangiwa zimekwisha malizika bila ya kutolewa maamuzi yoyote. Hivyo kuwapa wakati mgumu watendaji wa tume hiyo. Mhe. Mwenyekiti, mfano ni suala zima la kuanzishwa kwa akaunti ya pamoja ya fedha kwa serikalli mbili, yaani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo la kufungua akaunti ya pamoja limekuwa halipatiwi ufumbuzi kwa muda mrefu bila ya kutolewa hoja yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, laiti ingekuwa tunaendelea tena na ziara, basi kipindi kijacho kamati isingekuwa radhi kwenda kupata taarifa katika tume hii. Kwani tungeshindwa kuficha nyuso zetu kwa vile watendaji wamechoka kusubiri matokeo ya kazi tuliyowatuma. Kwa muda mrefu sasa kamati imekuwa ikipata taarifa hizo kwa hizo bila ya kutolewa ufafanuzi wowote kwa serikali zetu mbili. Tume pia, imeshatoa ripoti kwa serikali zote mbili tangu Agosti, 2006, lakini bado hakuna majibu yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, watendaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha wanajitahidi sana katika kuhakikisha mambo yanakaa sawa, ila cha kustajaabisha zaidi ni kuchelewa na kutotolewa maamuzi yoyote ya serikali mbili ya mapendekezo mbali mbali kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Mhe. Mwenyekiti, hii ni sawa na kusema Tume ya Pamoja ya Fedha imeundwa tu kama pambo la kuridhia katiba.

Ili lengo la kuwepo kwa Tume hii ya Pamoja ya Fedha litimie, basi ni vyema Mhe. Waziri wa Nchi AR (MBLM) Anaeshughulikia Fedha na Uchumi akakutana pamoja na Waziri mwenzake wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Kamati zetu za Fedha na Uchumi za Bunge na Baraza la Wawakilishi, ipatikane nafasi ya kina kuzungumzia matatizo yanayokwamisha utekelezaji wa majukumu iliyopewa.

- **Shirika la Bima**

Kamati ya Fedha na Uchumi iliweza kupata taarifa mbali mbali juu ya Shirika la Bima, kuanzia Makao Makuu hadi katika baadhi ya matawi yake yaliyopo mikoani. Kwa kuona umuhimu wa kuwa na Bima ya Maisha, Mhe. Mwenyekiti, kamati hii inaishauri serikali iharakishe katika kuhakikisha Zanzibar inatoa Bima ya Maisha. Kwa misingi ulivyo, sheria ya bima inafuta shirika kuwa na bima za aina mbili, yaani Bima ya Maisha na zile bima za kawaida, ama kuamua kuwa na bima ya maisha au bima za kawaida.

Kwa kuwa Bima ya Maisha inaonekana ni yenye tija yamkini ni bora kwa upande wa Zanzibar kuwe na shirika litakaloshughulikia Bima ya Maisha. Kwa hilo, tunaweza Mhe. Mwenyekiti, kama tutasimama imara kutetea suala hili. Pia ningependa kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, kuwa Shirika la Bima la Zanzibar lina nafasi nzuri ya kiutendaji hususan kwa upande wa Tanzania Bara. Hii inatokana na imani ya walio wengi juu ya Zanzibar.

- **Chuo cha Uongozi wa Fedha - Chwaka**

Mhe. Mwenyekiti, kila kukicha viongozi tumekuwa tukisisitiza umuhimu kuhusu elimu bora kwa watoto wetu, hususan katika kuweka mazingira bora ya kusomea. Hali ya kutokuwa na maji ya uhakika kwa wanafunzi wa Chuo cha Chwaka ni changamoto kubwa inayowakabili walimu pamoja na wanafunzi katika kutafuta mbinu za kutatua tatizo hilo. Hivyo ni vyema kwa serikali kuona juhudi zilizochukuliwa na Uongozi wa Chuo hicho na yenyewe kutia mkono katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

5.2 **Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji**

- **Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*)**

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) Zanzibar, ndiyo mamlaka iliyochaguliwa hapa Zanzibar kuwa ni kituo kimoja tu, cha maamuzi yote yahayohusu uwekezaji, yaani (*One Stop Investment Facilitation Center*). Dhana hii ya *One Stop Center* huenda isifanikiwe na kupoteza maana halisi kwa kuwa imekuwa ikikwamishwa na idara au taasisi husika ambazo zinashiriki suala zima la kufanikisha usahihi wa Uwekezaji ama kutowashirikisha wajumbe wenye maamuzi au kutokana na sababu mbali mbali zisizoeleweka, kutoa vipingamizi vinavyosababisha kucheleweshe kwa utekelezaji wa maamuzi, jambo linaloleta sifa mbaya kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza.

Wakati mwengine yanaweza kutolewa maamuzi, lakini baadae idara nyengine ikalalamika ruhusa ile ya uwekezaji. Kwa mfano, matumizi ya fukwe na ujenzi wa jeti au uharibifu wa mazingira wakati wa kuwekeza.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza kushindwa kuamini kwamba, pamoja na taratibu zetu na sheria zilizopo, lakini idara husika tu kama vile uhamiaji inaweza ama kufuta au kutokutoa kibali cha kazi kwa wawekezaji bila ya sababu ya msingi, ingawa *ZIPA* na Kamisheni ya Kazi zimeeleza vya kutosha juu ya umuhimu wa wafanyakazi hao kuwepo Zanzibar kama wataalamu.

Ni vyema tuwe tuna maamuzi ya pamoja yanayoongozwa na taratibu zetu, vyenginevyo tunaweza kuharibu sifa yetu nzuri iliyopo kwa kuwa na usumbufu usio na maana.

Kamati yetu inawaomba sana wenzetu wahusika wajipange vizuri ili tuwavutie wawekezaji wetu waone kwamba Zanzibar ni pahala pazuri pa kuwekeza.

- **Shirika la Utalii**

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Utalii linahitaji sana kuendelezwa kibiashara na eneo muhimu la kuliwezesha kujikongoja ni la *Kilimani Bar*, ambalo lilikuwa lijengwe Afisi ya Bodi ya Mapato Zanzibar. Kwa bahati, kutokana na sababu za uwezo wa ardhi iliyopo pale na jengo lililokuwa likitakiwa kujengwa ikaoneka ni vigumu kuweza kuhimili na hivyo *ZRB* wametafuta eneo jengine.

Kama katika zoezi hilo eneo lilishahamishiwa taasisi nyengine isiyokuwa Shirika la Utalii ni vyema na ni busara kubwa eneo hilo likarejeshwa kwenye

Mamlaka ya Shirika lenyewe na shirika litafute aina ya uwekezaji ambao utakuwa na tija kwa mfano: Ujenzi wa kumbi za burudani na mikutano.

5.3 **Wizara ya Kilito, Mifugo na Mazingira**

- **Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini**

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kuwa Sekta ya Uvuvi ni kichochoe kikubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi kama ikitumiwa ipasavyo. Kwa hiyo, ni vyema kutunza rasilimali zilizopo baharini kwa kuhakikisha kuwa hakuna madhara yoyote yatakayosababisha kupotea kwa rasilimali hizo. Idara ya Uvuvi imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika sana na uvuvi. Idara kwa sasa imeanzisha kamati mbalimbali za wavuvi ambazo kwa kweli zimesaidia sana kutoa elimu kwa wavuvi na kulinda rasilimali hizo, lakini pia kuzitunza na kuzihifadhi.

Idara ya Uvuvi kupitia kitengo chake cha uhifadhi wa rasilimali za bahari (*MARINE CONSERVATION UNIT*), pamoja na vitengo vya maeneo ya hifadhi za baharini *MENAI*, *MINCA*, na *PECCA* zimekuwa zikitoa elimu kwa wananchi mbali mbali juu ya uhifadhi wa bahari kupitia semina, mikutano na makongamano ambayo ndiyo tegemeo kubwa kwa wavuvi na vivutio kwa watalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile katika mkutano wetu huu unaomalizika ulipitisha Mswada wa Kufuta Sheria ya Uvuvi na Kuweka Masharti Bora Yanayohusiana na Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi ndani ya Zanziba, ni dhahiri kwamba sekta hii sasa itaimarika zaidi. Ushauri kwa wavuvi na wote wanaotumia bahari kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na mazao ya baharini wawe mstari wa mbele katika kusimamia na kufuata maelekezo ya sheria hiyo mara itakapoanza kutumika.

- **Karakana ya Matrekta - Mbweni**

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sasa, Karakana ya Matrekta - Mbweni imekuwa na kilio kisichokwisha. Hali ya kutotambulika kwa karakana hii kama ni idara au taasisi, inawatia unyonge watendaji wa karakana hiyo. Yapo madhara mengi yanayoipata karakana, mfano ni kutopewa fedha zinazokidhi mahitaji ya shughuli zao kwa kuwa haina hadhi ya idara au taasisi, hivyo kusababisha kupangiwa bajeti isiyotosheleza. Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo na ndio maana kule kwa wenzetu Tanzania Bara wanahamasisha Kilimo Kwanza. Tuisaidie hii karakana kwanza kwa kutambulika kwake ili iwe na uwezo wa kufanya shughuli zake kikamilifu.

- **Kiwanda cha Sukari Mahonda**

Mhe. Mwenyekiti, uwekezaji umepewa kipaumbele sana katika kuleta maendeleo. Kwa sasa, nia ya serikalli ni kuitangaza Zanzibar kuwa kivutio kikubwa cha uwekezaji. Hivyo basi, serikali haina budi kuangalia upya kodi ya ardhi inayotozwa kwa wawekezaji. Kwa mfano, gharama kubwa anazotozwa mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, gharama ni kubwa sana ukilinganisha na hali halisi ilivyo ulimwenguni, kwani gharama za kodi ya ardhi (mashamba) ni ndogo sana kuliko kodi zozote zile.

Jengine ni suala la baadhi ya wakulima kutumia baadhi ya maeneo ya sehemu ya shamba kwa shughuli za kilimo, ambapo kamati ilipata nafasi ya kujionea hali halisi na kukuta kweli kuwa baadhi ya maeneo yamelimwa mihogo na mazao mengine. Aidha, baadhi ya wananchi wamekuwa wakifuga mifugo yao katika shamba la miwa hasa katika miwa michanga. Hivyo husababisha hasara kubwa kwa mwekezaji.
Mhe. Mwenyekiti, tunaomba Serikali za Mkoa na Wilaya zisaidie kwa dhati ulinzi na kutoa elimu kwa wananchi wetu ili tusiwavunje moyo wawekezaji wetu tunaotumia muda mwingi katika kuwaita kuja kuwekeza nchini.

- **Shirika la Biashara la *ZSTC***

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la *ZSTC* linakua kwa kasi katika biashara linazozifanya, ambapo kwa upande wa Dar es salaam wamekuwa wakitumia nyumba ya kukodi kuendeshea biashara zao. Ili shirika lijiendeleze zaidi kibiashara, ni vyema nyumba hiyo wakauziwa hasa kwa vile wameshaitumia kwa muda mrefu, lakini pia wana nia ya kuinunua. Kamati inaomba mazungumzo yaliyoanza yaendelee katika ngazi za juu ili kufanikisha azma hiyo.

- **Idara ya Umwagiliaji Maji**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii inajitahidi sana katika utekelezaji wa majukumu yake mbali mbali, japo kumekuwa na changamoto kadhaa zinazorejesha nyuma gurudumu la maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipotembelea idara hii, kulikuwa na tatizo la umeme lililosababisha kutokuwepo utendaji mzuri wa shughuli za idara. Kama tunavyojua kwamba idara inategemea sana maji na umeme katika kazi zake, hivyo ni vyema suala la umeme lipewe kipaumbele ili matatizo kama hayo yasiweze kutokea na azma yetu ya kujitosheleza kwa chakula itimie.

6.0 Mwisho

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutoa shukrani kwa Wajumbe ni vyema nikasema haya machache kuhusu Kamati yetu ya Fedha na Uchumi. Kamati ya Fedha na Uchumi inashauri kuwepo kwa mawasiliano yaliyo sahihi baina ya Wakuu wa Idara, Taasisi na Watendaji wake, ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza ambazo si wa lazima, wakati Kamati zinapokuwa katika kazi zake za kawaida za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mawizara.

Vile vile tunaomba kungekuwa na uwezekano wa kamati kuongezewa muda wa ufuatiliaji wa shughuli za mawizara kwani muda uliowekwa ni mdogo sana na kusababisha kushindwa kufikiwa kwa baadhi ya taasisi na idara za mawizara.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe kwa usikilizaji wao mzuri na ninaamini kuwa ripoti iliyowalishwa kwao wameisoma kwa makini na kwa utulivu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu. Lakini pia nikushukuru wewe au nikupongeze Mhe. Mwenyekiti, kwa kiti chako kwa mara ya kwanza kukikaa leo na kuwa ni historia kwa Baraza letu hili kuwa kiti hicho kimekaliwa na mwenyekiti mpya mwanamke.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini pia makamo wake na wajumbe wote wa kamati hii na makatibu wao, na wale wote walioshirikiana kuhakikisha kuwa taarifa hii inaletwa katika Baraza hili na na kujua matatizo na maendeleo katika harakati zetu za kuiambia serikali au kuielekeza, pale palipopunguka pakazwe uzi ili tuhakikishe mafanikio yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza mawaziri wote wa wizara tatu pamoja na makatibu wao, kama kuna manaibu makatibu, wakurugenzi, makamishna kwa sababu wizara hizi zimekusanya fani mbali mbali kwa ajili ya kazi zao. Kamati hii ina wizara tatu, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mimi kwanza nianze na Wizara ya Fedha, naamini chachu ya maendeleo ni makusanyo mazuri ya fedha na bila ya makusanyo mazuri kwa ajili ya kuendeleza nchi basi matatizo hujitokeza. Kwa upande huu pamoja na kuwa kuna matatizo ya hapa na pale, lakini nachukua fursa hii kwa makusudi kuipongeza kamati kwa kusimamia vyema shughuli mbali mbali za kufuatilia

vianzio vya mapato. Lakini pia naipongeza Wizara ya Fedha kuanzia Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameionesha kwa kipindi chote hichi na mafanikio yanaonekana.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoka mbali, tunatoka safari ndefu na tulipo na *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tunakokwenda kutakuwa kunaendelea zaidi kwa mtiririko. Hii nasema kwamba, uchumi wa nchi huleta maendeleo kwa nchi, kwa hivyo, wizara hizi zote kuanzia wizara ya fedha na zilizobakia zote zinategemea mapato ya fedha ili ziendeshe shughuli zake.

Kwa hivyo, mimi niipongeze kamati hii kwa kusema kwamba kuna baadhi ya taasisi au wizara ambazo na sisi wakati wa kamati zetu tutazisemea kwa upande mwengine, kwamba bado kuna ufinyu mdogo mdogo ambao si walazima huwa unakosekana kupata kiwango ambacho wamekisiwa wakipate. Lakini kutokana na ufinyu uliokuwepo huwa zinakosekana. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wale wenzetu ambao wanakuja katika kuomba fedha mbali mbali kwa ajili ya maendeleo na shughuli za jamii ndio maendeleo yenyewe wasaidiwe sana.

Mimi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto wizara zangu zote zinaitegemea serikali kwa asilimia mia moja, hakuna hata wizara moja katika nilizobahatika mimi inayozalisha. Kwa mfano Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ingawa nitakuja kuisemea baadae lakini nasema kwa Wizara ya Fedha sasa ambayo inatoa fedha zile kuwahudumia wananchi. Naiomba sana kuhakikisha kuwa fedha zinazoombwa na Wizara ya Afya zipatikane.

Kwa sababu wananchi wengi wanaitegemea kwa mambo mbali mbali kama vile madawa, huduma nzuri za afya zinazoendelea vijijini kwa wingi na mambo mengineyo. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wanapokuja wenzetu hawa kwa sababu kuna wagonjwa, pamoja na jitihada nzuri iliyopo ya wizara hii pana haja ya kuangaliwa kwa jicho la huruma wanapotokezewa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, wizara hii pia tosha kwamba ni uti wa mgongo katika uchumi wa nchi yetu, hasa tukiangalia zao la karafuu, zao la baharini yaani mwani na samaki. Kwa sababu bahati nzuri Zanzibar ni nchi ambayo imezungukwa na bahari, tunaringa sana.

Mara nyingi mimi huiomba sana wizara hii pamoja na jitihada zake za kutafuta wafadhili wa *MACEMP* na wengine kwa wakulima na wafugaji, lakini pana haja ya kuwaomba wafadhili kupitia uvuvi wa kileo tuhakikishe kwamba tunapata nyanja au vifaa mbali mbali vya uvuvi na uwezekano uwepo wa kutafutwa kiwanda kikubwa cha kusindika samaki, ili nchi iweze kusafirisha samaki hao na kupata tija zaidi. Namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie.

Lakini jengine hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo lililokuwa gumu sasa hivi katika hali ya dunia kuliko uchumi wa nchi kupitia mambo ya kilimo. Wananchi wanalalamika chakula bado ghali katika nchi yetu, leo ukikuta mchele shilingi elfu moja kesho elfu na mia moja, elfu moja mia mbili mfano tu. Sasa niiombe Wizara ya Kilimo kupitia taasisi zake zinazohusika bado kilimo tukiite na kukipa lile jina la wenzetu si vibaya. Kuiga jambo zuri si vibaya Mhe. Mwenyekiti, lakini kuiga uovu ndio vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na sisi tuite Kilimo Kwanza. Wananchi wetu wameitikia wito mkubwa sana wa kilimo, lakini bado kilimo chetu kiko duni nab ado hakiko katika mtiroroko wa kuangalia kwamba, tukilima kwa wingi na tukiwa na zana za kulimia vizuri basi mahitaji ya mavuno yatakuwa makubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa kuzingatia hili nalo aliangalie.

Halikadhalika, mazingira yetu pamoja na semina tumepata mswada umekuja lakini bado pana haja ya kuzingatia mazingira yetu yanaharibika vibaya sana. Mhe. Mwenyekiti, utalii umevinjari sana katika nchi yetu na hizi ni fedha ambazo tunazihitaji. Lakini naiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira isimuonee aibu mtu yeyote au mwekezaji yeyote pindi akivunja sheria katika fukwe zetu akipindukia kile kiwango ambacho kawekewa mita 15 au 25.

Mhe. Mwenyekiti, hayo yamo na yanaharibu mazingira na tunaambiwa mmong'onyoko unaokuja *yarabi salama* kisiwa chetu baada ya muda fulani huenda kikawa hakipo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu asitufikishie huko.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri mazingira ni jambo la mwanzo vile vile na mazingira ni uhai katika kustiri kisiwa chetu, sisi wenyewe, vizazi vyetu na vinginevyo Mwenyezi Mungu atakaowajaalia huko mbele.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna mtiririko wa hali ya juu wa shughuli mbali mbali za wafanyabiashara wetu. Wafanyabiashara wanaitikia wito mkubwa sana wa serikali, wafanyabiashara tuwasikilize kutokana na maoni mbali mbali. Mimi ningeiomba wizara bado pana haja wakae wafanyabiashara na idara zinazohusika ili kuangalia mambo yanayoleta usumbufu yatafutiwe ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, suala ambalo limejitokeza hivi sasa wananchi wanalalamika kwa mambo ambayo chanzo chake hatukifahamu. Lakini pia niiombe serikali inapotokea haja ya kutokea kama bei zimeongezeka basi wananchi waambiwe ukweli. Hakuna jambo zuri katika maisha yetu tunayoishi kuliko kuwa tuko

katika uwazi kabisa. Kwa sababu siku hizi mtandao unatembea dunia nzima uko wazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano leo sukari ghafla imepanda bei inauzwa shilingi 1,500/= kutoka shilingi 1,000/= wananchi wameshtuka kuna nini. Mfanyabiashara anakwambia ushuru umeongezeka, mimi sijausikia, maana bajeti imepita hapa, Wizara ya Fedha ipo haikutangaza neno la ushuru hata siku moja.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri hili kidogo alielezee wananchi wafahamu. Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo zuri katika shughuli zetu zozote zile kuliko mwananchi kumuelekeza tu na akafahamu, kama hukumuelekeza hatari. Namuomba sana Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji alitolee ufafanuzi suala hili.

Lakini mambo mengine pamoja na hayo tuseme tu kwamba mimi nawapongeza wafanyabiashara wote kwa juhudi zao za kuisaidia nchi yao. Pia wananchi wetu japo ghali ipo lakini sitaki iwe ghali nataka iwe rahisi, maana itafutiwe ufumbuzi wa kupatikana ile bei ya kuwanusuru wananchi wetu wasiingie katika ukali wa maisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mara nyengine tena kuanzia Mwenyekiti na wasaidizi wake wote na naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Awali ya yote naomba nimpongeze Mhe. Mwenyekiti na kamati yake kwa namna ya uwasilishaji bora wa ripoti yao. Hii maana yake ni kwamba walijaribu kwa kadri walivyoweza kutumia muda mchache waliopewa kuhakikisha kwamba wanaifanya kazi katika mazingira ambayo wamewezesha angalau kuwa na ripoti kuipeleka hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika ripoti yao naomba nizungumzie mambo matatu. La kwanza nikubaliane na Mhe. Mwenyekiti kwamba hali ya karakana za matrekta zinakatisha tamaa sana. Hatuwezi kama nchi kwenda katika kilimo bora ikiwa hali ya karakana zitakuwa vile zilivyo. Bahati mbaya sana tumeshindwa hata kuzipa hadhi, yaani ile hadhi yake haijulikani. Sasa hili ni jambo la ajabu sana kwamba hatujui kama ni shirika, ni mamlaka, ni idara, ni kitengo, alimradi zipo tu.

Sasa ikiwa tuna taasisi muhimu kama zile halafu hatujui hata zina hadhi gani, kwa kweli tunafanya mchezo sana katika kilimo. Kwa hivyo, tutegemee siku zote kuwa ni watu wa uagiziaji tu. Kwa kweli nchi haiwezi kuendelea kama itaendelea kuagizia sana. Wataalamu wa uchumi wanatwambia mfumko wa bei wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa unasababishwa na uagiziaji hasa wa chakula.

Sasa ikiwa ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kutafakari na suala hili tumelizungumza muda mrefu katika Baraza hili, hadhi ya karakana za matrekta Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, mimi bahati nzuri miaka ya nyuma niliwahi kufanya kazi katika Karakana zile ya Unguja na Pemba zilikuwa ziko nzuri sana. Lakini leo zimefika pahala tulitembelea sisi pana *workshop* pale hata zile *tools* za kuchongea baadhi ya vipuri zinashindikana. Sasa ni tatizo hilo.

Wenzetu waliotilia maanani katika kilimo walianza na karakana kama zile, baadae wakaamua sasa waanze kujiundia wenyewe zana ndogo ndogo za kilimo. Halafu wakaamua sasa waunde matrekta wenyewe, walianza na matrekta ya mikono baadae wakenda kwenye kufanya matrekta makubwa. Tunaambiwa historia ya zana za kilimo za Korea wakati wa kiongozi Komredi Kim Il Sung alimwambia Waziri wa Kilimo nakupa miaka miwili nataka uniundie trekta *from nowhere*. Siku hizo ndio ukomunisti umepamba moto.

Kwa hivyo, akenda akajifungia na wataalam wake baada ya miezi 18 wakamwita wakamwambia mzee tayari. Basi akakusanya makamanda wake wa jeshi wakenda wakaangalia trekta liko tayari. Wakati wanatia *gear* kwenda mbele lile trekta likarudi nyuma. Akawaambia *yes*, angalau mmeweza, nakupeni miezi sita sasa mrekebishe mambo madogo trekta liende mbele. Mpaka leo Korea ni nchi moja ambayo iko mbele sana katika *manufacturing* ya *farm machinery*.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hatuwezi kuziacha Karakana za matrekta kama vile zilivyo halafu tutegemee miujiza katika masuala ya kilimo. Tunaomba matrekta kutoka Iran, kutoka Libya, Libya ana jangwa lakini anatengeneza matrekta. Kwa kweli umefika wakati na sisi wa kuanza angalau tumpe muda Mhe. Burhan Saadat Haji, tumwambie tunakupa miaka miwili angalau utuundie lile trekta la mkono. Ninaamini mimi tuna wahandisi wazuri ni kuwezeshwa wakapewa tu motisha kidogo, wakapewa zana, baada ya miaka miwili watatuundia *power tiller* angalau *made in Zanzibar*.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali na zaidi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira wakae waangalie sasa wafanye mapinduzi makubwa katika masuala ya Karakana ya Matrekta na Zana za Kilimo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi amelizungumza ni suala la umwagiliaji maji. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana kwetu. Ardhi ndogo ya kilimo ya Zanzibar tuliyonayo lazima iandaliwe utaratibu wa kilimo cha umwagiliaji maji. Tumesikia mara nyingi kauli za serikali katika suala hili, tumesikia kama kuna *irrigation master plan,* lakini ni *plan* sasa tunataka tuione katika vitendo.

Sasa tunaweza kuwa na *plan* kwa muda wa miaka 20 lakini *plan* hatushibi, tunataka tuione sasa *plan* iteremke mabondeni, tuone sasa watu wetu wanaingia katika suala la kilimo cha umwagiliaji maji.

Bahati nzuri au mbaya Zanzibar haina *potential* ya *surface irrigation*, yaani hatuna mito mikubwa wala hatuna maziwa. Lakini bahati nzuri tuna mvua ya kutosha na ambayo kila mwaka *volume and volume* ya maji yanapotea baharini.

Mhe. Mwenyekiti, huwa naangalia zaidi nikiwa Pemba katika vilima kwa sababu Pemba bahati nzuri jiografia yake ni vilima na mabonde, sasa ukikaa utaona mkondo wa maji Mwenyezi Mungu aliotujaalia mvua inanyesha inakimbilia baharini. Kumbe tungelikuwa wajanja kidogo na watu wenye mpango madhubuti basi vilima vile ilikuwa ni ku-*block* upande mmoja, bwawa tayari limejengwa huku na huku kwa mlima sasa ni ku-*block* upande wa mbele. Tayari umeshafanywa utaratibu wa kuyakusanya maji kwa ajili ya shughuli za *irrigation*.

Kuna nchi nyingi ambazo jiografia yake inafanana na Pemba wameweza kuendelea sana katika masuala ya uvunaji wa mvua na hivyo suala la umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipita katika Jimbo la Micheweni, jimbo ambalo mara nyingi huambiwa lina uhaba wa chakula, lakini niliona vitunguu maji vimemea vizuri sana. Kumbe lile eneo Mhe. Mwenyekiti, likipata maji kwa kweli linaweza kuzalisha vitunguu vikatosheleza Pemba nzima na labda na Zanzibar nzima.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira asaidiwe na serikali kuwa makini na wabunifu hasa katika suala la uvunaji wa maji ya mvua ili shughuli za umwagiliaji maji ziendelee vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la uvuvi ambalo jana na leo limezungumzwa sana suala hili. Mhe. Mwenyekiti, nimewasikia wenzangu wengi wanazungumzia suala la kilimo kwanza. Sasa mimi kauli hii ni nzuri kwa Tanzania Bara nchi ambayo ina eneo kubwa la ardhi kilimo kwanza kwao ni sawa. Lakini kwa nchi ya Zanzibar ambayo ina eneo dogo la ardhi na eneo

kubwa sana la bahari, basi mkakati ungelikuwa uvuvi kwanza, huu ndio ulikuwa mkakati muhimu zaidi. *(Makofi)*

Lakini kilimo kwanza kwa Zanzibar ni tabu kwa sababu tukikatiana vile vipande vya ardhi vidogo vidogo ikawa kila mtu aende katika kilimo hatuwezi kwa kweli kulishughulikia eneo ipasavyo. Lakini kwa ukubwa wa bahari tuliyonayo mita 200 kutoka Makunduchi au kutoka Tumbe au kutoka Micheweni. Ikiwa tutaamua kwenda na sera ya uvuvi kwanza tukajipanga vizuri, tutaliingia soko la Afrika Mashariki na sisi tutakuwa tunachangia vizuri katika *common market* ya Afrika Mashariki vizuri. Nchi zote tano za Afrika Mashariki tutakuwa na uwezo wa kulisha kitoweo na sisi tutakuwa tunafanya biashara nzuri bila ya ushuru.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala ambalo sisi kama Zanzibar na wizara hii pamoja na serikali kwa jumla tunalifanyia mkakati mzuri. Mhe. Mwenyekiti, naona unanitazama sitegemei kuchukua muda wako mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho ni masuala ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Fedha. Kwanza mimi naomba niungane mkono na Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba katika kipindi hichi na hasa cha pili cha awamu hii serikali imejitahidi katika kuona kwamba inakusanya mapato vizuri, ni jambo zuri. Lakini bado maandiko mbali mbali na tafiti zilizofanywa zinaonekana hatujaweza kwa kadri inavyowezekana kugema vizuri mapato yanayotokana na utalii.

Sasa hili ni jambo ambalo lazima tulikalie tena kitako. Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii na Bodi ya Mapato lazima walitafakari suala hili kwa kina kuangalia wingi wa mahoteli tuliyonayo na wingi wa watalii wanaoitembelea Zanzibar na kile ambacho tunakipata kutokana na shughuli hiyo. Hili likifanyiwa kazi kwa kweli tunaweza tukaongeza kwa kiwango kikubwa chanzo chetu cha mapato. Tunaambiwa kwamba kuna nchi nyengine ambazo hazina mahoteli mengi kama sisi lakini bado wanakusanya zaidi kuliko ambacho tunakusanya sisi.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba sana kwamba ikiwa tumeamua utalii ndio sekta kiongozi sasa tusiregee katika hili kuona mapato yanayotokana na utalii tunayafanyia mzaha, tunatakiwa tufanye mikakati na tusiwe na muhali katika hili. Tumesoma baadhi ya maandiko kwamba kuna wenye mahoteli hasa wageni wanadanganya namna ambavyo vyanzo vya mapato vinaingia. Udanganyifu huo unasababisha nasi kukosa mapato makubwa ambayo tunayahitaji.

Sasa nchi haiwezi kukubali kuendelea kuwa *cheated* kwa muda mrefu, inaweza kuwa *cheated* mara moja mbili lakini hatimaye lazima iamke na mikakati ambayo itadhibiti *cheating*. Sasa hili ndio jambo la msingi ambalo naiomba sana Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Fedha kuangalia namna gani suala hili litafanyiwa kazi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nichukue nafasi hii kutoa mawazo yangu kidogo katika ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara na pia nimpongeze Mhe. Mwenyekiti na kamati yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na inapendeza.

Mhe. Mwenyekiti, naanzia ukurasa wa 2 Idara ya Misitu. Mhe. Mwenyekiti, hapa Idara ya Misitu kamati haikueleza kitu. Kwa sababu kwa maandiko ambayo yako hapa kifungu 2.1.1 haijaonesha kwamba Idara ya Misitu inaendeleza misitu na inatoa tija. Kilichosifiwa hapa kidogo ni ufugaji wa nyuki na maendeleo yake, kubwa linalotia hamu kwamba mzinga mmoja zinaweza zikavunwa lita 20 za asali. Lakini ile mantiki ya misitu hasa haijaelezwa. Bahati mbaya mistari ya maelezo haikufika hata 10 wakati hii Idara ya Misitu ipo peke yake inaitwa idara lakini inavyoonekana maendeleo yake ndio hayo. Tungepata angalau maelezo ya Idara ya Misitu, maendeleo yake na matatizo.

Kwa sababu Idara ya Misitu Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi unapofika msimu wa karibu na mfungo wa Ramadhan huwa kuna mgogoro mkubwa baina ya Idara ya Misitu na wananchi. Kwa vile inavyovuma utafikiri labda huo msitu umepewa thamani kubwa. lakini kwa maandishi haya naomba kamati itakapokwenda mara ya pili kama itakuja kuchaguliwa hii au nyengine mwaka 2011 angalau ipate ukurasa mmoja wa maelezo. Lakini kama maelezo yenyewe ndio haya basi kamati imekula hasara katika kutembelea kwake. Naiomba sana inapofanya kazi iwe inafanya na isitanie. Kama haikwenda bora ingesema kwamba hatukupata kutembelea Idara ya Misitu kutokana na hali haikuruhusu kwa maelezo haya.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa huo huo wa 2 nizungumzie Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana idara hii, kama ndio ziko idara zinapeana vyeo basi hii ingeitwa idara kiongozi. Maana yake ina maandishi mengi na harakati zake zinaonekana. Lakini kwa upande mwengine pia ni idara ambayo inapunguza kwa kiasi kikubwa umaskini. Kwa sababu pana vikundi vingi tu ambavyo vimepata misaada hasa kupitia *MACEMP* na *TASAF* inaonekana kwamba inafanya kazi vizuri sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika jadweli na mchanganuo imetaja miradi lakini katika ufafanuzi haikueleza miradi ipi na ipi kwa sababu wana miradi mingi. Wana miradi ya ufugaji, wana miradi ya uvuvi, wana miradi mingi tu ambayo ina ukweli ndani yake. Lakini kwa maelezo haya imefafanua tu kwa mfano labda kwenye jadweli kwa Unguja kuna jumla ya miradi 114 yenye thamani ya bilioni 2,032,983,000.80, ni miradi 20 kati ya miradi 133 iliyopatiwa fedha.

Sasa miradi yenyewe ipi na tunasema siku hizi kuna ukweli na uwazi. Hapa pana ukweli lakini hapana uwazi. Kwa hivyo, ningeomba kamati itakapofanya kazi yake mara ya pili najua tu imepata maelezo na imepata mchanganuo mradi upi, uko wapi. Kwa sababu tukipata kujua mradi upi na uko wapi tunapata kuelewa hasa kwamba eneo fulani mradi huu wa *MACEMP* umefika.

Lakini namna hii hatuwezi tukajua wapi wamepata mradi, wapi hawajapata. Kwa sababu idara inajitahidi kutoa miradi katika maeneo mbali mbali lakini kwa mbali wananchi bado wanalalamika, kulalamika yao kwa maelezo haya itakuwa halali maana hawajijui. Lakini kama anajijua mtu anaweza akajua tu, akijua anaambiwa bwana mradi fulani umekwenda pahala fulani na huko ndiko uliko. Kwa hivyo, kwa kufuatilia fuata utaratibu huu.
Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa niingie Idara ya Kilimo lakini bahati nzuri wenzangu wameizungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, kinachonisikitisha tu kwamba Idara ya Kilimo ina upendeleo kwa sababu inashughulikia sana mpunga. Kweli katika chakula ambacho kinatambuliwa sana Zanzibar ni mchele. Lakini ardhi ya Zanzibar inakubali kutoa mazao mbali mbali ikiwemo kunde, mbaazi na kadhalika. Lakini vipaumbele vyote pembejeo, mbolea na kila kitu, hata hii miradi ya umwagiliaji inakwenda kwenye mpunga na mboga mboga tu.

Sasa ningewaomba watu wa Idara ya Kilimo wakaona kwamba kilimo cha maweni kinachukua nafasi kubwa katika kuwasaidia wananchi. Sijapata kuona katika ripoti hii na pengine palipojitokeza kuonekana kwamba iko sehemu wamepatiwa angalau mafunzo ya umwagiliaji katika maeneo ya maweni, si kwa migomba, si kwa mahindi, si kwa chochote.

Kwa hivyo, bado Idara ya Kilimo inajishughulisha sana nay ale maeneo ambayo wakiandika ile miradi yao basi wanaweza wakapata ufadhili. Nafikiri hiki ndio kinachowavutia zaidi kuliko ule uhalisia wa kazi yao. Naomba wajitahidi sana kuona kwamba zaidi wanashughulika na mambo ya kupunguza umaskini. Lakini tokea siku hizo mkulima wa maweni bado yuko vile vile na zana zake za kienyeji, hawana pembejeo.

Hata hii faida iliyotangazwa mwaka juzi na Mhe. Waziri ya kupunguza bei ya mbolea haiwasaidii wakulima wa huko, wala hawaelekezi kwamba wewe kama mwenzio katumia mbolea hii ya samadi au katumia mbolea hii ya chumvi chumvi, wewe tumia mbolea ya aina nyengine. Kwa sababu siku hizi tuna wanyama wengi kuku na mbuzi lakini bado hawapati maelekezo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kuna baadhi ya miaka hutangaza kwamba inanunua matrekta ili kukuza kilimo. Lakini bahati mbaya sana inaponunua matrekta haitambui kwamba matrekta hayafanyi kazi kama karakana ya matrekta haifanyi kazi. Itakuwa kazi yetu tunanunua mapya tunauza mabovu, kumbe si mabovu tunashindwa kuyafanyia *service* na mambo mengine. Kwa hivyo, serikali siku zote itakuwa inanunua tu matrekta. Kama ningekuwa ndio muagiziaji ningefurahi kwa sababu katika kuagizia na mimi sikosi chochote.

Labda hichi ndio kinachowavutia sana waone kwamba wasitengeneze wawe wanaagizia ili kile kinachobakia au zile pesa nyengine kama alivyozungumza siku moja Mhe. Abubakar Khamis Bakary kumwambia Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwamba *ten percent for boss.* Nafikiri na hizi ndio hivi hivi. Kwa sababu haiwezekani hata siku moja kwamba wewe unahakikisha kwamba unaagizia matrekta huna mawazo ya kwamba utaya-*maintenance* vipi ili yafanye kazi katika kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri asipojirekebisha kwa hili bajeti ya mara hii mimi na Mhe. Said Ali Mbarouk tutakuwa wakali sana kwa sababu tunaona kama mambo ya mchezo. Mnamo miaka ya 1998/99 tulikuwa tuna matrekta mengi sana lakini yote yalikwenda Tanzania Bara, hapa tunasema mabovu hayatiwi mnada, hayafanywi chochote yanapelekwa tu. Mpaka tulipokuja kukaa makini yamebakia matrekta mawili hayalimi, hayafanyi chochote. Kwa hivyo, huu unakuwa ni uzembe. Sasa tunaomba tuondoe uzembe katika shughuli hizi za kumpunguzia mwananchi umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niende ukurasa wa 5 katika Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Mhe. Mwenyekiti, idara hii inajitahidi sana na karibu wafugaji wata-*cover* soko ambalo liko hapa Zanzibar. Kwa kweli tunawashukuru sana watu wa idara. Isipokuwa katika maelezo yao kifungu 2.1.8 wamelalamikia maradhi ya mahepe kwa vifaranga pamoja na kuku wenyewe. Hili ni kweli.

Lakini nataka niwaulize hapa ndio wamegonga hawana tena nguvu ya kuweza kuyapiga vita maradhi haya ya mahepe. Kwa sababu mwaka juzi walijaribu kuleta chanjo hata mimi mwenyewe niliona itakuwa haina maendeleo. Maana yake chanjo ukaitie kwenye jicho la kuku halafu itamsaidia kuku mzima kumkinga na mahepe. Ilifanyika lakini haikusaidia chochote na matokeo kama

yalikuwa ya utafiti hatukupata ripoti kwamba ile chanjo waliyoikusudia imefikia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, bado mimi nawatetea wafugaji wa kuku wa kienyeji kwamba wana jitahidi sana lakini hawafiki pahala. Maana rafiki yangu hapa ananinong'oneza kwamba alikuwa na kuku wengi lakini hawafiki muda wanakufa kwa haya mahepe.

Kwa hivyo, tuone kwamba idara inajitahidi, imejitahidi kwa mambo mengi, lakini kuhusu kuku naomba sana kwamba wajitahidi ili tupunguze maradhi ya mahepe mfugaji wa kuku wa kienyeji ajione kwamba na yeye anasaidiwa katika kuona kuwa hali ya maradhi ya mahepe inapungua nchini.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nizungumzie Idara ya Utalii. Mheshimiwa Idara ya Utalii bado inachezea sana fukwe hasa ukanda wa mashariki. Kwa sababu wingi wa mahoteli yalioko ukanda wa mashariki na hali halisi ya maendeleo ya ukanda huo inaonekana hayalingani hata kidogo. Mategemeo ya wananchi katika kuanzisha utalii walizani kwamba watafaidika sana wale ambao wanatoa ardhi zao, walifikiria watafaidika mwanzo, kumbe kinyume hayakuwa hayo ni watu ambao wako duni. Lakini kinachowasaidia kidogo ni miundombinu inayopita mule moja kwa moja na wao wanapata kufaidika, lakini katika shughuli za maendeleo hawafaidiki.
Mhe. Mwenyekiti, ninachokusudia kukizungumza hapa ni kwamba serikali ione inatenga kifungu cha fedha. Kwa mfano asilimia 1 au 2 ambayo ibakie kule katika shughuli za maendeleo ya maeneo yale, kama si hivyo basi tutakuwa tunaumia sana. Kwanza hizo fukwe zenyewe zina malizika na watu wa ardhi hawana utaratibu wa kutoa ardhi, kwa pande zote tunaumia. Kwa hivyo, naomba sana hii Idara ya Utalii ione kwa jicho la huruma kuwa inaiambia serikali kwamba inapozalisha kule fedha ibakisha angalau asilimia 1 katika 100 iwe inashughulikia maendeleo ya maeneo hayo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsate.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, mimi mada yangu itakuwa moja tu sio kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba wananchi wetu wengi katika visiwa hivi viwili mara zote katika uhai wetu tunategemea kilimo. Lakini jambo la kustaajabisha kilimo chenyewe ambacho kilichoanza, yaani kilimo kile cha asili bado hakijaonesha maendeleo makubwa juu ya kilimo. Hii ni lazima kutakuwa kuna mapungufu, haiwezekani kwa muda mrefu watu sisi tulioko katika visiwa hivi tangu zama na zama tukaendelea na kilimo cha aina ile na ikawa ndani yake hatuna mabadiliko. Kwa hivyo, hilo nilitaka Mhe. Waziri alione kuwa hakuna mabadiliko makubwa sana kwa wananchi wetu katika kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nilizungumze ni kwamba tunataka sote tuone kutokana na hali ilivyo hivi sasa, kutokana na hali ya hewa *climatic changes* zinazotokezea hivi sasa. Kwa kweli hali ya hewa sote tunaiona hivi sasa kwamba kinachojitokeza ni joto jingi sana na kinachojitokeza ni kuwa na mapungufu ya mvua, ambapo tunasema watu wetu hawa hawa wakulima watakuwa mara zote wanategemea kilimo. Lakini kwa sababu ya upungufu wa hizi mvua, hata hicho kilimo chenyewe kinakuwa kidogo na uimarishaji wenyewe unakuwa ni mdogo na maendeleo yenyewe ya kilimo yanakuwa ni madogo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ya upungufu wa mvua kuna mambo ambayo ndani yake yamejitokeza. Katika vyakula vyetu na matunda tuliyonayo kwenye nchi hii, yametokezea kuwa na wadudu waharibifu ndani yake. Kutokana na upungufu huu wa mvua na kuna mimea ambayo ni mikubwa inahitaji mvua nyingi na kuna mimea mingine ni mdogo midogo ambayo haiwezi kustahamili katika kipindi cha kiangazi inakufa, ama itakufa moja kwa moja au itapata hujuma ya wadugu.

Sasa kama wizara ya kilimo hali hii inaeleweka kwenye miti mikubwa mikubwa ambayo inazalisha matunda makubwa na kwenye miti midogo midogo ambayo inazalisha matunda madogo madogo. Hali hii tunapokuwa tunazunguka katika maeneo tunaiona hali yenyewe ambayo bado haijawa ya kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano katika kilimo cha miembe, tunaona kwamba ni eneo moja tu au mawili wizara ilishughulikia kuweka mitego kwa ajili ya kuwatega wale nzi madume na sehemu nyengine zimeachiliwa kama zilivyo. Sasa hazijaendelezwa mwahala mwingi ili kuona kuna haja kuondosha hawa wadudu nzi dume ambao wanasababisha maradhi haya ya maembe. Hatujui athari za maembe haya baadae kwa binadamu, ingawa wengine wanasema kumla funza ni kinyesi tu, lakini *biological* hatujui kama inaleta athari au haileti, hatujaarifiwa katika utafiti wao.

Kwa hivyo, pia hapa nilikuwa nataka nitilie mkazo kwa wizara ya kilimo, kuwa matunda sasa hivi imekuwa ni chakula muhimu, wenyewe tuliokuweko kule visiwani tunatumia na mengine tunasafirisha katika sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, hili suala lisiachiliwe mpaka likaharibika kiasi hicho.

Mhe. Spika, ukiangalia katika hawa wadudu waharibifu mbali tuna miembe, ukiangalia vile vile katika michungwa iko katika hali mbaya, kama haukufa mchungwa basi utaukuta mchungwa umeelemewa na wadudu wengi sana. Kwa hivyo, utaukuta ule uzazi wake unaotoka katika matunda ni dhaifu, sio mazuri

na hayana maji ya kutosha kutokana na ukame wa mvua. Kwa hivyo, hali hii imejitokeza kila mahala.

Vile vile tunaona hali hii imejitokeza kwenye mihogo, mihogo mingi inaingiliwa na wadudu. Hii hali inaendelea na si kwa miembe tu, si kwa michungwa na wala si kwa milimau sasa hivi inaendelea mpaka katika sehemu za mipunga. Kwa hivyo, hii hali hasa katika sehemu za chakula cha mpunga utakuta wadudu sasa hivi wanaanza kufanya hujuma katika mipunga.

Mhe. Spika, mimi nasema kama hali ni hii ambayo inajitokeza, basi wizara ina wafanyakazi wake na ina watu ambao ni wa kushughulikia kilimo katika maeneo mbali mbali, lakini sisi tunaopita katika kila mahala hatuoni mabadiliko ya utekelezaji katika suala hili. Kwa hivyo, hapa nataka nimjulishe Mhe. Waziri kwamba pamoja na yote hayo ambayo nimeyaeleza hili hitilafu ndogo ndogo zipo na zinaonekana wazi wazi na hatuoni huduma ambazo zinatolewa kwa watu wa kilimo kupita wakaangalia hii mimea, wakatoa ushauri kwa wakulima au wakawasaidia dawa au wakawaeleza kwamba nendeni pahala fulani mkanunuwe dawa kwa ajili ya wadudu ambao wanaharibu matunda hayo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo nimelichunguza ni kwamba tunajua kilimo hakiwezi kunogea au kikawa kizuri zaidi hadi pale ambapo utaweza kuongeza mbolea. Sasa hapa hatuelewi kwamba katika matumizi ya kilimo watu wanatumia hizi mbolea kwa wingi au hawatumii mbolea, na ikiwa hawatumii kwa nini hawatumii je, hawana pesa ya kununulia mbolea au je, hawana ujuzi wa kutumia mbolea, au wanahisi kwamba labda mbolea si kitu muhimu, au pengine wanaweza kufikiria kwamba mbolea ni kitu muhimu lakini uwezo wa kununua mbolea hawana. Sasa hili ni suala muhimu la kuwa linaonekana kwamba watu wengi hawatumii mbolea na utakapokuwa hutumii mbolea kwenye ukulima wa mpunga basi kipato chake kitakuwa kidogo.

Halafu vile vile Mhe. Waziri uelewe katika suala hili la mpunga kuna suala la mbolea kutiwa katika mpunga, hawatii watu mbolea katika mpunga. Kwa hivyo, kipande ambacho kilichotumiwa vizuri kwa kutiwa mbolea kitakuwa na kipato kikubwa sana na kipande ambacho hakikutiwa mbolea kitakuwa na kipato kidogo. Kwa hivyo, suala hilo nalitolea indhari kwamba katika maeneo mengi watu hawatumii. Sasa hatujui kama katika maeneo yao madawa yapo, kama madawa yapo au pengine ni ghali, inahitaji kufanyiwa utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kama tunavyoelewa siku hizi kwamba kilimo chetu tunaondokana na kutegemea mvua kwa wingi, yaani mvua hazipatikani kwa wingi. Kwa hivyo, kama mvua hazipatikani kwa wingi, kuna maeneo mengi sana ambayo yanahitaji kufanyiwa *irrigation*.

Kwa mfano katika Jimbo langu la Konde, nina eneo *vast land* na hili eneo watu mara nyingi watu wanakosa kulima kutokana na upungufu wa mvua. Lakini Konde tunayo maji ya kutosha. Kwa hivyo, nilikuwa namshauri Mhe. Waziri katika hili suala apite kuyaona maeneo ambayo tunayaona sisi ni makubwa na yanaweza kufanyiwa kilimo kwa njia ya *irrigation*. Sasa mimi nataka nimkumbushe kwenye suala hili kwamba si vyema kuangalia upande mmoja tu wa kilimo, ambapo kuna uwezekano kwa sehemu mwingine kupatikana maji ya kufanyia *irrigation*. Lakini tuangalie na maeneo yale ambayo ni magumu kufanyiwa *irrigation* ili na sisi tuweze kusaidiwa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, sisi pale katika Jimbo letu la Konde kuna kituo kikubwa sana cha Matangatuani ambacho zamani kilikuwa ni *Matangatuani Agricultural Station*, ambacho hiki kinafanywa kama ni kituo cha utafiti. Lakini kwa hali ya kituo cha Matangatuani kilivyo hivi sasa bado kituo hiki hakijafikia *standard* ambayo inayotakiwa kwa kituo hiki ili kiweze kuwasaidia wananchi wa maeneo yale. Kwa hivyo, hiyo ni indhari au maelezo hayo nampa Mhe. Waziri ili ajuwe kwamba hili suala bado halitekelezwi vizuri kama inavyostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache na mimi naunga mkono hayo yote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kuchangia ripoti hii ya kamati ya fedha na uchumi. Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kilimo, kama walivyoanza wenzangu na mimi nataka nianzie hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na Mhe. Ame Mati Wadi kusema kwamba Wizara ya Kilimo ina wataalam wengi kabisa, lakini bado wanafanya mambo yao kwa upendeleo, kwa sababu sehemu za maweni bado hawajatutendea haki, hatujaona jinsi wanavyotoa elimu kwa watu wanaolima katika sehemu za ukame za maweni. Nyinyi ni mashahidi Waheshimiwa Wajumbe kwamba Micheweni ni eneo moja ambalo hapana asiyejua kama ni eneo moja ambalo ni la ukame na kila siku linakuwa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita niliwaambia waheshimiwa kwamba Micheweni haiwezi kuondokana na matatizo kwa kwenda kusaidiwa mara moja. Lakini cha msingi cha kuondoa matatizo ya Micheweni ni kufanya kitu ambacho kitakuwa ni endelevu kuondoa matatizo ya Micheweni. Sasa kitu ambacho ni endelevu cha kuondoa matatizo ya Micheweni ni kama kuwaelimisha na kuwaelekeza jinsi ya kilimo kwa wakati tunapopata mvua

kama hizi zinazoelekea za masika. Kwa sababu Micheweni sio kama haviwi vyakula, vinakua.

Mhe. Mwenyekiti, nakuhakikishia ukiuona muhogo unaolimwa Micheweni na ukaambiwa unatoka katika ardhi ya Micheweni kwa siku za mvua kama hizi huwezi kuamini kabisa. Muhogo mnene, unaoiva, mtamu na ni wa maajabu! Pia na ndizi ya Micheweni Mhe. Mwenyekiti, nakuhakikishia kama itazaliwa ndizi ya mtwike kweli ya Micheweni basi hakuna anayeweza kuibeba humu kwa ukubwa wake. Lakini sasa watu wa maeneo yale ya ukame wanataka kuelekezwa, kwa sababu kuna vilimo vinavyostawi katika sehemu za ukame, lakini hawana maelekezo. Watu wanaelekeza sehemu za mpunga tu.

Halafu suala la pili Mhe. Mwenyekiti, naomba nitowe maelezo yangu kwa masikitiko, kwa sababu Micheweni kama tunavyozungumza kwamba ni eneo moja la watu ambao wanahitaji msaada kwa hali na mali. Leo kuna bonde la mpunga ambalo wanalima watu wa Micheweni limeharibika huu ni mwaka wa 5. Kulikuwa kuna msingi, msingi ule umevunjika, sasa yanaingia maji ya chumvi. Mhe. Rais aliahidi kwamba bonde lile litatengenezwa, lakini kwa masikitiko mwaka wa 5 huu bonde lile hakuna anayelishughulikia. Anayelishughulikia ni Mbunge na Mwakilishi, sisi hatuliwezi kwa sababu fedha zinazotakiwa ni nyingi, tunalishughulikia lakini hatulimalizi, tunaendelea kulishughulikia.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kila siku nampa kilio hiki, bado watu wa mazingira pamoja na yeye mtu wa kilimo hawajalishughulikia hili bonde. Kwa hivyo, namuomba kwa heshima kubwa hili bonde walishughulikie ili wawaonee imani wale watu wa Micheweni na wao wapate kulima mpunga, hawana maeneo mengine isipokuwa ni eneo lile. Leo bonde lile linaingia maji na watu wa Micheweni walikuwa wanalima mpunga wanapata na wao wanajisikia hawapati tena kilimo ni mwaka wa 5 huu halifanyi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aje tushirikiane mimi na yeye twende katika bonde la Ukele ili aione hiyo hali na lishughulikiwe si hivyo kipindi cha bajeti na mimi nitakuwa mkaidi kweli kweli na nitazuia kifungu.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, ni suala la misitu. Kama tunavyojua Micheweni tuna msitu wa hifadhi ambao ni msitu wa serikali. Kule kuna kamati za misitu wanaoshughulikie ile misitu. Katika kipindi kilichopita nilieleza kwamba wale watu wanaoshughulikie zile kamati zinataka zipewe vifaa tu, angalau za kuingilia mule msituni, wana juhudi kubwa ya kulinda. Micheweni inasemekana kuna paa ambao kwa Afrika ya Mashariki wanapatikana pale Micheweni tu. Kwa hivyo, wale paa wanahifadhiwa na watu wa Micheweni wanawalinda, lakini wanataka zile kamati angalau zipewe vifaa

japo makoti ya kuingilia kule msituni tu. Lakini sasa wanawaacha tu hivi hivi hata kuwashughulikia au hata kuwapongeza tu. Wanajitihada lakini mwisho watachoka wale na wakiuacha msitu utaharibiwa. Watu wa Micheweni na kamati nyengine zilizopo ambazo zinauzunguka ule msitu wasaidiwe japo kuwapa vifaa vya kuingilia mule msituni wakati wa kufanya ulinzi. Nakuomba Mhe. Waziri hili ulizingatie na ulichukulie uzito.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la uvuvi. Mhe. Waziri hapa leo tulikuwa tukijadili sheria ya uvuvi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, watu wetu wa Micheweni, Kojani, Tumbe na baadhi ya sehemu nyengine kwa huku Unguja ndio wanaofanya shughuli za uvuvi, halafu ni wataalamu wa uvuvi na sio wataalamu kama hao wa nje, lakini utaalamu wao hawana vifaa vya kufanyia kazi na hawana zile zana za kufanyia kazi ndio vifaa vyenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hawa watu wawezesheni. Tuna bahari imetuzunguka na mazao ya bahari yamo lakini tunashindwa kuyavuna. Hebu jamani fanyeni jitihada, serikali nayo ijitutumuwe watu wake iwawezeshe, ili tupate hawa samaki tuwatumie, tusiwafuge tutawafuga mpaka lini.

Mhe. Waziri fanya juhudi zako kama inavyowezekana serikali na ijitutumuwe kwa hali na mali, hawa samaki tuwavuwe tusiwafuge. Tutawafuga mpaka lini watu waje wawachukuwe. Sisi tunafuga mali tukiendelea tunasema tuna umaskini tu mpaka lini. Hebu jamani jitahidi kutafuta hizi zana hii nchi yetu sio maskini, nchi yetu ni tajiri lakini tunaifanya iwe maskini sisi wenyewe. Kwa hivyo, jitutumuweni, ombeni misaada na fanyeni fikra za kila aina ili tupate zana ili hawa samaki tuwavuwe. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Mimi nitakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 6 ambapo kuna Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii ambayo imeletwa hapa, inasema ‘Sera ya Biashara ya Zanzibar imetungwa mwaka 2006 kwa lengo la kukuza na kusimamia mwenendo mzima wa biashara hapa nchini’. Kipengele cha kwanza ni kuendeleza mazingira mazuri ya kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, katika biashara, kisiwa kama hiki cha Zanzibar ni sawa sawa na visiwa vyengine vyote katika ulimwengu huu, ambapo kwa kweli biashara na viwanda ndio sera pekee ambayo inaweza kuinua uchumi ukainuka juu haraka. Ikiwa biashara inavia na ikiwa viwanda katika nchi hii hamna basi hiyo ni moja katika ukosefu mkubwa sana katika nchi hiyo kiuchumi na kimaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kwa bahati mbaya mpaka dakika hii imeshindwa kushajihisha suala la uwekezaji katika viwanda. Visiwa vyote hata ukiangalia jirani Mauritius, hapo ukienda Hong Kong, ukienda Singapore na visiwa vyengine vyote viliopo America huko chini vyote vile vimejiimarisha katika viwanda, biashara na utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya kwetu sisi hapa viwanda hamna kabisa. Ndio maana utaona katika malengo yale kushajihisha wafanyabiashara, wajasiriamali na wazalishaji bidhaa kutumia fursa ya masoko ya *East Africa Cooporation*, *SADEC*, *AGOA* na *AU* yameshindwa kwa sababu viwanda hatuna. Kama viwanda hatuna basi hatuwezi kusafirisha wala hatuwezi kuonesha hicho kitu tulichokuwa nacho.

Kwa hivyo, katika maonesho yote tunayokwenda sisi, tunakwenda kuonesha mahoteli tu basi. Lakini viwanda hasa vya kuonesha bidhaa kutoka hapa hatuna. Kwa hivyo, mimi ningeomba kabisa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kuweka mkakati madhubuti wa kuona kwamba viwanda vinafunguliwa Zanzibar na hivyo viwanda wawekezaji wapo lakini hapana mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda katika nchi yetu. Kwa hivyo, hili ni suala muhimu sana na ningeomba wizara hii ilichukulie hatua haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, ili viwanda vishamiri ni lazima pawe na maabara ya kuweza kutoa *quality* kama kule Bara TBS. Haiwezekani bidhaa zitengenezwe hapa Zanzibar lakini ubora wa bidhaa hiyo ikapasishwe Dar es Salaam. Ni lazima wizara yetu hii iwe na idara ya viwango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya idara hii ipo katika wizara ya afya, dunia nzima mambo haya ni kinyume nyume, wizara ya afya wana mipango yao, lakini wizara ya biashara inakuwa na kitengo cha kudhibiti viwango. Sasa hivi bidhaa zikiingia nchini zote zinapelekwa wizara ya afya, bidhaa zikitoka viwandani zinachukuliwa zinapelekwa Dar es Salaam TBS kuwekwa viwango. Kwa hakika haya ni matatizo ambayo ni moja katika matatizo ambayo yanakweza viwanda kufanyika hapa Zanzibar. Wizara ijitahidi ianzishe idara ya viwango na udhibiti bora wa bidhaa. Hiki ni kitu muhimu sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni maonesho ya kibiashara Zanzibar. Katika miaka 10 iliyopita tulianzisha sisi hapa maonesho ya kibiashara Zanzibar na yalianza vizuri sana. Shahidi wangu ni Mhe. Ali Juma Shamuhuna, tulikuwa katika kamati moja. Kwa bahati mbaya suala hili limefutwa kabisa mpaka sasa hivi Zanzibar imeshindwa kufanya *exhibition* hata ya watu 50 kuja Zanzibar kuonesha bidhaa zao, angalau na wa kwetu sisi hapa washajihike na wao waweze kuzalisha bidhaa zao.

Mhe. Mwenyekiti, wengi ambao wameanzisha viwanda hapa Zanzibar wamepata pingamizi mbali mbali ambazo zimewavunja moyo na viwanda vingine kupelekea hata kufungwa. Kwa hivyo, ningeiomba wizara ya biashara ikajikita zaidi katika suala hili, kwa sababu uchumi wetu haupati kukua kutokana na kila wakati tunaagiza, na tunaagiza mpaka tui la nazi wakati nazi zimo ndani, tunaagiza kila kitu na hatuzalishi kitu. Kwa hivyo, basi watu wetu hawapati kazi na hawapati kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo ningeomba lile suala la leseni, ile kamati iliyoundwa ya kushughulikia mambo ya leseni ikatupa angalau muda gani suala hili litamalizika. Imekuwa ni muda mrefu kamati imeundwa lakini bado haijaweza kufanya kazi zake kama inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 9 kwenye ZSTC Zanzibar na ZSTC Tanzania Bara. ZSTC Mhe. Mwenyekiti, ina mzigo mkubwa sana wa wafanyakazi. Wafanyakazi ni wengi ambao wanafanya kazi kwa misimu tu ya karafuu. Kwa hivyo, shirika hili linafanyakazi likiwa limebeba wafanyakazi wengi zaidi kuliko wanaotakiwa. Tungeomba mchakato ungefanyika au huo uamuzi wa kufanya hii biashara ya karafuu ikawekwa katika *private sector* ili iweze kufanikiwa kwa haraka zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuhifadhi wakati wako nakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 10 ambao kuna uenezaji wa huduma kwa wawekezaji. Hapa njia zote zimetajwa za kujitangaza, lakini suala la mtandao halikutajwa ambapo hii ndio njia mpya ya kuweza kupata kwa urahisi wawekezaji na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 12 kwa haraka haraka. Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Chuo hiki Mhe. Mwenyekiti, kilipoanza mwanzo kazi tulipata wanafunzi wazuri na kwa kweli walifanya kazi nzuri sana katika mahoteli yetu. Lakini kila siku zikienda mbele nafikiri wale mabingwa walianza kuondoka katika kile chuo, ikawa mwanafunzi akitoka pale ukimuajiri basi uwezo wa kufanya kazi ni mdogo sana ukilinganisha na miaka ya nyuma. Mhe. Mwenyekiti, tuna matatizo makubwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, leo mwenye hoteli akitangaza hapa Zanzibar anataka meneja wa hoteli mwenye ujuzi au mwenye *certificate* angalau diploma au digrii, basi hakuna Mzanzibari, wanaoomba wote ni kutoka Kenye, Uganda na Tanzania Bara. Mzanzibari akiomba humuoni hata mmoja. Ukitangaza unataka nafasi ya *chief cooker* hamna, ukitangaza *chief house keeper* hamna. Tunatarajia sisi kwamba watu wetu wote Wazanzibari waajiriwe katika mahoteli haya yanayojengwa katika nchi yetu. Kwa bahati mbaya zile fedha nyingi

zinakwenda kwa wale meneja, *chief cooker*, *house keeper* na viongozi wengine wa juu wa hoteli, wale ndio wanaochukua mishahara mikubwa. Mshahara mmoja wa meneja basi ni mishahara ya wafanyakazi 30 mpaka 40 wa kazi za chini chini. Tunashindwa kuwasomesha vijana wetu mpaka hii leo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mahoteli yamejaa mjini hapa na mashamba, lakini huwezi kumuambia Mtaliana kwamba katika hoteli yako ni lazima uwaajiri Wazanzibari, kwa sababu hakuna tena hakuna kabisa. Hiyo naweza nika-*challenge* kwa sababu tuna *advertise*, lakini Mzanzibari hakuna hata mmoja. Utakuta sisi tumekuwa tukiwachumia wengine na wetu sisi bado wanafanyakazi zile za chini kabisa za kufyagia na kubeba mizigo. Lakini kazi za fedha hasa, maana *chief cooker* mzuri hapa basi mshahara wake ni dola 2000 mpaka dola 3000 na meneja hapa wanaanzia na dola 1000 mpaka dola 5000 wa mahoteli, basi hao ndio wanaondoka na fedha na wanakwenda nazo nje ya nchi. Kwa hivyo, yale malengo ya kuweka utalii nchini kwetu hayakufanikiwa kwa sababu watu wetu hawapati ajira zile zenye malipo mazuri, ajira zilizokuwepo zote ni ndogo ndogo.

Kwa hivyo, naomba walimu wa chuo hiki hapa kwetu wapewe mafunzo, walimu wawe na ujuzi na waweze kusomesha ili tupate *product* nzuri zaidi. Vile vile kwa makusudi tupeleke vijana wetu waende wakasome angalau 40 au 50 ili wakifika hapa tuwalazimishe wawekezaji kwamba jamani muwaajiri hawa Wazanzibari wetu katika mahoteli yenu. Fedha nyingi wanaondoka nazo hao niliowataja na watu wetu hapa wanabaki na hali maskini na duni. Mshahara wa *chief cooker* mmoja wanachukua wafanyakazi wa kufyagia 30 hii inavunja moyo sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele na mchango wangu ambao huu ni wa mwisho, naomba univumilie nilikuwa na mengi lakini wakati ni mdogo. Katika ukurasa wa 19 kuna ripoti ya bodi ya mapato ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, bodi hii inafanya kazi zake vizuri hivi sasa na imeweza kudhibiti miinya mingi ya mapato na tukiangalia kwa kiasi kikubwa sana malengo yao yanakaribia kutimia.

Tatizo ambalo tunalo hapa wafanyabiashara ni kwamba tunazo taasisi mbili ambazo zinafanyakazi moja kuna *TRA* imekaa huku ikutoe roho na kule kuna *ZRB* ikumalize na hali hii kwa kweli inatusumbua sana *(Makofi)*.

Kwa sababu kule Tanzania Bara *TRA* moja inashughulika na *VAT* na Ushuru wa Forodha. Lakini hapa Ushuru wa Forodha unashughulikiwa na *TRA* na *VAT* pia inashughulikiwa na *TRA* pamoja na *ZRB*, sasa huku ukikatwa *VAT* hurejeshewi, yaani akichukua ndio amechukua. Hivyo sivyo inavyokwenda

kwani *VAT* inapochukuliwa inayo marejesho yake, wafanyabiashara wanahangaika sana.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri njia nyepesi ya tatizo hili ni kuondoa mmoja katika hawa. Kwa mfano, *TRA* ikafanyakazi zake Tanzania Bara na *ZRB* ibakie Zanzibar kwa ajili ya kufanyakazi zake hapa. Kwa sababu kazi ni moja na taasisi ni mbili, hii ina maana kwamba tunapoteza *resources* pamoja na wakati na kupelekea usumbufu kwa wafanyabiashara *(Makofi)*.

Kwa hivyo, naomba suala hili liangaliwe kwa umakini na kuona namna gani tunaweza kulifanyia kazi. Kwa kweli linasumbua, kubabaisha pamoja na kutuhangaisha na wala halileti tija yoyote katika Mfumo wa Uchumi Huria.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye ukurasa wa 21 tukianzia ukurasa wa 20 kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha. Kwa kweli mimi mwenyewe binafsi nimevunjika moyo sana, kwa sababu sote sisi tunategemea kwamba tume hii inafanyakazi zake. Wakati unapouliza swali basi unaambiwa aa! Tusubiri Tume ya Fedha.

Lakini tume hiyo haijafanya kazi yoyote na mwisho wa habari imeandikwa kwamba kutofahamika vizuri kwa tume pamoja na majukumu yake katika changamoto ukurasa wa 21. Mhe. Mwenyekiti, suala hili linavunja moyo sana na tume kama iko na hali hii basi bora ingevunjwa na tukapumzika. Kwa sababu tume haijafanyakazi na wala haina mwelekeo wa kufanyakazi, tena tukate tamaa kwamba tume hii itafanyakazi na kuleta mafanikio yoyote katika suala hili.

Kwa hivyo, jambo hili bado ni gumu sana na linafanywa kuwa gumu, kwa sababu ya kuwa tume hii ndio ingeweza kutatua matatizo haya, lakini tume imeshindwa. Kwa maana hiyo, itafutwe njia nyengine na ninaomba Baraza la Wawakilishi liingilie kati suala hili *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache sana katika kuchangia ripoti au kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Vile vile nikupongeze kwa kuweza kukimudu kiti vizuri na ninamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie, ili uendelee kudumu katika kiti hicho *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nataka nisema kwamba Mhe. Subeit Khamis Faki wakati alipokuwa akitoa mchango wake alieleza kilio cha

wananchi wa Micheweni na zaidi katika lile eneo ambalo wananchi walikuwa wakilima kilimo cha mpunga. Lakini kwa bahati mbaya kutokana na hali ya hewa pamoja na tabia ya nchi siku hizi inavyoitwa, kwamba maji ya bahari yamevamia katika maeneo ya wananchi wanayolima.

Kwa kweli kilio kile ni cha wananchi na kimsingi bado unaweza Mhe. Mwakilishi kuwashajiisha wananchi wako katika shehia hiyo inayohusika, ili tutakapoanza Miradi ya *TASAF III*, basi upo uwezekano mkubwa sana wa kupata fedha kupitia kwenye miradi ya hiyo. Lakini fedha hizo haziji tu, isipokuwa wananchi wenyewe wafuate ule utaratibu wa kawaida wa kujaza fomu kupitia kwa masheha na kuelezea ule mradi ambao wanaoutaka.

Kwa hiyo, fedha hizi kwa upande wetu sisi Afisi ya Waziri Kiongozo zitaweza kupatikana kupitia *TASAF* kutokana na mazingira. Kwa sababu fedha za *TASAF* zina maeneo tofauti, kama vile fedha za UKIMWI, walemavu, wajane na vile vile zipo fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira pamoja na suala zima la mambo ya uvuvi.

Kwa kuwa Wizara ya Fedha inayo mambo mengine, lakini zipo *channel* nyengine ambazo wananchi wenyewe wanaweza kukaa na kujipanga vizuri na kukubaliana, basi uwezekano wa kujenga tuta na kuweza kuzuia hayo maji ya bahari na suala hilo linawezekana sana.

Mhe. Mwenyekiti, sina maneno mengi, nadhani Mhe. Waziri ameandika mambo mengi na ameweza kujiandaa vizuri, isipokuwa nilikuwa nataka nimsaidie Mhe. Mwakilishi, kwa sababu Micheweni ni eneo moja ambalo hata serikali imeelekeza nguvu zake kwamba ni eneo maalum kwa ajili ya *Program* ya Kuondoa Umasikini. Kwa hivyo, bado maeneo yetu mbali mbali kupitia taasisi zetu za serikali tunaweza kushirikiana kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu hao, ili waweze kujiimarisha katika kilimo chao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, naipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kuweza kufanayakazi nzuri na kuangalia yale maeneo yenye mapungufu na pia Waheshimiwa Wajumbe kuweza kutukumbusha yale maeneo ambayo kama serikali tunahitaji kuyafanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwa kukupongeza kupata wadhifa huu na kutuonesha kwamba kweli wanawake mnaweza, hongera sana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza pongezi hizo naomba nimshukuru sana Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) pamoja na wajumbe wa kamati yake, kwa kazi kubwa kabisa waliyofanya kwa karibu sana na Wizara ya Fedha na Uchumi na kuweza kutupa miongozo mbali mbali, kutuelekeza, kutukosoa na hatimaye kukamilisha ripoti yetu hapa leo *(Makofi)*.

Kwa kweli nikipitia ripoti ya Mwenyekiti mengi sana ni ushauri, kwa sababu nimependa sana kwamba ametoa tatizo na baadaye ametushauri hasa, yaani ufumbuzi na hiyo ndio njia nzuri. Kwa sababu siku zote usiseme tatizo tu bila ya kushauri ufumbuzi au suluhisho. Lakini yeye amesema tatizo na sehemu nyingi sana ameonesha njia.

Kwa mfano, alipomalizia Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuhusu suala la Tume ya Pamoja, basi ametoa ushauri kwamba ingefaa sasa tukutane pamoja, yaani hii Kamati ya Fedha na Uchumi, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Tume ya Pamoja na Fedha.

Kwa hivyo, nadhani tukikutana tunaweza kupiga hatua na *challenges* hiyo tumeipata tokea kwenye kamati na tumeichukua, kwa kweli tutajitahidi kabla ya bajeti ikiwezekana basi tuweze kufanya kikao hicho cha pamoja *(Makofi)*.
Mhe. Mwenyekiti, *general issue* nyengine kubwa sana ya Mwenyekiti wa Kamati kuhusu suala la bajeti alisema kwamba *Other Charges* hazipatikani. Nafikiri sio kama hazipatikani labda ni kidogo Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu kwamba "Halikadhalika wizara zimekuwa zikilalamika sana kuhusu kuchelewa kwa matumizi mengineyo ya fedha, yaani *Other Charges"*.

Nazungumzia kuhusu suala la *ceiling* pamoja na linavyogaiwa kwenye mawizara na Mhe. Mwenyekiti ameelezea kwamba bajeti haitoshelezi kabisa mahitaji ya wizara, kwani bajeti imekuwa ikitolewa kutokana na ukomo wa bajeti.

Nafikiri haya ni mambo mawili tofauti kwanza tukubali kwamba mahitaji ya mawizara yanategemea na makusanyo na hilo ni jambo la msingi kabisa, tumeweka bajeti kwamba tutatumia kiwango hiki sawa, lakini itategemea tunakusanya kiasi gani. Kwa hivyo, hicho tunachokusanya ndio tunakaa kwenye *Ceiling Committee*.

Hiyo *Ceiling Committee* ni vyema kuipongeza kabisa Wizara ya Fedha na Uchumi au serikali kwa jumla kwa kuweka wazi kabisa, maana yake zamani labda anakaa mtu mmoja au wawili na kugawa yeye tu aa! Kutokana na *cash*

flow na mahitaji yenyewe ya mawizara wanaleta na halafu *Ceiling Committee* inakaa na kesi yetu jamani kwa mwezi huu tuliyoipata ni hii baada ya kutoa zile *first charge items* ambazo ni mishahara, mahospitali, bajeti ya maendeleo na sehemu nyengine, kinachobakia ndicho tunachogawana.

Kamati hii wajumbe wake ni hawa wafuatao:-

1. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Uchumi	-	Mwenyekiti,
2. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira,	-	Mjumbe mmoja,
3. Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji	-	Mjumbe mmoja,
4. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	-	Mjumbe mmoja,
5. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi	-	Mjumbe mmoja,
6. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	-	Mjumbe mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hao ndio *component members* wa *Ceiling Committee*. Sasa wao ndio wanaokaa na kuchambua mahitaji yaliyokuja serikali kwa mwezi ule ni yepi na tulichokipata ni hiki, kwa hiyo wanakigawa. Kwa hivyo, lazima tukubali na tungependa sisi bajeti itekelezeke kwa asilimia mia moja.

Nadhani ndio maana tunapopanga bajeti tunatoa mtiririko mzima wa matarajio ya makusanyo pamoja na matumizi na tunasema iwe asilimia mia moja na ile sana kimahesabu. Lakini hali halisi ilivyo si hivyo kwamba tunachokichuma ni kidogo kwa ajili ya mahitaji yetu na tatizo linakuwa hapo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoshauri ni kwamba sote tujitahidi kukaza mikanda yetu, tuzidi kuhamasisha walipakodi walipe vizuri na sisi Wizara ya Fedha na Uchumi tunajitahidi kudhibiti matumizi na kilichoingia tukitumie vizuri. Hizo ndizo *Access za Financial Management* kwamba tunachokichuma tunakidhibiti, ili tukitumie vizuri, pia tuhamasishe uzalishaji zaidi.

Kwa kweli tunashukuru sana nafikiri sote tuna-*acknowledge* juhudi za *Revenue Generation* zinavyotoka kutoka *ZRB* na *TRA*. Kwa mfano, mwezi wa Januari pamoja na matatizo ya umeme Mhe. Mwenyekiti tumekwenda *record* na *click* 9 billion na ajabu tulikuwa kizani.

Lakini nafikiri hicho kiza kwa sababu ya uingizaji mwingi wa mafuta basi *Alhamdulillah Petroleum Levy* imekwanda mpaka 2 *billion*. Sasa hii inaonesha kwamba hali yetu ya makusanyo ni mazuri na tunadhibiti, kwa sababu zamani tulikuwa tunakusanya, lakini hatudhibiti *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba tunayo matumizi makubwa sana hasa kwenye miradi ya maendeleo, kwenye bajeti naomba ninukuu nadhani tunakumbuka sote kwamba tulitoa changamoto na kusema bajeti ya mwaka huu

itaitwa “Bajeti ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Kuimarisha Kilimo na Utalii”. Vile vile tulisema kwamba tuna-*allocate* asilimia 58.1 ya matumizi yote kwenda kwenye maendeleo na hii ni asilimia kubwa sana.

Kwa hivyo, matumizi ya bajeti lazima tuyaridhie kwa sababu tusipotoa basi na hawa wafadhili wetu hawatoi na miradi mingi sana wanategea, maana yake wana-*calculate* mpaka *percentage* umetoa kiasi gani, haidhuru wanasema wewe nakuachia 5 *percentage*. Sasa katika ile 5 *percentage* anai-*calculate* umetoa ngapi kwenye ile na halafu ndipo atoe chake. Kwa kweli siku hizi hatulali wala hatusinzii kwenye miradi ya maendeleo, tena sisi tunatoa mapema zaidi kuliko hao wahisani *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, lakupongezwa tunaona miradi kama vile Uwanja wa Ndege, barabara Pemba, Ujenzi wa Baraza la Wawakilishi umekwenda vizuri sana kwa sababu mchango wetu wa serikali ni mzuri sana tena wa kupigiwa mfano *(Makofi)*.

Hoja nyengine kubwa ilikuwa kwenye suala zima ambalo alizungumza Mhe. Ali Suleiman Ali kuhusu bei za bidhaa muhimu kwa nini huko nje zinapandishwa mara kwa mara na wala hazikamatiki kama vile sukari sasa kilo moja ni shilingi 1,500/-.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni kweli na kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, yaani tuna-*monitor* hali iko vipi na halafu tuna-*review* hali ya bei, ili kumpungumzia mzigo mwananchi wetu. Suala hili si kwa sukari tu, isipokuwa kwa unga wa ngano na mchele, yaani hivi vitu vitatu tunakwenda navyo serikali na mara kwa mara tunavi-*monitor*, ili kuona kwamba watu wetu hawapati shida.

Lakini kuna matatizo makubwa sana ya wafanyabiashara na lazima tukubali kwamba wafanyabiashara wetu wanataka ku-*maximize profit*. Masuala ya kupita madukani na kuangalia na kusema weka bei hii, nadhani tusirudi nyuma. Isipokuwa hivi sasa tunakwenda kwa siasa na wao wafanyabiashara tunakaa nao, tunawaelimisha na *penalty* zipo lakini hatujafikia huko.

Mhe. Mwenyekiti, tukichukulia zile kodi zilizopo za bidhaa, kwa mfano kama vile mchele tungetakiwa tu-*comply* na *East Africa Community standard* waliyoweka, basi tulipe kodi kwa asilimia 75. Lakini sisi Zanzibar tumejiwekea tulipe asilimia 25 kwa mchele, bado tumeipunguza hiyo asilimia 25 na tunalipa 12.5.
Sasa kwa nini kipolo kiwe shilingi 40,000/- au 50,000/- kwa mfano. Isipokuwa naamini tukiitoa hii asilimia 50 tuliyoitoa hapa na kuifanya 25 nadhani kipolo

kitafika shilingi 60,000/- mpaka 70,000/- na mtu wetu hataweza kumudu hata kidogo.

Kwa hivyo, ninachosema kwamba sisi bado hasa mchele na tunazidi kupunguza na tunagombana na wenzetu na kusema kwamba mchele unavuka na wenu rahisi unakwenda huko na tunawaambia na nyinyi sembe kwenu mnafanya hayo hayo, yaani mahindi mnatoa *subsidies*, Kenya wanatoa *subsidies*, sukari wanaachia *Zero Tariff*. Kwa kweli kila mmoja anaangalia *stability* ya nchi yake, sisi tunayafanya haya kwa kuona *stability* ya nchi yetu na haidhuru tunajua tunakosa *revenue*, lakini je wananchi wetu wawe na njaa na itakuwa hakuna siasa tena na tutakuwa hatarini.

Mhe. Mwenyekiti, *equal* ni unga wa ngano kwa kodi za *East Africa Community* ni asilimia 60, lakini tuna-*operate* kwa asilimia 25. Sukari iliyozungumzwa kilo moja shilingi 1,500/-. Hivi sasa bei ya sukari huko nje imepanda sana mara dufu kabisa, yaani hainunuliki na wala sikumbuki bei vizuri. Lakini wafanyabiashara wenyewe wametu-*approach* na kutuambia jamani tunaomba mtupunguzie kodi kama si hivyo itakuwa haiuziki na mtatulaumu.

Kwa hivyo, tumelizingatia ombi na tumekubali na sukari tumeipunguza kodi kwa asilimia 50 badala ya kuwa asilimia 25, basi iwe asilimia 12.5 angalau kwa miezi mitatu tuone mpaka mavuno yatakapokuwa tayari labda kwenye mwezi wa Mei, Juni au Julai.

Kwa sababu *fluctuation* za bei zinategemea masoko ya nje, kwani huko nje nako haipatikani. Sasa hili ni suala la msingi na lazima tulizingatie kama wakati ule tulipokuwa na matatizo ya mchele, basi hizi *agricultural commodities* zina-*fluctuate* na matatizo ya hali ya hewa pamoja na mengine mengi.

Kutokana na hali hii ni jukumu lao kwa upande wa wafanyabiashara hii shufaa tunayoitoa serikali basi na wao waipokee kwa ajili ya kutusaidia. Lakini ile mikono inakuwa mingi, pengine mfanyabiashara mkubwa atatoa shufaa na yule mdogo mpaka inamfikia mlaji ndio inaangakia kilo shilingi 1,500/-.

Nadhani Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa upande wake tena anacho Kitengo cha Kumlinda Mlaji wanajitahidi kuona kwamba wafanyabiashara hawaendi ku-*maximize profit* na haidhuru kuna *other charges* nyengine *overhead cost*, ambazo pengine nauli kuitoa hapa na kupeleka Kibeni, Nungwi, Fumba ama Mkoani, basi na yeye anataka atie chochote japo kwa gari la ng'ombe apate kitu, lakini asizidi mpaka tena kila mmoja akalia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nakuomba umalizie.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante namalizia kwa hili alilomalizia Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwamba Zanzibar hatuna *Investment Policy* kwenye viwanda, mimi nasema si kweli na mwenyewe Mhe. Waziri yupo na atakuja, lakini nasema sikweli.

Kwa kweli tumetoa hapa *incentives* nyingi sana kwa wenye viwanda kuwekeza tumetenga maeneo huru Micheweni, Fumba na tumemwambia mtu aje awekeze na *cost* zote za kuwekeza, kwa mfano kuagiza malighafi tutamuachia bure na miaka mitano tutakuja kumpa *tax holidays*, yaani yote hayo tumeweka.

Lakini wenyewe tu tunajua mambo ya biashara wanaona haii halisi na biashara hiyo, wanaona bora viwanda hivyo wengine walioweka hapa wakavihamisha wakavipeleka Dar-es-Salaam. Sasa haya zaidi ni mambo ya biashara na wala sio kama hatuna *Investment Policy* kwenye Viwanda, tunayo ambayo ni mzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa pia alizungumza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwamba vijana wetu hawana uwezo, chuo kidogo na wala hakifundishi vizuri. Suala hili si kweli, kwa sababu chuo kinafundisha *very high standard* ya *qualification* za wanafunzi kwenye *Doha International Hotel*, yaani *Five Stars Hotel* tumewakuta Wazanzibari watatu na sisi wala hatukuwajua tunazungumza Lugha ya Kiswahili na huku tunapita, tukaambiwa *Assallam Allaykum* wazee.

Ah! tulishangaa nani huyu, tukasema huku tuko Qatar labda wako Waswahili, walituambia sisi ni fulani na fulani na tumesoma Chuo cha Utalii Zanzibar. Tuliwauuliza mme-*apply* vipi, walisema tumekwenda kwenye *Internet* tu tumekuta *Doha International Hotel* wanatangaza nafasi ya kazi, basi tume-*apply* tumepata, wengine *Service Manager* na ndio hawa wa kawaida tu.

Lakini sisi tunalo tatizo la kuwadharau watu wetu pamoja na chuo chetu, yaani tunakidharau na kuona ah! Na kuwapa *priority* mgeni Mtaliana na kumuacha Mzanzibari ambaye mwenye ujuzi mzuri yupo tu. Sasa hilo wafanyabiashara na kwa bahati nzuri Mhe. Mjumbe naye ni mfanyabiashara kwa hiyo nadhani angelichukua hili kwa ajili ya kutusaidia na wengine kuweza kufahamu suala hili. Nafikiri ni jambo la msingi kabisa kwamba hawa tunaowadharau huko nje wanaitangaza Zanzibar na kweli wanatusaidia na wenyewe wanapata riziki zao.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna yale ambayo nilitakiwa kutoa ufafanuzi, lakini Mhe. Waziri wa

Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi amenisaidia, hata hivyo nitajitahidi kugusa hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kuhusu suala la bei za bidhaa. Kwa kweli wizara inajitahidi ku-*maintain* bei za bidhaa na tumekuwa tukijitahidi kuweka *stability* ya bei. Kwa sababu hivi sasa tunaweza kwenda kwa mwananchi wa kawaida na kukwambia bei ya sukari ni shilingi 1,200/- tukiacha kipindi hiki ambapo sukari imepanda kutokana na sababu ambazo nitazieleza. Bei ya unga wa ngano ni shilingi 900/- mpaka 1,000/- bei ya mchele anaweza kukuambia. Kwa maana hiyo, bei hizi tumekwenda nazo kwa kipindi cha miaka miwili mpaka miwili na nusu.

Sasa tunachokifanya ni kujitahidi ku-*balance cost* ya mfanyabiashara, ushuru tunaomtoza, ili mwananchi aweze kununua katika bei ile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sukari imepanda karibu mara mbili, sababu ni kwamba tumeambiwa kunakozalishwa sukari maeneo mengine kulikuwa na *earthquake*, lakini hali mbaya katika maeneo mengine ambako sukari inazalishwa. Kwa hivyo, sukari kuanzia mwezi wa Januari imepanda na itaanza kushuka kutokana na *Lager* la Biashara za Kimataifa, sukari itaanza kushuka mwezi wa Mei.

Mpaka mwezi Disemba tulikuwa tunanunua sukari kwa dola 350 za Kimarekani kwa tani, lakini kuanzia Januari sukari imekuwa ikiuzwa dola 745 kwa tani na ndio maana kuna hiyo *shootup*. Hata hivyo, jitihada tumezichukua na tumeweza kupunguza ushuru wa sukari kufikia nusu na mategemeo yetu kwamba mzigo utaoingia hivi sasa utakuwa unauzwa kwa bei ya kawaida 1,200/-.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mapato yanayotokana na utalii Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi anaeleza vizuri, kwa sababu wizara yangu ni muandaaji tu, mpikaji na mpakuaji anakuwa mwengine. Kwa hiyo, hili siwezi kusema yanakusanywa kiasi gani, kwani si kamisheni wala wizara inayoindia katika ukusanyaji wa mapato *(Makofi)*.

Vile vile kuna suala la viwanda. Katika hili labda niseme kwamba serikali imejitahidi kuweka sera na hiyo ndiyo kazi yake, yaani kuweka Sera ya Maendeleo ya Viwanda. Lakini hapo hapo tukaweka Sera ya Viwanda Vidogo Vidogo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuweka sera hizi tumejitahidi sana kuzungumza na *Private Sectors*, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa ufahamu wa zile sera

ambazo tumeziweka. Pamoja na hayo ziara za nje zimefanyika baina yetu na *Private Sectors* na tukienda kule tunakutana na wafanyabiashara wengine na tunakaa, kwa ajili ya kujadiliana na kukubaliana.

Sasa kinachojitokeza ni kwamba wafanyabiashara wa nje wanasema wako tayari kuwekeza katika viwanda, lakini wawe na mashirikiano na wafanyabiashara wa ndani. Kwa kweli katika kuhamasisha wafanyabiashara wa ndani ni wachache sana waliojitokeza kuwekeza katika viwanda, hawa nao kuna *factors* ambazo zimewafelisha. Kwa hivyo, serikali inalijua hilo na tunalifanyiakazi vizuri.

Vile vile kuhusu suala la maabara. Mhe. Mwenyekiti, suala hili limekuwa likipigiwa kelele tokea bajeti ya mwaka juzi kama sikosei na Mhe. Najma Khalfan Juma alilishikilia sana. Kwa kweli tumeshafanya mazungumzo na *Tanzania Bureau of Standard* waweke Tawi hapa. Lakini maagizo tuliyopata ndani ya Baraza hatutakiwi kuwa na *Tanzania Bureau of Standard* bali *Zanzibar Bureau of Standard*.

Sasa kuwa na *Zanzibar Bureau of Standard* kunahitaji kazi, kwanza tuwe na fedha za kutosha baina yetu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wenye maabara, kwa ajili ya kuikuza maabara yetu na kufikia kiwango kinachotakiwa.

Kwa upande wa trainning tayari tumeshasomesha watu ndani ya Kitengo cha Kumlinda Mtumiaji na tunakwamwisha na suala la maabara, vitendeakazi ndani ya maabara na kuiweka maabara kwenye *standard* inayotakiwa. Lakini kwa upande wetu tayari tumeshalifanyiakazi.

Maonesho ya Biashara ni kweli kwamba tukiacha yale maonesho ya Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pamoja na mimi tulishiriki kikamilifu kama Babeninayaweza na Mameninayaweza basi hakuna maonesho mengine ambayo yamefanyika. Hata hivyo, jitihada zinafanywa za kurejesha maonesho Zanzibar.

Hivi sasa tunalo eneo la ukubwa wa *square* kilomita moja katika eneo la Fumba, ambalo tumelitenga maalum kwa ajili ya kujenga eneo la Maonesho ya Biashara. Kazi hii tunaifanya sisi, *Commonwealth* pamoja na *World Bank*. Sasa *Commonwealth* watatusaidia kufanya *setup* na *World Bank* baadaye watakuja tukikubaliana na Wizara ya Fedha na Uchumi kupata mkopo wa kujenga hilo eneo.

Kwa hivyo, kazi hii tunaifanya na tunachokifanya hivi sasa ni kulihifadhi hilo eneo, ili kuepusha kuvamiwa na watu na baadaye kupata matatizo ya kuja kulipa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Kamati ya Leseni lini itakuwa tayari. Hivi sasa bado sijaweza kusema ni lini kutokana na hali halisi, isipokuwa nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kazi inafanyika na hofu itaondoka si muda mrefu, kwa sababu hata sisi linatukera.

Kwa mfano, unapita Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji ambapo Kamisheni ya Utalii inakusanya, Manispaa inakusanya, Halmashauri inakusanya na inakuwa ni kero kwa wafanyabiashara wetu. Kwa hivyo, hata sisi linatukera na ndio maana tunalifanyia kazi.

Vile vile kuhusu Shirika la *ZSTC* kama ninavyosema mara zote *reforms* zake zinaendelea, sisi wizara tumeshafikia hatua ya ku-*identify* wafanyakazi wepi wabakie na wengine waondoke. Kwa hiyo, nadhani kinachokwaza ambacho chini ya kitengo cha mabadiliko ya sera ya kiuchumi nadhani ni mambo ya fedha kumalizia hiyo kazi, lakini kwetu sisi tayari tumeshafanya hiyo kazi.

Mtandao wa *ZIPA* kama haikuwekwa kwenye ripoti ya kamati nataka niseme tu kwamba *ZIPA* wana mtandao tena uko *active* kweli kwa sababu kazi zote za *ZIPA* zinapitia katika mtandao ule. Tuliwahi kuwa na kesi katika Mahakama ya Kimataifa lakini *communication* zetu zote zilikuwa zinakwenda *through* mtandao wa *ZIPA* ku-*submit* ripoti zetu na mambo yote mpaka tumeshinda ile kesi. Kwa hivyo, mtandao upo na unafanya kazi vizuri.

Jamani Chuo cha Maendeleo ya Utalii kufufua si kitu rahisi. Chuo hiki kina changamoto nyingi kama zilivyooneshwa ndani ya ripoti hii. Lakini pamoja na changamoto hizo kimekuwa kikitoa *product* tena nzuri tu. Kama alivyosema waziri yeye amewakuta Qatar wafanyakazi katika hoteli ambao wamesoma Zanzibar. Mimi nimekwenda Afrika ya Kusini nimekuta watatu vile vile na maeneo mengi ukenda unawakuta. Hapa Bara kila hoteli unayoingia utasikia mheshimiwa chechei, mheshimiwa habari za nyumbani, wewe nani? Mimi Mzanzibari nilisoma chuoni lakini ndio nimepata kazi huku.

Lakini la karibuni chuo kimeweza kutoa *bench* mbili za diploma na tulikuwa tuna mpango *bench* ya kwanza kuipanga wawe ma-*PO* wa mahoteli ili kurekebisha hali ya ajira. Lakini wakati mwengine tuna-*locate* zile hoteli *bench* nzima imeshachukuliwa tukabakiwa na watatu ndio walikuwa hawana ajira. Sasa hivi tuna kundi jengine la diploma ambalo wamemaliza wata-*graduate* kesho kutwa tunawapangia *graduation* yao. Hawa nao tayari tumeshawafanyia *location,* sasa sijui wakati wa *location* kama tutawapata wote au wengi watakuwa wameshachukuliwa.

Kwa kweli *product* zinatoka lakini zikitoka tu huwa zinachukuliwa ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar. Kwa hivyo, si chuo ambacho labda kinazalisha 1000 kwa mwaka, diploma wanatoka 15 -18. Kwa hivyo wakitoka tu wanachukuliwa lakini mwanzo wa safari ni hatua moja, kwa hiyo tunakwenda na chuo kinabadilika. Kubwa zaidi ni kwamba serikali imea-*locate* pesa ambayo tulipata msaada wa Iran kama 1 billion *Tanzania shillings.* Pesa hiyo yote ikipatikana inakwenda chuoni. Tunachofanya sasa hivi sisi pamoja na Idara ya Upimaji ni kupima *site* ya chuo na kuwa-*locate* wapi kuingia nini.

Pia tunachofanya ni kupata ule mfumo mzima na michoro yote tui-*submit* kwa wale wanaotoa pesa na baadae tuwasikilize wanatwambia nini, kwa sababu siku hizi mwenye pesa yake atakupangia na *contractor* mpe huyu lakini pesa hii hapa. Mhe. Mwenyekiti, sisi hatujali nani atajenga chuo, tunachotaka ni chuo. Kwa hivyo, kazi tunafanya lakini hatua zetu ni fupi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kujaribu kutoa ufafanuzi wa hapa na pale kutokana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao yote ambayo ni mizuri na yote ilikuwa ni kujenga au kutupa changamoto wizara yetu ili tufanye vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla tumezipokea changamoto hizo na kama desturi yetu tutajitahidi kadri ya uwezo wetu ikitegemea na uwezo wa serikali kutuwezesha, lengo letu kubwa sana ni kuanzisha au kuleta maendeleo ya kilimo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla nakubali kwamba pengine hatujafikia hasa ile asilimia iliyokusudiwa ya maendeleo ya kilimo hapa Zanzibar, lakini naweza kusema kwamba tuchukue kiasi miaka 10 iliyopita na ukilinganisha na leo kwa ujumla kilimo kimepiga hatua kubwa sana juu ya umaskini wetu. Lakini tunaipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa juhudi zake juu ya upungufu wa raslimali lakini tunajitahidi sana kutusaidia na kila mwaka wanajaribu kuongeza asilimia fulani ya fedha katika kilimo.

Kwa hivyo, kwa ujumla napenda kuwahakikishia wajumbe kwamba kilimo kinaendelea vizuri sana. Kwa mfano, mabonde yaliyokuwa hayalimwi miaka mitatu mpaka minne nyuma sasa hivi yanalimwa. Kwa ujumla mabonde yetu ya mpunga kwa sasa hivi yanalimwa zaidi ya asilimia 90 na ushahidi kamili kuna bonde kubwa sana la Cheju, safari hii wenyewe wale wakulima wanasema sijui vipi wamefikia kiwango kile. Kwa hivyo, kwa ujumla nilikusudia kusema kwamba tunakubali kwamba bado hatujafikia hatua hiyo tunaikusudia lakini

tukubali kwamba hatua zinachukuliwa na maendeleo makubwa sana yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo yale yote mimi nasema ni changamoto, tumeyapokea na kwa kweli mimi nikiondoka hapa kama ni waziri dhamana wa wizara hii, mimi mwenyewe nitakwenda kuyaandika vizuri haya yote na baadae kukaa na watendaji wangu kila mmoja kwa idara yake kuweza kumpa kipande chake ili aweze kutekeleza, na sisi kama wasimamizi wa maendeleo tutakuwa tunafuatilia na kusimamia utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, labda nichukue mfano mmoja niseme hapa kabla sijaendelea kujaribu kujibu hapa na pale. Mhe. Mwenyekiti, tunapiga kelele juu ya suala la malalamiko kuhusu Micheweni, Micheweni napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba serikali yenyewe imeamua kwa makusudi kuipa kipaumbele katika hali zetu, katika njia ya kilimo, mifugo na kadhalika.

Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi Mhe. Subeit Khamis Faki hilo alitambue kuwa serikali yenyewe imelitambua hilo na dalili zipo. Juzi mimi nimekwenda kutembelea kule, nimeona maendeleo, mradi wa *PEDEP* upo na *TASAF* ipo, tunasaidia sana na tutaendelea kusaidia. Kwa ufupi ni kwamba Micheweni tunajaribu kuipa *priority* tukitegemea keki ambayo tutaipata. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo aliyotoa kwamba tutizame uwezekano wa kilimo cha mbadala katika mawe yaliyokuwepo, hilo ndio lengo letu kwa upande wa Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, jibu langu katika hoja zilizotolewa au michango iliyotolewa hoja yangu ni kwamba tumeyapokea na tutayanukuu vizuri halafu tutayafanyia kazi moja kwa moja. Isipokuwa labda baadhi ya mambo kwa mfano karakana yetu imepigiwa kelele sana kwamba karakana ni nzuri na mimi nakubali hivyo, *machine* zake ni nzuri. Lakini tatizo wanasema wajumbe wanasema haitambulikani kama ni idara au shirika. Napenda kusema kwamba sisi wenyewe hatuna matatizo, tatizo ni kwamba kwa sababu suala la ufundi tunao mafundi wazuri sana na matrekta yanatengenezwa ingekuwa kama hayatengenezwi tusingeona yakitembea katika mashamba.

Lakini wakati mwengine inakuwa tunachelewa kwa sababu ya kupata *spares* na Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi tumezungumza nao na tumekubaliana kwamba watupatie pesa tuweze kununua *spares* kabla ya msimu, na shahidi huyu atasema kwamba wamekubali kutupatia fedha hizo kila mwaka kabla ya kuanza msimu basi watatuongeza pesa. Kwa ufupi nakusudia kusema kwamba matrekta yapo na malengo ya kuongeza matrekta na serikali yenyewe ndio iliyoamua kwa makusudi kuongeza matrekta na hivi karibuni tutapata matrekta zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, umwagiliaji maji kama nilivyosema mara zote katika bajeti yetu kwamba tumekubaliana kuwa kwa ujumla uimarishaji wa kilimo serikali yenyewe imeunda kamati kupitia katika mpango wake mkuu, imeunda kamati ndogo ya kukaa na kusaidia na wizara yangu kutazama kila maeneo vipi tutaweza kuimarisha kilimo. Kamati hiyo imeshafanya kazi yake na imetoa ripoti yake na ripoti imepita serikalini na imejadiliwa la msingi ni kwamba imekubalika.

Mhe. Mwenyekiti, kamati hiyo mshauri wake ni Mhe. Waziri Kiongozi na namshukuru kwamba kila baada ya muda fulani hivi karibuni ameshataka tukutane ili tuweze kufanya tathmini hatua gani zimefikiwa tangu kamati ile imeundwa na kuna matatizo gani. Hivi karibuni kamati hiyo itaitwa na tunao baadhi ya wajumbe ambao ni Wakuu wa Mikoa wote wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo umwagiliaji maji ni moja katika lengo kuu la serikali. Tumesema mara nyingi kwamba lengo letu la wizara yetu na serikali ni kuwa tumeona kilimo kuwa ni mali, kwa hivyo tunafanya kila njia tunayoiweza kuhakikisha kwamba mabonde yetu yote ya Unguja na Pemba hatimae yanakuwa ya umwagiliaji. Kwa sababu hatuwezi kutegemea mvua hasa wakati tulionao huu ili kutokana na hii *clement change* ya dunia kwani mvua sasa hivi hazitabiriki. Kwa hivyo, uamuzi tulioamua kwamba twende katika umwagiliaji katika mabonde yetu yote. Napenda kuwahakikishia wajumbe kwamba wafadhili wengi tumeshakutana nao na wengi wameonesha nia ya kuweza kusaidia. Kwa mfano, siku ya Ijumaa nina miadi na Waturuki kuhusu suala la kilimo vipi wataweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla nawaomba wajumbe wakubali michango yao tumeipokea na tutaifanyia kazi ipasavyo. Kwa haya machache nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nifanye majumuisho kwa muda mfupi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii ni kidogo lakini kutokana na muda wameweza kuchangia wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia ni sita nao ni:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali.
2. Mhe. Said Ali Mbarouk.
3. Mhe. Ame Mati Wadi.
4. Mhe. Suleiman Hemed Khamis.
5. Mhe. Subeit Khamis Faki
6. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa michango yao waliyoitoa.

Mhe. Mwenyekiti, pili niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri waliotoa ufafanuzi mbali mbali ambao naamini umesaidia sana katika kufafanua mambo mbali mbali ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Moja tu ambalo ningemshauri Waziri wa Fedha pale aliponitajia Wajumbe wa Kamati ya *Steering Committee*, kuna Katibu mmoja ambaye ni muhimu sana hakuweza kumtaja sijui amemsahau au sio mjumbe, naye ni Katibu Mkuu Afisi ya Waziri Kiongozi ambaye kwa kweli kwa mujibu wa taratibu afisi hii ndio inayosimamia masuala ya shughuli zote za serikali. Kwa hivyo, kama hayupo kwenye *committee* hiyo ningemshauri basi na yeye awemo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ni suala la Mhe. Ame Mati Wadi ambaye wakati wa uchangiaji wake alizungumzia juu ya suala la ripoti ya Idara ya Misitu ambayo haikumtosheleza na ni idara ambayo ina eneo pana.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kamati yetu huwa inaripoti pale ambapo inapopata nafasi ya kufanyia kazi, katika wizara hii sehemu ambayo tulipata nafasi ya kwenda Wizara ya Kilimo ni eneo hili la misitu na nyuki na ndio maana utakuta ripoti yetu imeelezea suala hili tu. Kama ripoti yangu ilivyoeleza mwanzo kwamba kamati hizi huwa hazipati muda wa kutosha wa kutembelea maeneo mbali mbali katika taasisi mbali mbali. Kwa hivyo, ndio maana utakuta ripoti yetu imeelezea suala dogo tu ambalo sisi wenyewe *physical* tumepata nafasi ya kwenda. Kwa hivyo, sio maana ya kwamba hatukuweza kutoa taarifa kamili, ni eneo ambalo tulipata kutembelea katika idara hii peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoikubali ripoti hii wanyanyue mikono, wasiokubali. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo hii, kwa madhumuni ya kujadili mambo mbali mbali yenye maslahi mema na ustawi mzuri kwa nchi yetu na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru mno kwa kunipa nafasi hii muhimu na adhimu ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu mukhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika tunaendelea kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuzifanya na hatimae kuzikamilisha shughuli za kamati yetu kwa mafanikio makubwa. Ni jambo la kujivunia sana kwamba tumeweza kufanya shughuli za kamati kwa muda wa wiki sita ikiwa ni wiki mbili mbili kabla ya kila kikao cha Baraza bila ya vikwazo au matatizo yoyote makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika muda wote wa shughuli za kamati, wajumbe takriban wote waliweza kuhudhuria na kushiriki kazi za kamati kwa ukamilifu. Kwa hakika hii ilikuwa ni miongoni mwa neema kubwa katika neema za Mwenyezi Mungu. Vyenginevyo lau angelitaka Mwenyezi Mungu kungeweza kutokea mtihani au kikwazo cha aina yoyote na kuzuwia ufanisi wa kazi za kamati. Lakini mambo yalikwenda vizuri kiasi cha kuiwezesha kamati yetu kupata mafanikio makubwa, *alhamdulilah*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika neema za Mwenyezi Mungu ni nyingi na hazina mipaka. Kwa neema zake *Subuhanaahu Wataala*, kila kitu kilikwenda vyema zaidi ya matarajio. Kila ambalo lingekuwa gumu lililainika, yaliyo mazito yakawa mepesi, masafa marefu yakafupika, na kila kitu takriban kilikwenda vizuri hadi kamati ikakamilisha majukumu yake ya kikatiba na kikanuni kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea, naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako tukufu, muhtasari wa taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu utekelezaji wa shughuli za wizara nne za serikali ambazo ziko chini ya usimamizi wa jumla wa kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, kamati yetu imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(d) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2009. Majukumu na kazi za kamati hii yameainishwa katika Kanuni ya 110 ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo, pamoja na mambo mengine, kamati ina majukumu ya msingi yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na kamati hii katika mwaka uliopita.
b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya wizara zinazosimamiwa na kamati hii.

c) Kufuatilia mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi iliyo chini ya wizara zinazosimamiwa na kamati hii.

Mhe Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kiujumla imepewa jukumu la kuzisimamia wizara nne za serikali ambazo ni:-

i. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
ii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
iii. Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

iv. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe Mwenyekiti, kamati yetu ina wajumbe kumi na moja na makatibu wawili. Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Mzee Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Mjumbe
5.	Mhe. Haji Faki Shaali	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Haji Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Mjumbe
8.	Mhe. Mohamed Ali Salim	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	Mjumbe
10.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	Mjumbe
11.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
12.	Ndg. Salmin Amour Abdallah	Katibu
13.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu

Mhe Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita baina ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Kamati ilianza kutekeleza shughuli zake Kisiwani Pemba kwa muda wa siku 12, kuanzia tarehe 07/09/09 hadi 18/09/09.

Aidha, kamati iliendelea na utekelezaji wa kazi zake Unguja kwa awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza ilifanya kazi kwa muda wa siku 14, kuanzia tarehe 10 hadi tarehe 23 Disemba 2009 na katika awamu ya pili, kamati ilitekeza shughuli zake Unguja kwa muda wa siku 5 kutoka tarehe 08/03/2010 hadi tarehe 12/03/2010. Halikadhalika, kamati iliweza kwenda Tanzania Bara na kufanya shughuli zake huko kwa muda wa siku 5, kuanzia tarehe 01/03/2010 hadi tarehe 05/3/2010.

Mhe Mwenyekiti, kamati yetu kimsingi imeridhika na utendaji wa wizara zote 4 zilizotembelewa na kamati. Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wa wizara zote kwa juhudi kubwa wanayoichukua kutekeleza majukumu yao, licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo. Baada ya shukurani za jumla za kamati kwa wizara zote sasa napenda nizungumzie wizara moja moja kati ya wizara zilizotembelewa na kamati huku nikigusia mafanikio, changamoto na maoni ya kamati.

Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo

Mhe Mwenyekiti, natumai sote tunaelewa na kufahamu kwa kina umuhimu uliopo kwa wizara hii na vitengo vyake. Kamati inazipongeza Sauti ya Tanzania Zanzibar, Televisheni Zanzibar na Gazeti la Zanzibar Leo kwa kuendelea kutoa huduma zao katika kipindi kigumu cha nchi kukosa umeme. Kamati inafahamu fika kuwa, idara hizi zilifanya kazi ya ziada na pengine katika mazingira magumu ya kuendelea kutowa huduma hali ya kuwa nchi haina umeme.

Mhe Mwenyekiti, kifungu cha 18(2) cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza kuwa kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali, nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii. Kwa kuwa Idara ya Televisheni, Redio na Gazati la Zanzibar Leo wameweza kutekeleza wajibu wao huu wa kikatiba licha ya ukosefu wa umeme ulioikumba nchi, kamati inawapongeza sana kwa uzalendo wao na inawaomba waendelee na moyo wao wa kuitumikia nchi kwa moyo mkunjufu.

Mhe Mwenyekiti, kamati imeridhishwa mno na ujenzi wa academia ya michezo huko Dole ambayo inatarajiwa kumalizika na kufunguliwa mwishoni mwa mwaka huu wa 2010. Hata hivyo, kamati inashauri kuwa watoto wenye vipaji maalumu na wenye uwezo mkubwa ndio wapewe kipaumbele kujiunga na chuo hicho cha *academic* ya michezo ili kukuza vipaji vyao.

Mhe Mwenyekiti, kamati imeshangazwa kukuta wanafunzi wa Chuo cha Habari hawafahamu hata mambo ya msingi yaliyomo katika Katiba ya Zanzibar. Ili kurekebisha dosari hii, kamati imeshauri kuwa chuo hicho kianze kufundisha masomo ya *Media Law* na *Constitutional Law* kwa lengo la kuongeza ufahamu wa wanafunzi wa chuo hicho kuhusu mambo ya Katiba.

Aidha, kwa kuwa Chuo Cha Uandishi wa Habari kinakabiliwa na ukosefu mkubwa wa nyenzo za kufanyia kazi, kamati inaiomba wizara kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa chuo kinapata nyenzo hizo hasa *machine* ya *photocopy*, *computer* zilizounganishwa na mtandao wa *internet*, na vitabu vya

kutosha na vya kisasa kwa ajili ya maktaba ya chuo. Upatikanaji wa nyenzo hizo utaimarisha kwa kiasi kikubwa mazingira bora ya utolewaji elimu katika chuo hicho.

Mhe Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ni muhimu sana katika kufikia maendeleo endelevu. Kwa mantiki hiyo, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, kwa kushirikiana na Serikali ya Watu wa China, imefanya matengenezo makubwa ya Uwanja wa Amaan ili kwenda sambamba na maendeleo ya michezo tuliyoyafikia. Kamati kwa upande wake, ilikagua ujenzi huo na kupata maelekezo kutoka kwa wataalamu.

Sanjari na hilo, uwanja wa Gombani nao umefanyiwa matengenozo na kwa hivi sasa, Wizara inaendelea na mipango ya kuweka nyasi bandia kiwanjani hapo.

Mhe Mwenyekiti, kwa upande wa ziara ya kikazi huko Dar-es-Salaam, kamati ilipata fursa ya kutembelea vitou vya *TBC* radio na televisheni na kujionea hatua kubwa iliyofikiwa katika kubadilisha mfumo wa habari ambapo kwa mwaka huu wa 2010, *TBC* tayari zimeshaingia katika mfumo wa *digital* na hivyo kuvuka lengo la kimataifa lililowekwa la kuingia katika mfumo huo kikamilifu ifikapo mwaka 2012. Waheshimiwa Wajumbe, hii ni changamoto kubwa kwetu, katika kuendeleza radio na televisheni yetu, kwani maendeleo yaliyoonekana ni makubwa ukilinganisha na muda mfupi tangu kuanzishwa kwa *TBC* ambayo zamani ikijulikana kama *TVT*.

Pia, kamati ilitembelea uwanja wa taifa na kujionea matumizi ya teknolojia ya hali ya juu kiwanjani hapo. Kutokana na hayo, kamati inatoa wito kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujenga uwanja mpya wa kisasa kabisa utakaofunika jua na mvua watu wote waliopo badala ya kuwa na paa katika jukwaa la *VIP* pekee kama ulivyo sasa uwanja wetu wa Amaan.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Mhe Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa afya bora ndiyo uhai. Kwa kuzingati hilo, serikali ya awamu ya kwanza ya Zanzibar iliweka matibabu bure mnamo mwaka 1964. Kwa hivi sasa, kutokana na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar, wananchi hulazimika kutoa michango midogo midogo ili kuipa uwezo mzuri zaidi Wizara kutoa huduma zinazohitajika na jamii kwa ubora na ufanisi wa hali ya juu.

Mhe Mwenyekiti, kamati yetu ilifanya ziara katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kujionea haya yafuatayo:

Hospitali ya wagonjwa wa akili *"mental hospital"* imefanyiwa matengenezo makubwa kwa kuezuliwa na kuezekwa mabati mapya na katika sehemu nyengine za hospitali hiyo, matengenezo ya kuta yamefanyika. Pamoja na hayo, hospitali hiyo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wauguzi ambapo wauguzi wapatao 30 wanahitajika ili kukidhi mahitaji halisi ya hospitali hiyo.

Mhe. Menyekiti, nachukua fursa hii kwa niaba ya wanakamati wenzangu kuipongeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara. Ujenzi huo umefanywa katika muda muwafaka kwani jengo lililokuwa likitumika lilikuwa chakavu mno lisilokuwa na haiba yoyote ya kuwa ni Wizara ya Serikali.

Vile vile kamati inatoa pongezi za dhati kwa wizara kwa ujenzi wa jengo jipya la Kitengo cha UKIMWI, Uimarishaji wa Huduma za Mama na Mtoto pamoja na ununuzi wa mashine muhimu ya kuchunguzia maradhi, *CT scan*.

Kwa upande wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, kamati ilishuhudia jengo la kitengo cha viungo bandia ambalo limefanyiwa matengenezo makubwa limekamilika na kuanza kutumika.

Pia, wajumbe walitembelea kitengo cha macho na kuona jinsi vifaa vya kisasa vilivyobanana kwenye chumba kidogo cha upasuaji. Hivyo, kamati inatoa wito kwa serikali kuipatia msukumo zaidi Wizara ya Afya katika mwaka ujao wa fedha, ili iweze kufanya utanuzi wa *theater* hiyo ya macho kwa lengo lile lile la kuwapatia wananchi huduma bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati yetu ilipotembelea katika Hospitali ya Muhimbili Dar-es-Salaam, tulishuhudia mabadiliko makubwa ya majengo, vifaa, utendaji na mfumo mzima wa uongozi wa hospitali. Matumizi ya mtandao unaounganisha baina ya daktari mmoja na mwengine yamesababisha wagonjwa kutibiwa kwa haraka sana. Kimsingi, kamati imejifunza vya kutosha kwamba matibabu bora ndiyo yanayopelekea ustawi wa jamii. Hivyo, tunaiomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutafuta wafadhili wa ndani na nje ili iweze kupiga hatua za kimaendeleo zaidi hadi kufikia kule waliko wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, tukijikita katika matibabu ya saratani, Hospitali ya Mnazi Mmoja bado iko nyuma sana ukilinganisha na wenzetu wa *Ocean road* ya Dar-es-Salaam. Hii inatokana na upungufu mkubwa wa madakatari bingwa na vifaa vya kuchunguzia ambapo wagonjwa hubainika kuwa na saratani katika hatua (*steji*) kubwa za ugonjwa, hali inayosababisha wengi wao kupoteza maisha muda mfupi baada ya kuanza tiba. Kwa mantiki hiyo basi, kamati inashauri kuwekwa kitengo maalumu cha uchunguzi na matibabu ya saratani katika

Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili kupata urahisi wa kujua mapungufu yaliyopo ya vifaa, madawa na madaktari na kupatiwa ufumbuzi muwafaka.

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati ilipotembelea Afisi ya Mkemia Mkuu huko Dar-es-Salaam, ilipata fursa ya kujionea haya yafuatayo:

Mazingira bora ya Afisi hii ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali, yalidhihirisha wazi umuhimu wa kazi anazozifanya kwa Ustawi wa Jamii na Taifa kwa ujumla. Kamati inapendekeza kuwa, Afisi ya Mkemia Mkuu wa Zanzibar iboreshwe zaidi ili kumpa mkemia wetu na watendaji wake moyo wa kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Aidha, kamati inatoa wito kwa sheria ya kemikali kuanzishwa Zanzibar, ili usimamizi wa kemikali uende sambamba kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Maabara ina majukumu ya kutoa mchango wake kwa Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kufanya uchunguzi wa sampuli za:

- Mikojo ya vijana na kubaini walioathirika na madawa ya kulevya na hivyo kutoa ushauri kwa madaktari.
- Kutambua wabakaji kwa kuchuguza sampuli za binti au mama aliyepatwa na mkasa huo.
- Vipodozi na kemikali mbali mbali ili kubainika ambavyo vina kemikali zenye madhara kama zimebaki na ushauri ukatolewa kwa kuviondoa kwenye soko.
- Bidhaa za wajasiriamali wengi wao wanawake na kutoa ushauri wa namna ya kuongeza ubora (unga wa uji wa watoto, juice, asali, nk)

Maabara pia inafanya uchunguzi wa vinasaba (*DNA*) kwa sampuli na vielelezo vinavyohusiana na makosa ya jinai na kutoa ushahidi Mahkamani.
Uwezo wa kuyafanya yote haya umetokana na kuwepo kwa vifaa vya kisasa pamoja na wafanyakazi wenye utaalamu na uzoefu wa kutosha.

Hivyo, kmati inashauri kwamba ni vyema Afisi ya Mkemia Mkuu wa Zanzibar ikapatiwa vifaa bora na vya kisasa ili kuzifanyia kazi sampuli za kemikali zinazopatikana hapa Zanzibar badala ya kuzisafirisha kwenda Dar-es-Salaam ili kupunguza gharama za usafirishaji na uchunguzi.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Mhe. Mwenyekiti, “Elimu ni Ufunguo wa Maisha”. Ni kauli ya wahenga iliyozoeleka. Ili kuwapatia wananchi elimu bora bila ya ubaguzi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitangaza elimu bila ya malipo mnamo tarehe 23/9/1964

kwa nia ya kujenga taifa lililo bora zaidi kwa kuwa na wasomi wengi watakaotumika katika shughuli mbali mbali za maendeleo.

Wizara ya Elimu inaendesha shule za serikali za maandalizi, msingi, sekondari na vyuo. Halikadhalika, wizara inasaidiwa na shule binsfsi za maandalizi, msingi, sekondari na vyuo katika jukumu zito la kutoa elimu kwa watu wa rika zote nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeridhika na imependezewa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha *SUZA* huko Tunguu. Chuo hicho kinatarajia kuongeza kitivo kipya cha Uhandisi "*Engineering"* mara baada ya kumalizika kwa ujenzi wake. Kwa kweli, serikali imepania kujenga haraka chuo hicho ili ifikapo muhula ujao wa masomo majengo hayo yaweze kutumika. Tunamuomba Mola azidishe bidii kwa mjenzi ili amalize na kukabidhi majengo hayo kwa wakati uliopangwa.

Mpango wa Elimu Mbadala kwa vijana waliokosa nafasi ya kujiunga au kuendelea na masomo kwa sababu tafauti, umewapatia fursa nzuri ya kujifunza vijana hao na hivyo kuwatoa katika kundi la wasiosoma na kuwaunganisha na kundi la walioelimika. Hivyo, wizara imechukua nafasi nzuri katika kukuza takwimu za watu wenye elimu nchini "*literacy rate"*, sambamba na kuwajengea uwezo mzuri wa kifikra wahitimu wa elimu mbadala kwa mustakbali wa kujenga maisha yao na taifa kwa ujumla.

Kamati imependezewa na hatua nzuri ya matayarisho ya Chuo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni, ambacho kwa pamoja na kile kilichopo Vitongoji kisiwani Pemba, kitatoa mafunzo ya amali kwa vijana wetu na kupunguza lile tatizo sugu la ukosefu wa ajira nchini. Kwani vijana hao mara baada ya kuhitimu wataweza kuajiriwa na makampuni mbali mbali ya ndani na nje ya nchi au kujiajiri wenyewe kwa vile watapata utaalamu wa kutosha na cheti cha ufundi chenye kutambulika cha *VETA*.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imetakiwa kuyahifadhi na kuyaendeleza magofu na mapango ya kale kwa nia ya kuhifadhi historia ya nchi yetu ili kuirithisha kwa vizazi vijavyo na kukuza uchumi kutokana na watalii watakaotembelea katika magofu na mapango hayo.

Hayo yalielezwa wakati kamati ilipotembelea hifadhi ya Kuumbi na kushuhudia ujenzi wa ukumbi wa kuhifadhi mambo yanayohusu historia ya Kuumbi.

Wizara ya Kazi, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaipongeza Wizara ya Kazi kwa utendaji wake wenye ufanisi wa hali ya juu, kwani imeweza kutekeleza majukumu yake kwa kiasi kikubwa, ingawa ilikabiliwa na upungufu mkubwa wa Fedha.

Wizara kwa kupitia mfuko wa kujitegemea, imeratibu utoaji wa mikopo kwa mfuko wa JK na AK ambapo kamati ilijionea mfano wa *SACCOS* ya Kombeni ambayo imepatiwa fedha hizo na wanaendelea kulipa kidogo kidogo.

Hata hivyo, kutokana na kasoro ndogo ndogo, kamati imependekeza *SACCOS* na watu mmoja mmoja wanaopatiwa mikopo hiyo wabuni miradi madhubuti ambayo itawawezesha kulipa kiasi cha fedha zinazohitajika kwa wakati ili kuwapa fursa wananchi wengine wanaohitaji waweze kukopeshwa. Aidha, wizara imetakiwa kuchukua hatua kali dhidi ya wale wasiolipa fedha hizo, ili iwe funzo kwa wengine ambao wana nia kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7(2)(c)(ii) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kinaweka bayana kuwa, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi litatoa wawakilishi wawili kwa kuingia kwenye Bodi ya Mfuko. Kwa bahati mbaya, kamati iliarifiwa kuwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi limepewa nafasi moja tu ya kushiriki katika Bodi ya *ZSSF* badala ya mbili zilizotajwa katika sheria. Kamati inaomba sana maelekezo ya sheria yafuatwe na hivyo Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi lipatiwe nafasi mbili kama ilivyoelekezwa na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatoa pongezi za dhati kwa wizara kupitia Mfuko wa Kujitegemea ambao umeratibu Jumuiya ya JUWAPO, ambayo imepata mafanikio makubwa kwa kuwapatia ajira wanachama 63. Zaidi ya yote, Kamati inaiomba Serikali kuipatia Wizara hiyo ziada ya shilingi milioni 35 ili bajeti yake ifikie milioni 135 ambazo zitaweza kukidhi angalau mahitaji yake ya msingi.

Mwisho kabisa, natoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wao, tunamuomba Mola Mtukufu awalipe malipo mema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha nakushukuru ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tunakushukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali, sasa kutokana na muda Waheshimiwa Wajumbe mahojiano ya hotuba hii ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii itabidi yaendelee kesho. Sasa naomba niahirishe Baraza hili mpaka hapo kesho tarehe 01/04/2010 siku ya Alhamisi saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 01/04/2010 saa 3:00 asubuhi)